BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NANE

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

Kikao cha Sita – Tarehe 1 Februari, 2010

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Job. Y. Ndugai) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 53

Mfuko wa Kusisimua Maendeleo ya Jimbo (CDCF)

MHE. MBAROUK K. MWANDORO aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wengi wanafahamu kuwa, Sheria ya Mfuko wa Kusimamia Maendeleo ya Jimbo ulipitishwa kwenye Mkutano wa 16 wa Bunge na kupata kibali cha Mheshimiwa Rais kuwa sheria; na kwa kuwa, kumekuwa na ugumu mkubwa kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa kufikisha fedha Wilayani kwa matumizi ya Ofisi za Wabunge:-

(a) Je, ni lini Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge inatarajia kuanza rasmi matumizi ya fedha za mfuko huo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani ya kuhakikisha kwamba, hakutakuwepo na hali ya kukwama kwa mfuko wa *CDCF* katika ngazi ya Ofisi za Mikoa kama ilivyo kwa kasma nyingine?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, ningependa kutoa maelezo ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nielezee tofauti ya Fedha za kuendesha Ofisi za Wabunge na Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo Nchini yaani *CDCF*. Fedha za Kuendesha Ofisi za Wabunge zimekuwa zikitolewa kupitia Ofisi za Wakuu wa Mikoa kupitia (Makatibu Tawala wa Mikoa) na hatimaye kupelekwa kwenye Ofisi za Wakuu wa Wilaya kupitia (Makatibu Tawala wa Wilaya).

Fedha hizi zimekuwa kwa shughuli za ununuzi wa Samani, Shajala, Malipo ya Madai ya Maji na Umeme. Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo ni fedha za Maendeleo na siyo fedha za matumizi mengineyo kama ilivyo kwa fedha za kuendeshea Ofisi za Wabunge. Baada ya ufafanuzi huo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kuanzishwa Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo *(CDCF)* ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuidhinishwa na Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria siku chache kabla ya Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuahirishwa. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa wananchi wengi wanafahamu kuwa Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo ilikwisha idhinishwa na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Spika alizungumzia suala hili katika Mkutano huo wa Kumi na Sita wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa fedha hizo zinapatikana, aidha, fedha hizo zikipatikana zitagaiwa katika jimbo kwa kufuata mchanganuo ulioandaliwa kulingana na vigezo ambavyo vimo ndani ya Sheria iliyoanzisha Mfuko huo wa Jimbo. Utaratibu wa kutumia na kusimamia fedha hizo umebainishwa katika Kanuni za Sheria iliyoanzisha Mfuko huo ambazo hivi karibuni zitatolewa katika Gazeti la Serikali *(GN).(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro na Wabunge wote kuwa fedha za Mfuko huo hazitakwama katika ngazi ya Mkoa kwa sababu utaratibu na Kanuni zilizoandaliwa kuhusu fedha hizo hazitapita ngazi ya Mkoa bali Halmashauri zitapokea mchanganuo wa fedha za kila Jimbo moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha. Aidha, fedha hizo zitaingizwa katika Akaunti Maalum na nafikiri hili mnalikumbuka na zitakazofunguliwa kwa shughuli hiyo nchini na chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo husika. *(Makofi)*

MHE. MBAROUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya

Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini itakumbukwa kwamba wakati tulipofanya *briefing* tulielezwa kwamba suala hili matayarisho yake yamefika hatua ya mbali na kwamba tangazo la Serikali lingetolewa Ijumaa iliyopita. Je, tangazo hilo limetolewa au bado?

Je, Wizara ya Fedha tayari imeshaandaa fedha na lini utaanza rasmi utaratibu huu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi naomba ni-*declare interest* hapa. Hizi fedha na mimi nazihitaji. Kwa hiyo haya maswali yanayoulizwa hapa nayafurahia kwa sababu na mimi kule Siha nina shule zangu ambazo ziko hoi ambazo nataka nikazisaidie shule ya Samaki Maini ina matatizo, shule ya pale Nchali ina matatizo. Kwa hiyo, maswali haya yanaulizwa hapa nayafurahia na nina hakika Mheshimiwa Waziri Mkuu anayafurahia kwa sababu yeye ana jimbo kule. Mheshimiwa Cellina Kombani anayafurahia kwa sababu ana jimbo kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *briefing* iliyofanyika siku ya Jumanne ilikuwa *very clear*. Tulitaka pale ionekane kwamba siku ya Ijumaa ndiyo zitakuwa zimepelekwa. Lkini baada ya mjadala ule ikaonekana muda ule utakuwa ni mfupi mno kwa hiyo tupewe nafasi ili tuweze kuipeleka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nataka nithibitishe hapa kwamba hiyo kazi ya kupeleka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye mwenye dhamana ya jambo hili imeshafanyika na nina hakika kwamba kazi sasa ya kupeleka na kuipata hiyo *GN* kama tulivyosema hapa inafanyika. *(Makofi)*

La pili, linahusu fedha. Mimi siku ile nakumbuka nilikuwepo na nilikuwa sikusinzia. Mheshimiwa Waziri Mkuu alimtaka Mheshimiwa Mustafa Mkullo asimame pale na aithibitishie nyumba hii kwamba hizi fedha zitapatikana au hazitapatikana na Mheshimiwa Mkullo akasema zitapatikana na Mheshimiwa Waziri Mkuu akasema kwamba fedha hizi atahakikisha kwamba zinapatikana. Sasa ninyi mnaniuliza maswali haya niseme hapana halafu mimi nipate mgogoro hapa. Fedha hizi Serikali imeshasema na hao mnaowataja ndio Serikali wameshasema hivyo naomba tuamini kwamba Serikali iko makini na kwamba itafanya hivyo.

MWENYEKITI: Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, swali hili muhimu sana kutakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Katika swali la msingi kuna suala zima la fedha za matumizi ya Ofisi za Wabunge. Mimi sina uhakika kwa sababu sijathibitisha wala sijaziona kwamba kuna fedha katika matumizi ya Ofisi ya Mbunge. Serikali ituhakikishie fedha hizi zipo na zinapitia utaratibu gani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha nilipojibu hapa nilijibu kwa sababu ya kuweza kupambanua kati ya kitu kinachoitwa *Constituent Development Catalyst Fund* na fedha ambazo zinapelekwa katika Ofisi za Wabunge kwa maana ya matumizi ya Ofisi za Wabunge.

Fedha hizi zinaingizwa katika *OC* na kama nilivyoeleza zinaingizwa Ofisi za Katibu Tawala Mkoa na zinakwenda kwa Katibu Tawala wa Wilaya. Inawezekana kabisa kama wanavyozungumza Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba kuna watu wengine ambao hawazioni hazijitokezi humu ninaomba tuelekezwe na tuonyeshwe kwamba ni watu gani. Mimi nafahamu kabisa fedha kwa ajili ya chai pale ofisini kwa ajili ya Mbunge na fedha kidogo kidogo zinazotumika kwa ajili ya kupata samani na vitu vingine ziko zinatengwa na zinaingizwa.

Ninachosema kama wako ambao hawapati hilo mtuletee sisi tufuatilie. *(Makofi)*

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa vile mimi huu ni mwaka wa 15 ndani ya Bunge hili sijawahi kuziona zile fedha. Niliwahi kukarabati ofisi Serikali ikaniandikia kwamba hii Ofisi haifai kwa matumizi ya Mbunge. Sasa Serikali inasemaje juu ya hili na watu wengine ambao hawapati, Serikali haioni kwamba sasa fedha za Ofisi za Wabunge zipite kwenye huu Mfuko wa *CDCF?*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona tu nisimame ili niweze kusaidia kidogo kwenye jambo hili zito. Kwanza nianze na nini tumefanya tangu tulipozungumza mara ya mwisho juu ya *CDCF*. Tuliahidi kwamba kanuni zile zitakamilishwa na baadaye ziende *for printing.*

Kanuni hizo zililetwa nikasahihisha na mimi nikaweka *input* zangu kidogo baada ya pale nimeshazisaini na maelekezo nikatoa ili tuweze kupelekwa kwa *Government Printer* na bahati nzuri *Government Printer* yuko Dodoma tu hapa na nilisaini nafikiri ilikuwa Jumatano au Alhamisi. Kwa hiyo, napenda niamini kwamba ile *printing* itakuwa imefanyika ningekuwa nimepata muda tunge-*cross check.*

Sasa liko hili jambo la msingi ambalo mmeliuliza kuhusiana na fedha za uendeshaji kwa ajili ya Ofisi za Wabunge. Nadhani tukubali kwamba mfumo ulivyo haujasaidia sana kuweza kubainisha kwa uhakika kwanza ni fedha kiasi gani ambazo zimetengwa kwa ajili ya Ofisi ya Mbunge fulani, ziko katika mzunguko wa ujumla wa *OC.*

Kwa hiyo nadhani tutakachoweza kushauriana ndani ya Serikali ni kutafuta namna ya *rainfence* hizo fedha zikishatolewa na kuziwekea utaratibu mahsusi

utakaokuwa unaonyesha dhahiri kwamba hizi ndio fedha na zitatumika kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli ya Mbunge.

Tungeweza tukakubali rai kwamba fedha ziingie katika *CDCF,* lakini tutakuwa tunachanganya majukumu katika mambo mawili ambayo hayafanani sana. Nipeni fursa nijaribu kutafuta huu mfumo mwingine naamini kabisa utafanya kazi sawa sawa. (*Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Esther Nyawazwa simwoni, Dr. Mongella.

Na. 54

Serikali Kulipa Madeni ya Nyuma ya Watoto wa Mazingira Magumu Inayowasomesha

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA(K.n.y. MHE. ESTHER K. NYAWAZWA) aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali Kuu imejitoa kusomesha watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na kuziachia Halmashauri za Wilaya:-

(a) Je, ni lini Serikali italipa madeni ya nyuma?

(b) Je, Serikali Kuu haioni kuwa, imezipa Halmashauri za Wilaya mzigo mkubwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Serikali wa kugharimia Elimu ya Sekondari kwa watoto wanaotoka katika mazingira magumu ulianza kutekelezwa mwaka 2003 kwa lengo la kuwapa fursa sawa watoto wote nchini. Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeendelea kuwasomesha watoto hawa kwa kuzingatia mahitaji yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2008, Serikali iliwalipia ada wanafunzi 23,368 waliokuwa vidato vya II, IV na VI kwa kutumia jumla ya shilingi 3,277,827,052/=. Hata hivyo jumla ya wanafunzi 27,852 wanaosoma kidato cha I, III na V kwa mwaka 2008 hawakupatiwa msaada wowote kwa sababu ya upungufu wa fedha. Fedha zinazotakiwa kuwahudumia wanafunzi hao ni shilingi 5,678,036,000/=. Deni hili litaendelea kulipwa kwa kadri Wizara itakavyopata fedha.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kugatua masuala yanayohusu Usimamizi na Uendeshaji wa Shule za Sekondari kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Halmashauri zimeelekezwa utaratibu wa jinsi ya kugharamia Elimu ya Sekondari kwa watoto wa Mazingira Magumu kama ifuatavyo:-

(i) Kuendesha zoezi la kuwabaini watoto wote wanaotoka katika mazingira magumu katika Halmashauri zao.

(ii) Kuandaa gharama za kuwasomesha na kujumuisha katika Bajeti ya mwaka ya ruzuku ya uendeshaji *(OC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia utaratibu huu, Serikali Kuu kupitia Wizara ya Fedha itaendelea kutoa fedha na Halmashauri zitawalipia wanafunzi watakaohusika. Hivyo, Halmashauri hazitakuwa zimepewa mzigo mkubwa wa kulipia wanafunzi wa mazingira magumu.

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna wanafunzi ambao waliahidiwa na Wizara kwa maandishi kwamba watalipiwa na mpaka sasa hawajalipiwa na wengine wako Kidato cha Nne. Je, Waziri atatoa maelekezo baada ya Bunge hili ili walipiwe waweze kufanya mitihani yao. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA : Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapa na kama ulivyosikia hao wanafunzi ambao tuliowapa kipaumbele ni wale ambao walikuwa wanafanya mtihani. Kwa maana ya wale wa Kidato cha II, IV na VI. Kwa hiyo, hawa wanafunzi sasa kwa sababu watakuwa wameondoka watakuwa wamekuja hawa anaowazungumza Mheshimiwa Getrude Mongella.

Nataka niliambie Bunge lako hapa jumla ya fedha zote zile ambazo ni *arrears* ambazo ni shilingi bilioni 5 na hizi ambazo zinazungumzwa sasa ambazo zinatakiwa ni shilingi bilioni 9 jumla zinafika shilingi bilioni 15. Ninaamini kabisa kwamba kipaumbele kitatolewa kwa wale watoto ambao sasa wanatakiwa kufanya mtihani. Kwa hiyo, sisi tunachofanya kama Wizara ni kufuatilia hizi hela kuhakikisha kwamba zinapatikana ili hawa watoto wanaotakiwa kufanya mtihani kama ilivyokuwa wakati uliopita ziweze kupatikana.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linasema. Je, Serikali haioni kuwa imezipa Halmashauri za Wilaya mzigo mkubwa na kwa kuwa Halmashauri za Wilaya mapato yake ni kidogo sana zaidi ya asilimia 90 wanategemea ruzuku ya Serikali Kuu. Je, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya kuongeza fedha au

kutenga fungu la kutosha ili watoto hawa wanaoishi katika mazingira magumu wote wapate elimu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema mimi nakielewa, anachosema hapa, tuongeze fedha zile katika bajeti. Kitu kinachozungumzwa hapa tunazungumza habari ya kiporo ambacho kimepita na ambacho kama nilivyoeleza hapa tunakitafutia fedha.

Sasa hivi nimetoa maelekezo hapa kusema kwamba katika Bajeti zetu zote zinazokuja kwanza tufanye kazi ya kubaini hao watoto wanaozungumzwa kwamba wako wangapi katika Halmashauri kwa sababu jukumu hili kwa kweli limesharudishwa kwetu sisi kama Halmashauri.

La pili, waingize katika Bajeti zao za Halmashauri katika *OC* ili hao watoto wanaozungumzwa hapa waweze kusaidiwa kama anavyosema Mheshimiwa Lubeleje. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo sasa tumeshalikubali liingie kwa sababu tumeshagatua sasa shule hizi za sekondari kwa maana *Management* na *Administration* ziko chini ya TAMISEMI. Kwa hiyo, tunataka wafanye hivyo ili waingize katika Bajeti yao ili maswali haya tena yasiendelee kuulizwa kama ambavyo yanavyoulizwa hivi sasa.

Na. 55

Gesi Aina ya *Helium* Katika Kijiji cha Nyabusi-Rorya

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI aliuliza:-

Kwa kuwa, Tafiti nyingi zilizofanywa na wataalam wa Madini kutoka Tanzania na nje ya nchi zimebaini kuwa nchi yetu imebarikiwa kuwa na Madini mengi ya aina mbalimbali ikiwemo gesi asilia:-

(a) Je, Serikali ina taarifa kuwa, Wilaya ya Rorya, Tarafa ya Girango, Kata ya Garibe, Kijiji cha Nyamusi kuna gesi aina ya *Helium*?

(b) Kama jibu ni ndiyo. Je, ni lini Serikali itaanza uchimbaji wa gesi hiyo?

(c) Je, ni lini Serikali itawatuma wataalam wake kwenda kijiji cha Nyamusi kuwaelimisha kuhusu faida na athari ya rasilimali hiyo?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi, Mbunge wa Rorya, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina taarifa kuwa Wilaya ya Rorya, Tarafa ya Girango, Kata ya Garibe Kijiji cha Nyamusi kuna gesi aina ya *Helium*. Uchunguzi wa

kijiolojia wa chemichemi za kina kirefu zinazotoa maji moto (*deep seated hot springs)* nchini Tanzania ulifanywa na Idara ya Madini ya wakati huo katika miaka ya 1950 na 1960. Mojawapo ya chemichemi zilizofanyiwa uchunguzi ni ile ya Nyamusi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

Utafiti wa gesi ya *helium* katika Wilaya ya Rorya ulifanyika mwaka 1957 hadi 1958 ambapo *United Kingdom Atomic Energy Authority* ilifuatilia utafiti uliofanyika awali na kutathmini matokeo ya kazi za utafiti ikiwemo michorongo (*diamond drilling*) iliyofanywa na Idara ya Madini. Lengo kubwa lilikuwa ni kubainisha maumbo (*structural control*) yanayosababisha joto ardhi na kuangalia uwezekano wa kuongeza kiasi cha ububujikaji wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iligundulika kuwa gesi ya *helium* ipo mbali sana chini ya ardhi na hutoka nje kupitia mipasuko inayoambatana na misuguano ya miamba. Hakuna mwamba ulionekana kuwa na hifadhi (*reservoir rock*) ya gesi hiyo. Gesi ya *helium* ilikuwa inatoka kwa wastani wa mita za ujazo 1.7 kwa saa na ni mashimo mawili tu yaliyoonesha dalili za kuwa na gesi kati ya mashimo manane yaliyochorongwa. Matokeo ya utafiti pia yalionesha kuwa maji ya chemichemi ya Nyamusi ni maji ya magadi soda (*sodium bicarbonate water*) na yana kasi ya mmiminiko wa maji wa takriban lita 391 kwa saa. Mmiminiko wa gesi ni lita 55 kwa saa ikiwa ni mchanganyiko wa gesi za *nitrogen* na *helium.*

Gesi ya *helium* inapatikana kwa wingi ikiwa ni asilimia 17.9 hivyo kuifanya chemichemi ya Nyamusi kuwa yenye gesi ya *helium* nyingi zaidi kuliko chemichemi nyingine za maji moto zinazopatikana hapa nchini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za utafutaji madini hufanywa na Kampuni na watu binafsi baada ya kupewa leseni. Katika eneo la Nyamusi na maeneo yaliyo jirani yake, Kampuni ya *Mase Exploration and Mining Company Limited* ilipewa leseni ya utafutaji madini PL 3452/2005 tarehe 9 Agosti, 2005 kwa ajili ya kutafuta madini ya aina zote isipokuwa madini ya ujenzi na vito.

Leseni hiyo iliisha muda wake tarehe 8 Agosti, 2008 na baada ya hapo wakajitokeza waombaji wanne ambao ni *Mineral Evaluation, Mobile King Limited*, Thobias Robert Nyalwa na Agricola Fidelis. Maombi hayo yanafanyiwa kazi ili leseni ziweze kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kuzalisha gesi hiyo kwa faida inatakiwa iwe inabubujika kwa kiasi cha mita za ujazo milioni 2.8. kwa mwaka. Utafiti wa awali uliofanywa ulionesha kuwa gesi ya *helium* hububujika kwa kiasi cha mita za ujazo 2 kwa saa kwa siku, ambapo ni kiasi cha mita za ujazo 17,568 kwa mwaka. Kiasi ambacho hakitoshelezi kuzalisha kwa faida. Hata hivyo kunahitajika kufanyika utafiti wa kina wa kutosha ili kuweza kubaini kama gesi hiyo inaweza kuzalishwa kwa faida, kazi ambayo itafanywa na Kampuni itakayopewa leseni ya utafutaji madini.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba ububujikaji wa gesi ya *helium* katika eneo la Nyamusi kwa sasa haukidhi kigezo cha kuanzisha uchimbaji hadi utafiti wa kina utakapofanyika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Jimbo la Rorya kwa ujumla kwamba, Wizara yangu itatuma wataalamu kwenda kuelimisha wanakijiji wa Nyamusi kuhusu faida na athari ya rasilimali hii, ndani ya mwezi huu wa Februari, 2010.

Aidha, nitumie fursa hii kwa niaba ya Wizara ya Nishati na Madini kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala hili kwa karibu na kwa ushirikiano ambao amekuwa akitupa katika Wizara yetu. *(Makofi)*

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Rorya, hususan kijiji cha Nyamusi nataka nimshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zake na kwa jinsi anavyofuatilia na kusimamia sekta ya madini kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja tu. Kwa kuwa amekiri kwamba gesi ya *helium* katika eneo la Nyamusi haitoshelezi kuanzisha uchimbaji na amekubali kwamba utafiti wa kina utafanywa na tukizingatia kwamba tangu Kampuni hiyo ya Uingereza kufanya utafiti ni miaka 52 iliyopita.

Je, Waziri sasa anawaambia nini wananchi wa Rorya kwamba utafiti huo wa kina utaanza lini? Kama ni kuanza mimi nashauri uanze mara moja mwaka huu kwa sababu miaka 52 ni muda mrefu sana. Ahsante. *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru kwa kuipongeza Serikali kwa juhudi ambazo inaendelea katika kusimamia rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba kuna Kampuni 4 ambazo sasa hivi tunazifanyia uchambuzi ili hatimaye tutoe leseni miongoni mwa hizo Kampuni ile ambayo sasa tunaelewa kwamba tukishatoa leseni kwa sababu leseni mojawapo ni kufanya utafiti kwa ajili ya kujiridhisha kwenda hatua ya pili ya uzalishaji tuna imani kwamba zoezi hilo la kufanya tathmini na utafiti wa kutosha kujiridhisha litafanyika ndani ya mwaka huu na naendelea kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuwasiliana naye kama ambavyo tumekuwa tukifanya siku zote.

Na. 56

Ahadi ya Kufikisha Umeme Jimbo la Lushoto

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kufikisha umeme Ngwelo na Mlola kutoka Mlalo; na Malibwi kutoka Kwekanga?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kufikisha umeme Ngwelo na Mlola ni shilingi bilioni 1.7 na mradi utahusisha ujenzi wa kilomita 25 za njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33. Maeneo yatakayonufaika ni pamoja na Vijiji vya Hemtoe, Masale na Makole. Jumla ya tranfoma 4 zenye uwezo wa kVA 100 kila moja zitafungwa katika maeneo husika. Mradi wa kupeleka umeme Malibwi kutoka Kwekanga gharama zake ni shilingi milioni 720.

Mradi huo utahusisha ujenzi wa kilomita 5 za njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 11 na kufunga transforma 2 zenye uwezo wa kVA 100 katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi hiyo ulikwama kutokana na uhaba wa fedha. Hata hivyo, mradi wa umeme katika vijiji vya Ngwelo na Mlola ni miongoni mwa miradi iliyopendekezwa na *TANESCO* kuingia katika Bajeti ya Mfuko wa Wakala Vijijini *(REA)* ya mwaka 2010/2011.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha na ni mategemeo ya Serikali kuwa miradi itatekelezwa pindi fedha zitakapokuwa zimepatikana kutoka *REA* au vyanzo vingine vya fedha kama ambavyo Serikali inaendelea kutafuta.

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu haya ya Waziri. Je, Serikali itaweza au itawezesha sekondari 12, vituo vya afya 4 na zahanati 2 tarafa ya Mlola kuwekewa umeme wa *solar*?

Pili, kwa vile Kata ya Makanya iko mbali na grid je Serikali iko tayari kujenga mtambo wa *mini-hydro* katika Mto Mdando ambao una maji mengi na uwezo mkubwa?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza linahusu uwezekano wa kufikisha huduma ya nishati inayotokana na nguvu ya mionzi ya jua *solar* katika maeneo ambayo ameombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba swali lilihusu nishati inayotokana na umeme wa gridi ya Taifa kwa sasa na nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa miradi ambayo inatekelezwa kwa utaratibu wa nishati inayotokana na vyanzo vingine zaidi ya gridi ya Taifa tuwasiliane

rasmi kwa sababu pia utaratibu wake unatofautiana kidogo na huu ambao tulikuwa tunaongelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Balozi nakuomba tuwasiliane na ofisi yetu sisi na wewe tuone kupitia Kitengo chetu ambacho kinashughulikia huduma hiyo ya umeme kwa kutumia nishati mbadala tuone ni jinsi gani na kutegemea kasma iliyopo kama tunaweza kufanya katika kipindi kifupi kilichobaki au kwa mpango unaokuja katika Bajeti ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la maeneo ya Makanya kwa kutumia *mini-hydro* sasa hivi Serikali kwa kushirikiana na wafadhili ikiwemo Norway na nipende kutumia nafasi hii kuwashukuru sana wahisani hawa wamekuwa wakitusaidia. Tumefanya tathmini ya vyanzo vingi ambavyo vinaweza kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya maji hasa vile vyanzo vidogovidogo na tunatarajia kwamba katika zoezi hili kuna uwezekano wa kupata megawati zaidi ya 390 ambazo zinaweza kuzalishwa kutokana na vyanzo vidogo vidogo vinavyoweza kuzalisha umeme kwa kutumia Nguvu ya maporomoko ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hilo alilosema ni kati ya maeneo ambayo tunayafanyia tathmini lakini taarifa tutazidi kuzitoa kwa umma kwa kadri ambavyo tunafikia hatua kwa kila tunachokifanya kwa sasa. Ahsante sana.

MHE. DANIEL N. NSAZUNGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, kwa kuwa, juhudi za kupeleka umeme huko Lushoto zinafanana sana na juhudi za muda mrefu za kupeleka umeme wa jenereta katika Miji ya Kibondo na Kasulu, nilitaka nichukue nafasi hii kumwuliza Waziri kwa sababu ni Waziri mwenyewe mwenye dhamana, ni lini sasa hizo jenereta za Kasulu na Kibondo yatafika katika Miji ya Kasulu kwa ajili ya kuwasha umeme huo, kwa sababu tayari maeneo kwa ajili ya *TANESCO* tumeshayatenga kwa Kibondo na Kasulu?

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nichukue fursa hii Waziri Mwenye dhamana awaeleze wananchi wa Kasulu na Kibondo waweze kumsikia moja kwa moja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumekuwa tukitoa taarifa nyakati mbalimbali, majenereta hayo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameulizia yanahusu Wilaya ya Kibondo na Kasulu, inahusu Mji wa Sumbawanga pamoja na Nkasi kwa Mheshimiwa Nyami lakini pia Wilaya ya Ngorongoro Loliondo kwa Mheshimiwa Telele majenereta hayo tunatarajia kuyafikisha kabla ya mwezi wa nne na kwa sababu taratibu zote zilishakamilika imani yetu ni kwamba mara tu yatakapofika taratibu za ufungaji zitaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti niendelee kuwaomba wananchi katika maeneo hayo kwa sababu Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkifuatilia kwa karibu sana suala hili, wananchi katika maeneo hayo wavute subira wawe watulivu kwa sababu taratibu zote za utekelezaji wa miradi hiyo zinaendelea vizuri sana.(*Makofi*)

Na. 57

Vifaa vya Maabara - Sekondari ya Mbelei

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wamejitahidi kujenga maabara ya sayansi kwenye baadhi ya shule za skondari kama vile shule ya sekondari Mbelei katika Jimbo la Bumbuli ambao wamejenga vyumba viwili vya maabara lakini hawana vifaa:-

Je, ni lini shule ya sekondari Mbelei itapatiwa vifaa vya maabara ili juhudi zao zisirudi nyuma?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuwapongeza sana wananchi wa Bumbuli kwa kujenga vyumba viwili vya maabara katika shule ya sekondari Mbelei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba uwepo wa maabara shuleni unaongeza ubora wa elimu kwa kuwa wanafunzi huweza kujifunza kwa kufanya mafunzo ya sayansi kwa vitendo (*practicals*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua uwepo wa maabara katika shule hiyo, katika mwaka wa fedha 2007/2008 na 2008/2009 shule ya sekondari Mbelei ilipelekewa jumla ya sh. 6,808,857/= kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa vya maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya kununulia vifaa vya kufundisha na kujifunzia pamoja na vifaa vya maabara kwa shule za sekondari nchini ikiwemo shule ya sekondari Mbelei kadri Bajeti itakavyoruhusu.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, nina swali mmoja la nyongeza.

Kwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imeazimia kuzipandisha hadhi shule za sekondari za Mbelei, Mbumbuli pamoja na Kwimalamba Jimbo la Mheshimiwa

Ngwilizi. Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kuzipa kipaumbele kwa ajili ya ngazi hiyo ya kufundishia sayansi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa pamoja nawapongeza Wabunge wote wa Wilaya hiyo na Mjimbo hayo kwa juhudi zao na mimi mwenyewe nikiwa Mbunge wa viti maalumu Mkoa wa Tanga nimo nitahakikisha hilo linatekelezeka, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la maabara ni karibu nchi nzima kwa shule za sekondari hasa zile za Kata, na kwa kuwa wananchi wamejitahidi sana kujitolea nguvu zao kujenga majengo ya maabara ikiwemo shule za sekondari za Mkoa wa Singida mfano Shelui.

Je, Serikali inaunga vipi mkono wananchi wa nchi nzima ambao wamejitolea kwa nguvu zao kujenga majengo haya na yapo tayari muda mrefu mpaka sasa hayana vifaa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inatambua juhudi za wananchi katika kusaidia hasa ujenzi wa maabara katika shule zetu za Kata. Naomba nitamke rasmi kwa niaba ya Waziri mwenye dhamana ya Elimu kwamba suala la maabara pamoja na vifaa vya maabara tumeliwekea kipaumbele katika Bajeti itakayofuata mwaka 2010/2011 kwa sababu tumetambua mahitaji makubwa ya walimu wa sayansi ni lazima tuanze na maabara kwanza. (*Makofi*)

Na. 58

Muda wa Kustaafu Majaji

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI (K.n.y. MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS aliuliza:-

Kwa kuwa muda wa kustaafu Majaji wa Mahakama Kuu ni miaka 60 na Mahakama ya Rufaa ni Miaka 65; na kwa kuwa nchi nyingine Afrika Mashariki Majaji wa Mahakama Kuu muda wa kustaafu ni miaka 65 na Mahakama ya Rufaa ni miaka 70. Aidha kwa *Supreme Court* ya Uganda muda wa kustaafu Jaji ni miaka 72:-

Je, Serikali itafanya lini mabadiliko ya kikatiba ili kuendana na nchi nyingine za Afrika Mashariki?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba muda wa kustaafu kwa Majaji wa Mahakama Kuu na Majaji wa Rufaa unatofautiana. Aidha muda wa kustaafu kwa Majaji wetu ni mfupi kuliko ilivyo kwa Majaji wa nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na nchi nyingi za Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana kwamba majaji wanapata uzoefu na umahiri wao kazini kwa jinsi miaka yao inavyoongezeka na wengi wa majaji waliostaafu wangeweza kuendelea kufanya kazi za ujaji zaidi ya kipindi chao cha kustaafu. Kwa kuzingatia hayo yote Serikali bado inashauriana na wadau ili kuongeza umri wa Majaji wa kustaafu ili ilingane na nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itaonekana inafaa, Serikali italeta Muswada wa kutunga Sheria kwa ajili hiyo.

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, kwa, kuwa Mwanasheria Mkuu amekubaliana na suala hili na kwa kuwa, Wizara nyingi zimekumbwa na mambo kama haya kama vile Jeshi la Polisi na Jeshi la Ulinzi huwa wanastaafu wakiwa na nguvu zao.

Je, sasa Serikali itakuwa tayari kufanya marekebisho katika Wizara ambazo zinaonekana wafanyakazi wake wanastaafu wakiwa na umri mdogo?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vya kustaafu katika nchi yeyote inategemea pia na *life expectus* katika jamii, hivi sasa umri wa kuishi kwa Mtanzania ni chini ya miaka hamsini na kwa ajili hiyo pia ni jambo la kuangaliwa na katika mchakato huo wa Majaji pia hilo litaangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa ujumla hilo pia ni jambo ambalo tutakapokuwa tunafanya mchakato, Wizara inayohusika inaweza kuyaangalia pia. *(Makofi)*

Na. 59

Mafundi Sanifu Dawa, Mionzi na Maabara Msaidizi Kutotambuliwa na Muundo wa Utumishi Na. 23 wa Mwaka 2002

MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA aliuliza:-

Kwa kuwa watumishi ambao ni Fundi Sanifu Dawa (Pharmaceutical Assistant) Fundi Sanifu Maabara Msaidizi, Fundi Sanifu Mionzi (Radiographer Assistant) wanalalamika vyeo vyao na mishahara yao na haki zao stahili kutotambuliwa katika Muundo wa Utumishi Na. 23 wa mwaka 2007 ya tarehe 11/8/2002, hivyo kutotambuliwa

na waajiri wao na hatimaye kuwekwa katika ngazi ya mishahara TGS badala ya TGOS; na kwa kuwa majibu ya barua ya TUGHE ya tarehe 23/4/2008 yanaeleza kushughulikiwa malalamiko hayo na kwa kuandaa Muundo mpya wa Utumishi.

Je, watumishi hawa wameshatambuliwa na kama bado hawajatambuliwa Serikali haioni kwamba haiwatendei haki?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu**:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mabadiliko ya Muundo wa Utumishi wa kada za afya wa mwaka 2002 Na. 23 kada za Fundi Sanifu Wasaidizi wakiwemo aliowataja Mheshimiwa Mbunge vyeo vyao vilihuishwa na kuwa Wahudumu wa Afya. Aidha, mishahara yao ilibadilishwa kutoka ngazi ya TGS na kuwa TGOS na siyo TGOS badala ya TGS kama anavyodai Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema iliyokuwepo katika marekebisho ya Muundo wa afya wa mwaka 2002, utekelezaji wake ulibaini mapungufu mbalimbali ikiwemo kuwajumuisha mafundi sanifu wasaidizi wenye taaluma mbalimbali katika kundi moja la wahudumu wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mapungufu yaliyokuwa yamejitokeza katika Muundo wa afya wa mwaka 2002, pamoja na sababu nyingine za kuuboresha muundo huo kama vile kujumisha kada za Ustawi wa Jamii baada ya Wizara ya Afya kuunganishwa na Idara ya Ustawi wa Jamii mwaka 2006. Wizara ilifanya marekebisho ya Muundo huo ambao pamoja na maboresho mengine sasa unawatambua mafundi sanifuwa fani zote (dawa, maabara, macho, meno, viungo bandia na mionzi) ambao sasa watatambulika kama wateknolojia wasaidizi (*Assistant Technologists*). Muundo mpya wa kada zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni Na. 1 wa mwaka 2009 na utaanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 1 Julai, 2010.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Naibu Waziri kwenye ngazi hizi bado amenichanganya, watumishi walikuwa kwenye ngazi ya *TGS* wakatoka wawe kwenye *TGOS* lakini sasa ameniambia kuwa hawako tena kwenye *TGOS*, sasa nataka aniambie sasa hivi wapo kwenye ngazi gani?

(b) Kwa kuwa mafundi sanifu hao sasa hivi wameshapandishwa madaraja yao na kuwa *Assistant Technologists* na sasa hivi madai yao yalikuwa yanaanzia mwaka 2002

na Muundo mpya wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Na. 1 wa mwaka 2009 wamesema kuwa wataanza Julai 2010. Je malimbikizo yao kuanzia mwaka 2002 mpaka 2010 watapata?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amesema nimemchanganya labda alikuwa hajanisikiliza vizuri. Lakini nilichosema ni kwamba Muundo wa Utumishi Namba 23 wa 2007 wa tarehe 11 Agosti ndiyo ambao ulipitia yale yote ambayo walikuwa wanalalamikia. Hivyo kuweka katika ngazi ya mishahara *TGS* badala *TGOS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti *sorry*, nilisema kwamba aidha mishara yao ilibadilishwa kutoka ngazi ya *TGS* na kuwa *TGOS* na siyo *TGOS* badala ya *TGS* hapa sijamchanganya kwa sababu yeye alisema badala, sisi tumesema kwamba ametoka ngazi hii kuwa. Lakini hawakuwa *TGOS* badala, kwa hiyo haya maneno mawili badala na kuwa yana maana tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti swali lake la pili, tumesema kwamba wale ambao wamekuwa *Assistant Technologists* kuanzia mwaka 2009 Julai, malimbikizo yao na stahiki zao zitakuwa zinashughulikiwa kadri muundo wa utumishi unavyosema. Kwa namhakikishia Mheshimiwa Mbunge mara itakapoanza kutumika utaratibu utafanywa tuweze kuona kwamba kila mtu anapata haki yake kulingana na muundo unavyosema.

Na. 60

Kupunguza Vifo vya Akina Mama.

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inapigania kwa asilimia kubwa kupunguza vifo vya akina mama na watoto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na upungufu wa zahanati, Vituo vya Afya na Waganga ili kufikia lengo la kupunguza hivyo vijijini:-

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali inapigania kwa kiwango kikubwa vifo vya akina mama na watoto nchini. Katika vita hiyo Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeandaa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi 2007 – 2017 (MMAM). Mpango huu ulilenga kusogeza huduma za afya ya msingu kwa wananchi kwa kuwa na zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya kwa kila kata ifikapo

2017. Mpango huu utasaidia kupunguza umbali kwa akina mama wajawazito na wagonjwa wengine kufikia vituo vya kutolea huduma za afya na hivyo kuyapa huduma wanazostahili kwa wakati.

Aidha, Serikali ina mpango wa kuanzisha huduma za upasuaji mdogo kwa wajawazito *Emergency Obstetric Care (EmOC)* katika vituo vya afya. Katika vituo hivyo kutakuwa na jengo la kusubiria wajawazito wanaotoka mbali (*Waiting Maternity Home)* na ili kuwawezesha kupata huduma kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kuboresha huduma za rufaa inaendelea kutekelezwa kwa kuboresha huduma katika hospitali za Wilaya na Mkoa, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa magari ya wagonjwa na pikipiki za miguu mitatu *(motorbike ambulances)* zenye muundo maalum kwa ajili ya kubeba wajawazito. Katika mwaka huu wa fedha Wizarani kwa kushirikiana na wadau imenunua magari ya wagonjwa 15 na pikipiki 370 zimeagizwa kwa ajili ya kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipango ya kuongeza watumishi ni kama nilivyoelezea Bunge lako Tukufu tarehe 28 Januari, 2010 wakati nikijibu swali la Na. 33 lililoulizwa na Mheshimiwa Paschal Costantine Degera Mbunge wa Kondoa Kusini. *(Makofi)*

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu ambayo ameyajibu. Lakini naomba nifahamu mwaka 1995 kule Cairo katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa, Ibara ya Nane Kifungu cha 21 kulikuwa na makubaliano mbalimbali. Lakini kifungu namba tano kulikuwa na makubalinao ya kupunguza vifo vya akina mama na watoto.

Je, Serikali inatoa kauli gani ya kusema kuwa makubaliano hayo yaliweza kufikiwa kwa kiwango gani mpaka sasa imefikia miaka 15?

Swali la pili, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri kutokana na malengo mbalimbali ya jitihada za Serikali tuweze kwenda naye Tabora baada ya Bunge hili ili aweze kuona jitihada zile zinazofanyika ambazo hazijazaa matunda yoyote na wanawake wale bado wanapata shida na watoto wanaozaliwa kukosa vifaa mbalimbali. Naomba Naibu Waziri aweze kunifahamisha atakwenda na mimi Tabora?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nchi yetu ya Tanzania kama ilivyo nchi nyingine katika Dunia imekubali kabisa ifikapo mwaka 2017 iweze kupunguza vifo vya akina mama na kwamba sasa hivi idadi ya akina mama wanaofariki 578 kati ya wazazi 100,000. Lengo letu itakapofikia mwaka 2017 tuwe tumefikisha 265 kwa wazazi 100,000 hivyo nataka niseme tu kwamba kwa haya yote ambayo nimeyazungumza nia ya Serikali bado ipo pale pale kwa sababu tunategemea itakapofika mwaka 2017 walau tuweze kufikia lengo ambalo tumejiwekea kupungua kutoka 578 na kufikia 265.

Aidha, kufanya hivyo ndiyo maana tumesema kwamba tumeagiza pikipiki za miguu mitatu ambapo baiskeli 370 zitagawiwa katika kila kituo cha afya na ambapo hii baskeli itakuwa na kitanda kitakachoweza kumbeba mama na kumpeleka katika kituo cha karibu ambapo anaweza kupata huduma ya ziada.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsate sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Kamati yetu ya *LAAC* katika ziara zake imezunguka na kukutana na matatizo ya vituo vya afya na zahanati ambazo zimejengwa kwa gharama kubwa lakini hazitumiki na kusababisha kuendelea kupata vifo vya watanzania wengi na Mheshimiwa Waziri anadai kwamba kuna mpango wa kuendelea kujenga vituo na zahanati.

Je, haoni kuendelea kujenga vituo hivi na zahanati wakati vile vilivyopo havifanyi kazi na havina wahudumu wala madawa ni kuendelea kupoteza fedha za Watanzania?

MWENYEKITI: Nampongeza Mheshimiwa Kiwelu kwa vazi lake la kijani.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kweli kabisa ili kuhakikisha kwamba tunapunguza vifo vya akina mama ni lazima na kama alivyokuwa ameagiza Mheshimiwa Rais kwamba kila Mtanzania ni lazima atembee ndani ya km 5 ili aweze kupata huduma za afya.

Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeazimia katika mpango huu wa maendeleo ya Afya ya Msingi najua kabisa kuna hospitali au zahanati ambazo hazina watumishi. Lakini sisi lengo letu ni kwamba ifikapo 2010 idadi tuwe na watumishi kufikia 80,659. Kwa sasa hivi watumishi waliokuwepo ni 48,553 ikiwa ni asilimia 39 tu.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imejipanga tutaendelea kuwa na watumishi wa kuwaweka zile zahanati ambazo hazina watumishi na hata zile tutakazojenga katika mpango huu.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeze. Kwa kuwa Serikali inasema ina mpango wa kuhakikisha tunapata wahudumu wa kutosha lakini mpaka mwaka 2017. Hivi sasa Wilaya ya Urambo ina zahanati 15 zilizojengwa na wananchi hazina wala hazijapata watumishi wala vifaa kwa muda zaidi ya miaka nane sasa.

Zipo nyumba za watumishi ambazo zimejengwa na wananchi wanazipangisha wanachukua kodi; sasa Serikali haioni kama kuendelea kuona wakina mama wanaendelea kufa haioni sababu angalau ya kuchukua watumishi kutoka nje ya nchi ili kuweza kukidhi haja ya zile zahanati zilizojengwa tayari?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na swali la Mheshimiwa Aziza la kuambatana kwenda naye Tabora hukulijibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Sakaya nimalizie tu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally kwamba ninamwahidi kwamba nitapanga nikimaliza Mkutano wa Bunge hili Tukufu basi nitapanga naye na ndani ya wiki tatu nitakuwa nimepanga safari ya kuweza kwenda Tabora.

Sasa nijibu swali la Mheshimiwa Sakaya. Nilipokuwa najibu nimesema kwamba mpango wa maendeleo ya afya ya msingi unaanza 2007 – 2017. Nikasema kwamba wale ambao ninategemea wataalam wafikie 80,659 nimeweka *range* ni mpaka 2017. Sikusema kwamba watumishi watapatikana itakapofika 2007. Naomba anielewe hivyo.

Lakini hata hivyo najua kabisa kwamba kuna baadhi ya zahanati hazina vifaa na suala la kwamba wanapangisha hilo kwa kweli namimi nalisikia hapa lakini kwa kuwa anazungumzia eneo la Tabora nitakapokwenda nitaenda kuona hawa wanaopangisha hayo majengo.

Nataka kusema kwamba anayeagiza vifaa ni Mkurugenzi katika Halmashauri zetu ambazo Bajeti zimewekwa. Wakurugenzi hawa waweke katika mipango yao ili katika zile pesa wanazotengewa waanze kununua vifaa ili waweze kuweka katika hizo zahanati na ziweze kutumika.

Lakini suala la kuajiri watumishi kutoka nje sera yetu ya afya bado hatujafikia lakini hilo ni wazo tunaweza tukalifanyia kazi. Ila mfanyakazi yoyote kutoka nje akija hapa anaweza akapata ajira kwa kutumia taratibu na sheria za nchi na hivyo anaweza kufanya kazi mahali popote. Lakini sasa hivi hatuna mpango wa kuchukua watumishi kutoka nje kwa sababu tunaamin tutakuwa nao wa kuweza kutosheleza.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi. Naomba niongeze tu kidogo katika majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

Kwanza naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Miramba na Mkurugenzi wetu kwa kuunda Kamati ndogo ambayo ilitembea nchi nzima katika vyuo vya afya wakishawishi wafanyakazi wa huduma ya afya kwenda kufanya kazi Urambo.

Kwa maana hiyo juhudi zao zimezaa matunda na naomba kutoa taarifa kwamba katika hizo zahanati zinazozungumzwa hapa 12 zimeshafunguliwa kwa juhudi hizo. Kwa hiyo, ni kweli kwamba Serikali inafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba huduma inatolewa. Hakuna nyumba inayopangishwa katika Wilaya yetu ya Urambo.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la mwisho la nyongeza. Kwa kuwa matatizo haya yote tunayoyazungumza ya kuhusu sekta ya afya, yanatokana na sisi kutokufikia lengo la Mkutano wa Cairo la kuhakikisha kwamba Bajeti ya Wizara ya Afya inaongezwa angalau kufikia asilimia 10 ya Bajeti yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hiyo ingeweza kukidhi mahitaji yote ya watumishi ya vifaa vya zahanati na mambo mengine mengi. Matatizo hayo yako Iramba Mashariki, yako Sikonge, yako kule Peramiho na kwingine kote hapa nchini. Mimi naomba tu labda nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, hivi Azimio hili la Cairo la kuhakikisha utekelezaji wa *goal number* 5 la kupunguza vifo vya wanawake na watoto kwa kuongeza Bajeti ya afya kwa asilimia 10 tunaweza kulitekeleza katika mpango wa Bajeti wa mwaka huu 2010, tukatoa kipaumbele kwa Wizara hii ya Afya kuwa na Bajeti kubwa ili kukidhi mahitaji haya?

MWENYEKITI: Swali hili lilikuwa lijibiwe na Mheshimiwa Mkulo, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii majibu!

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda niwapongeze sana Wabunge wote ambao wameuliza swali hapa wakionyesha kwamba kweli hali ya vituo vyetu lakini vile vile na akina mama ni kitu ambacho kinawakwaza watu wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama Mheshimiwa Jenista Mhagama anavyosema kwamba Bajeti yetu bado haijafikia malengo ambayo yamezungumzwa. Mpaka sasa hivi Bajeti yetu tunayopata ni asilimia 11, tofauti na ile ambayo ilitakiwa ifikie asilimia 15. Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema tu ni kwamba sisi kama Wizara katika mipango yetu huwa tunaomba ile fedha ambayo inaweza ikatusaidia *at least* kufikisha *goal* la kupunguza vifo vya akina mama pamoja na magonjwa mengine.

Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti, sasa sisi hiki ndicho tunachopangiwa, kwa maana hiyo pia tulichopangiwa ndicho tunachotoa. *(Makofi)*

Lakini, nataka kusema kwamba Serikali kwa kweli inatambua kabisa matatizo yote haya ambayo yanazungumzwa na nina imani safari hii kwenye Bajeti na kwa sababu Mheshimiwa Mkulo yuko hapa ambaye ndiye Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwenyewe, basi, atasikia kilio hiki ili aweze kuongeza Bajeti katika Wizara ya Afya na hatimaye hata kama hatutapunguza kwa kiasi kikubwa, lakini *at least* tutakuwa tumeona kwamba ile pesa kidogo imeongezeka.

MWENYEKITI: Ahsante sana na pole Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maswali mengi. Tunahamia Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Na. 61

Ahadi ya Kupeleka Maji Vijijini Mufindi Kusini

MHE. BENITO W. MALANGALILA aliuliza:-

Kwa kuwa wakati Serikali ikijibu swali namba moja (1) katika Mkutano wa Kumi na Sita, ilisema kuwa huwa inatekeleza ahadi ambazo huwajibu Wabunge:-

(a) Je ni kwa nini mpaka sasa Serikali haijatekeleza ahadi zake ambazo imeulizwa na kuahidi mara mbili kuwa itapeleka maji katika vijiji vya Sawala, Mtwango na Kibao?

(b) Kwa kuwa Serikali ilipokuwa ikijibu swali langu la msingi ilisema Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi itapeleka maji katika vijiji vya Mpango, Kitiru na Lufuna. Je, kwa nini ahadi hizo hazijatekelezwa hadi sasa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafahamu tatizo la upatikanaji wa maji katika vijiji vya Sawala, Mtwango, Kibao, Mpanga, Kitiru na Lufuna. Vijiji hivyo vilipata huduma ya maji katika miaka ya 1970, lakini kutokana na ongezeko la watu na uchakavu wa miundombinu ya maji, upatikanaji wa huduma ya maji kwa sasa hauridhishi.

Kwa kutambua ukubwa wa tatizo hilo na umuhimu wa maji kwa wananchi wa vijiji vilivyotajwa, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi katika mwaka wa 1999 ilifanya usanifu wa mradi ambao ungewapatia maji wananchi wa vijiji nilivyotaja kwa gharama ya sh.356,409,000/=. Kwa bahati mbaya Halmashauri haikuweza kutekeleza mradi huo kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 30 Juni, 2008 nikijibu swali namba 126 katika kikao cha 14, Mkutano wa 12, nilieleza kuwa Serikali ilikuwa inaendelea kufanya

mazungumzo na Benki ya Dunia na Washirika wengine kutafuta fedha na uwezekano wa kuharakisha utekelezaji wa miradi wa maji katika Halmashauri zote nchini ikiwemo Mufindi.

Napenda sasa kumwarifu Mhesihmiwa Mbunge na wananchi wa jimbo la Mafindi Kusini kwamba tarehe 27 Julai, 2009, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilisaini mkataba kati yake na Kampuni ya Wataalam Washauri inayoitwa *Service Plan* kwa ajili ya kufanya usanifu wa miradi ya maji ya vijiji 12 vya:- Sawala, Mtwango, Kibao, Ikimilinzo, Kiponda, Luhunga, Igoda, Lufuna na Mkonge (hivi viko Mufindi Kusini) vingine ni Igomaa, Mapanda na Ukami (hivi viko Mufindi Kaskazini). Kazi ya usanifu na maandalizi ya makabrasha ya zabuni ya ujenzi wa miundombinu ya maji sasa inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2010 na kufuatiwa na ujenzi wa miundombinu ya maji.

Katika jitihada nyingine za Serikali, Halmashauri ya Mufindi kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la *Living Water International* imechimba visima virefu vinne katika vijiji vya Kibao, Mtwango, Sawala na Nyororo. Kwa niaba ya Serikali napenda kutumia fursa hii kulishukuru Shirika hilo kwa mchango wake huo mkubwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi imepanga kutekeleza miradi ya maji ya vijiji vya Mpango na Kitiru katika awamu ya pili ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira.

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kwamba, mimi nilikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati iliyofanya *survey* ya mradi huo hadi zikafikia hizo shilingi milioni 365. *Survey* yenyewe ilikuwa inasema kwamba lijazwe lile tanki lililoko pale Sawala kwa sababu Sawala iko juu sana, halafu litapata maji kijiji cha Sawala, Mtwango, Mpanga, Kitilu, Lufuna na Kibao. Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vijiji viko jirani sana kwamba ukijaza maji pale Sawala, nina hakika kabisa vijiji vyote *through gravity system* watapata maji vijiji vyote hivyo. Sasa, kwa kuwa na mimi ni Mhandisi kama Naibu Waziri, yuko tayari kutengeneza Kamati ya Wahansisi wenzangu twende tukaangalie ili mradi huo uweze kuwa mmoja badala ya kuwa Serikali Kuu na Halmashauri?

Swali la pili; nawashukuru sana *Life Water Internationa*l na namshukuru sana Naibu Waziri ametuambia *Life Water International* ndio wahisani wa mradi huu. Kuna mtu mmoja alikuwa anasema yeye ndiye anauhisani, kumbe ni *Life Water International*. Lakini, sasa kwa sababu hiyo *Life Water* wanaendelea kutusaidia, mimi kama Mbunge, Naibu Waziri yuko tayari kuwaomba tena tuendelee kusaidiana kutafuta maeneo mengine ya Jimbo langu la Mufindi Kusini ili waendelee kutusaidia?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi wetu ule kitaratibu tulisema ni mradi wa vijiji 10. Lakini, tuliangalia tukaona kibusara wakati mwingine mradi unatoka kijiji kimoja unakwenda kijiji kingine ukipita katika kijiji kimoja kilicho

katikati siyo busara. Sababu hiyo ndiyo iliyopelekea vijiji vingine vikaongezeka kwa mfano kijiji cha Lufuna. Kwa hiyo, ssa wao wanatekeleza vijiji 12 na sio 10.

Lakini, naomba niseme kwamba Mheshimiwa Malangalila, Mhandisi mwenzangu, wala hakuna sababu yoyote ya kuunda Kamati labda ya Wahandisi kwenda huko. Tutakachokifanya sisi ni kuangalia, huyu Mtalaam Mshauri ambaye sasa anafanya usanifu wa miradi ya maji katika vijiji hivyo anazingatia, kama kuna tanki lipo na mradi ulikuwepo tangu zamani.

Taarifa za awali lazima tuzizingatie, tutakachokifanya ni kuhakikisha tu kwamba Halmashauri ya Wilaya na watalaam walioko pale wanaangalia hayo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyazungumza, na mimi mwenyewe nitafuatilia ili angalau yaweze kuingizwa katika kusanifu mradi huo ili tupunguze gharama ya Serikali badala ya kutekelza miradi mingi. Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hilo linatekelezeka kirahisi bila hata kuunda Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *Living Water International*, sina hakika kama jina ndilo hili *Life Water* au *Living Water*. L akini vyovyote vile hii ni *NGO* ambayo imesaidia kutekeleza miradi ile. Basi nitaomba kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge, tushirikiane na *NGO* na *NGO* nyingine kama zipo katika eneo hilo ambazo ziko tayari kusaidia kutatua tatizo hili ili tuhakikishe kwamba matatizo ya maji katika Jimbo hilo na Wilaya ya Mufindi angalau yanapata ufumbuzi.

Na. 62

Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji

MHE. SAID J. NKUMBA (K.n.y. MHE. LUCAS L. SELELII) aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa wananchi na Taifa kwa ujumla na kwamba kilimo hasa cha umwagiliaji ndicho pekee kinachowezesha kuondoa uhaba wa chakula unaotokea mara kwa mara hapa nchini:-

(a) Je, kuna mpango gani thabiti wa kuhakikisha nguvu inaelekezwa kwenye kilimo cha umwagiliaji?

(b) Je, ni maeneo/mabonde gani yaliyoainishwa kwa ajili ya kuanzisha kilimo kikubwa cha umwagiliaji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imedhamiria kuondoa uhaba wa chakula unaotokana na ukame wa mara kwa mara hapa nchini ili kuchangia kwa kiasi kikubwa

katika usalama wa chakula. Ili kutimiza azma hii, kutimiza Malengo ya Milenia (2015), Dira ya Taifa (2025) na kuchangia katika utekelezaji wa MKUKUTA, Serikali imekwishaamua kwamba kilimo cha umwagiliaji maji mashambani iwe njia ya kutuwezesha kufikia mapinduzi ya kijani na hivyo kutekeleza azma ya kuongeza kasi ya kuleta mabadiliko ya kilimo nchini kupitia kauli mbiu mpya ya Kilimo Kwanza. Ili kutoa msukumo katika umwagiliaji, Serikali kwa nyakati tofauti imekamilisha mipango madhubuti ambayo ama imetoa dira ya maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji au inatekelezwa kihalisi moja kwa moja. Napenda kutoa mifano michache tu ya mipango hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Umwagiliaji *(National Irrigation Development Plan)*, 1994 ambao ulielekeza kuwepo kwa mfumo wa kisheria wa kilimo cha umwagiliaji.

(ii) Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji *(National Irrigation Master Plan)*, 2020 unaoainisha rasilimali za ardhi na maji zilizopo na uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji.

(iii) Programu ya miaka saba ya kuendeleza sekta ya kilimo *(ASDP)* iliyoanza kutekelezwa mwaka 2006/2007 ambayo inakadiriwa kutumia shilingi takribani trilioni 1.97 kuendeleza sekta ya umwagiliaji. Programu hii inayo Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)*, Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji wa Wilaya *(DIDF)* na fedha za Bajeti ya Wizara *(NIDF)*. Asilimia 75 ya fedha za mpango zitatumika kuendeleza umwagiliaji.

(iv)Azma ya Serikali ya Kilimo Kwanza inayotoa mwelekeo wa uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji kwa kuzihusisha sekta za umma na binafsi.

(b) Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji ulibaini maeneo yenye ukubwa wa hekta milioni 2.3 zenye uwezekano mkubwa wa kuendelezwa *(High Irrigation Development Potential)* ambayo yamo katika mabonde ya mito mikubwa kama vile Rufiji, Kilombero, Malagarasi, Wami, Ruvuma na Lukuledi. Kati ya mwaka 2010 na 2015 miradi iliyo katika mabonde hayo na mengine ambayo sikuyataja itatekelezwa. Lakini, ili kupata matokeo mazuri ya haraka, Serikali itaweka kipaumbele cha uwekezaji katika Mikoa sita ya Morogoro, Kigoma, Rukwa, Iringa, Ruvuma na Mbeya , yenye mazingira mazuri zaidi ya kuzalisha mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine litakalopewa umuhimu ni uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga mabwawa hususan katika Mikoa kame ya Dodoma, Tabora, Singida na Shinyanga. Aidha, mabwawa na malambo ya zamani kama yale ya Idudumo, Irambo – Itobo, Mihama na Isikizya yaliyoko Nzega yatakarabatiwa. Tayari Wizara yangu imefanya uchunguzi wa malambo na mabwa wa 125 ambayo baada ya kukarabatiwa au kujengwa upya, yatawezesha eneo la hekta 142,234 kumwagiliwa.

MHE. SANING'O OLE TELELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Ngorongoro

asilimia 75 ya Wilaya hiyo ni kame na kwa hiyo kuna upungufu mkubwa sana wa chakula kila mwaka, lakini katika maeneo ya Kisangiro, Digodigo, Samunge na *Lake Natron* hasa kule Pinyinyi na Ngaresero kuna mabonde na mito ambayo hutiririsha maji mwaka mzima. Je, Serikali ina mkakati gani wa kusaidia kilimo cha umwagiliaji katika maeneo hayo ili kunusuru Wilaya hiyo katika hali mbaya ya chakula?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa eneo la Ngorongoro hususan maeneo aliyoyataja mimi nayafahamu na yana ukame wa mara kwa mara. Labda niseme tu kwamba, nimepata mawazo hivi karibuni kwamba kutokana na uhaba wa fedha tunaopata, basi ni vizuri angalau tuangalie uwezekano, maeneo yote ambayo tunaweza tukajenga mabwawa, tuangalie uwezekano wa kutumia programu zetu mbili kubwa hizi. Tunayo Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji, lakini tunayo pia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo.

Sasa, pale inapowezekana na kama gharama zinazidi kuwa kubwa, basi tutaangalia uwezekano wa kutumia programu zote mbili ili kuweza kutengeneza miradi ambayo inaweza ikahudumia wakulimwa wote kwa pamoja bila kuogopa gharama kuwa kubwa kwa ajili ya kutegemea sekta moja. Nakubali kabisa kwamba eneo hilo linahitaji kuangaliwa kipekee kwa sababu pia watu hawa ni wafugaji na wanahitaji kupewa maji ya kunywa, kulima na kunywesha mifugo yao.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mwaka jana wakati tunapitisha Bajeti, Bajeti ya Maendeleo ya kilimo katika Wizara zote ilikuwa imekaribia bilioni 140; na katika mchanganuo huo ni asilimia nyingi sana ambazo zilikuwa zinategemea wahisani.

Sasa, kwa kuwa uzoefu umeonyesha kwamba fedha za wahisani huwa zinachelewa. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akaliambia Bunge hili ni kiasi gani ambacho kimeishapatikana mpaka sasa hivi ili kuweza kuturidhisha ama kuuridhisha umma kwamba ile azma yetu ya kilimo kwanza inatekelezeka?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo linatakiwa lipate takwimu kwamba ni fedha kiasi gani tayari zimekwisha toka kwa wahisani. Sitakuwa na majibu dakika hii, lakini majibu yatapatikana kwa sababu Wizara ya Fedha ipo na Wizara zetu zipo, nitampa majibu baada ya hapa.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukurru sana. Kwa kuzingatia swali la msingi la Mheshimiwa Selelii, kipengele cha (b) ambacho kinazungumzia kilimo kikubwa cha umwagiliaji; Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hiki ambacho kinazungumziwa kikubwa kitaweza kufanikiwa tu endapo tutafanikiwa ku-*mechanize* kilimo chetu; na kilimo hiki kinahitaji matrekta; na kwa kuzingatia kwamba Sheria ya Manunuzi ambayo Bunge hili Tukufu na Wabunge wote wameiona kwamba ina upungufu. Je, Serikali haioni haja sasa hivi ya kuleta sheria hii ili iangaliwe haraka ili kipengle hiki kinachokwamisha kununua matrekta kwa haraka, kwa kasi kiweze kuondolewa haraka iwezekanavyo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nifafanue kidogo tu kuhusu kilimo kikubwa *(large scale)*. Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania tunalima karibu hekta 255,675 kwa wakulima wadogo. Kilimo cha wakulima wakubwa ziko hekta 55,000 na kilimo hiki kiko chini ya makampuni kama *TPC,* makampuni yale ya maua yaliyoko Arusha na Kilimanjaro na makampuni mengine na yale mashamba ambayo tumeyabinafisha kwa ajili ya wakulima wakubwa wakubwa.

Kwa hiyo, utaratibu wa mikopo kwa ajili ya wakulima wakubwa huo uko tofauti. Wakulima wakubwa tunatarajia kwamba Bajeti yao kwa sehemu kubwa wajigharamie wenyewe na sio Serikali kugharimia wakulima wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kama kuna utaratibu wa kuingiza matrekta ambayo bado una utata kidogo, tutawasiliana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ambayo inashughulikia jambo hili ili tuliangalie.

Lakini nina hakika kabisa kwamba suala la *mechanization* limepewa kipaumbele na Serikali inaliangalia katika utaratibu huo wa kuhakikisha kwamba sio wakulima wakubwa tu, hata wakulima wadogo pia nao wanapata matrekta. Na kwa kuanzia, Halmashauri zote nchini tayari zimeweka kwenye Bajeti na zingine tayari zimeishaingiaza matrekta madogo kwa ajili ya wakulima wadogo.

Na. 63

Madeni ya Wafanyakazi wa Chuo cha Magereza
Ruanda – Mbeya

MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. BENSON M. MPESYA) aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilionyesha dhamira nzuri ya kulipa madeni ya wafanyakazi wake wote waliokuwa wanaidai Serikali:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimelipwa kwa wafanyakazi wa Chuo cha Magereza Ruanda – Mbeya?

(b) Je, mpaka sasa wafanyakazi hao wanaidai Serikali kiasi gani cha fedha?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha fedha za madeni kilicholipwa kwa wafanyakazi wa Chuo cha Magereza, Ruanda – Mbeya ni Tsh. 59,403, 793/= mpaka Juni, 2007.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa wafanyakazi hao bado wanaidai Serikali jumla ya Tsh. 55,745,143/= kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2007 hadi Juni, 2009. Kati ya fedha hizo, madeni ya mwaka wa fedha 2007/2008 yanayofikia kiasi cha Tsh. 24,538,368/= yatalipwa kwa Bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010. Aidha, kiasi cha deni litakalobakia la Tsh. 31,206,775/= litalipwa katika Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2010/2011.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri anasema deni la shilingi karibu milioni 55.7 sehemu yake itaendelea kulipwa hadi mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya mwaka huu yanalipwa hadi 2010/2011.

Mheshimiwa Waziri haoni kwamba huku si kuwatendea haki hao Askari Magereza wa Ruanda – Mbeya pamoja na Askari wengine nchini kote ambao watakuwa wanaidai Serikali akichukulia maanani kwamba pesa yetu inapungua thamani kwa muda mfupi sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa sababu Serikali imekuwa na tabia ya kutokuwalipa watumishi wake malipo yao wanayostahili kwa muda na hususan watumishi wa Sekta ya Ualimu, Afya, Kilimo na hawa sasa Askari, naamini Askari wa maeneo mbalimbali.

Sasa, Mheshimiwa Waziri anatuambia Serikali itakomesha tabia hii lini ya kundelea kutolipa watumishi wake madai ya mara kwa mara na hivyo kupunguza manung’uniko na migomo kwa watumishi katika nchi hii?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge Zambi kwa maswali mawili ya nyongeza. Analolisema yeye, naafiki, nakubaliana na yeye kwamba haya madeni yamekuwepo, ni madeni ambayo kwa kweli hayaleti raha kwa watumishi wetu, kwa wenzetu ambao wanaidai Serikali.

Lakini pia hayo madeni siyo kwamba ni jambo jipya hususan yale ambayo yanahusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Wale ambao wako katika Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama wanafahamu fika, tulizungumza kwa kirefu katika Kamati na tukaeleza hali halisi ilivyo.

Ni kweli haya madeni ni makubwa na nilitamka pale na ningependa nitamke tena hapa kwamba Amiri Jeshi Mkuu ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alieleza kukerwa kwake na kutaka haya madeni yalipwe mara moja. Na hiyo kauli ilifuatiwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda, ambaye alisema haya madeni yalipwe kwa mara moja.

Jibu tulilolipata kutoka Hazina ni kwamba wanakubali kwamba huo mzigo ama deni hilo lipo, lakini tumepata barua ambayo inasema kwamba *CAG* amepewa jukumu la kuhakiki madeni hayo na hayo madeni yakishahakikiwa, ndio inasemekana kwamba yatalipwa. Siyo kwamba Wizara haikuweka msukumo, tumeweka msukumo, hili sualoa liko Hazina na Hazina kwa mujibu wa barua waliyotuletea wametuambia kwamba kabla malipo hayajafanyika ya madeni mengine yote haya hasa ambayo yanahusu Wizara yangu, itabidi wapate uhakiki ambao unatoka kwa *CAG.* Sasa, lini utapatikana huo, hilo anaweza akajibu Waziri wa Fedha.

Na. 64

Changamoto kwa NGOs Kufikia Rasilimali za Ndani

MHE. RIZIKI OMAR JUMA aliuliza:-

Kwa kuwa Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* ilifanya mikutano na wadau ili kubaini changamoto zinazokabili mashirika hayo; na kwa kuwa pamoja na changamoto zilizoainishwa ni uwezo mdogo wa *NGOs* kufikia rasilimali za ndani:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani kushughulikia changamoto hizo?

(b) Kwa kuwa, wadau 383 waliohudhuria mikutano hiyo ni kutoka katika Mikoa ya Dodoma, Arusha na Tanga.

Je, ni lini Serikali kupitia Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* itakutana na wadau wa Mikoa mingine ili nao wapate fursa ya kubainisha changamoto zinazowakabili?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya *NGOs* imeweka mikakati ambayo

itawezesha *NGOs* kufikia rasilimali za ndani. Mikakati hiyo ni pamoja na:- Marekebisho ya Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002 ambayo imebadili tafsiri ya neno *NGO* kutoka *Non-Profit Making* na kuwa *Not for Profit Sharing*.

Kufuatia marekebisho hayo, *NGOs* sasa zinaweza kisheria kuanzisha na kuendesha miradi ya kuzalisha faida ili itumike kuendeleza shughuli zao pasipo kutoa gawio kwa wanachama. Aidha, Wizara imezindua Tovuti inayopatikana kwa anuani ya www.tnnc.go.tz kwa lengo la kuzitangaza *NGOs* kwa kuweka wazi malengo na kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine ambayo *NGOs* zinanufaika kutoka Serikalini ni pamoja na msamaha wa kodi *(VAT).* Hali ya uchumi ikiruhusu, Serikali huendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa *NGOs* pamoja na kuwawezesha kukutana na kubadilishana uzoefu wa namna ya kufanya harambee kutafuta hela.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufanyika kwa mikutano kati ya Bodi na wadau wa sekta ya *NGOs* ni utaratibu wa kudumu ambao Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* imejiwekea. Ukiondoa Mikoa ya Dodoma, Arusha na Tanga ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja, Bodi imefanya mikutano kama hiyo katika Mikoa ya Manyara, Singida na Shinyanga ambako walikutana na wadau 293 katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia kufanya kikao cha 21 cha wadau Mkoani Iringa Mwezi Februari 2010. Utaratibu huu wa Bodi utaendelea ili kuwafikia wadau wote wa Mikoa ya Tanzania Bara.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Swali langu la kwanza, utaratibu huu wa Bodi kukutana na *NGO's* ambao unakwenda kwa mwendo wa taratibu sana, je, unaweza kuwafikia wadau wote hadi umalizikapo mwaka 2010 ili wote waweze kufaidika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa baadhi ya sehemu kumeanzishwa *NGO's* ambazo zinaonekana ni hewa kabisa na haziko kwa maslahi ya walengwa kama ilivyokusudiwa, je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba *NGO's* zote zinazosajiliwa ni sahihi na zipo kwa ajili ya malengo fulani na zile zitakazobainika ni hewa zitachukuliwa hatua gani? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu kwa kifupi Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI – MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba huu utaratibu unaoendelea sasa hivi wa Bodi kutembelea katika Mikoa unakwenda taratibu, hili Baraza limeanzishwa mwaka 2002 na lina vikao mara nne kwa mwaka na kila kikao kinachofanyika, kwa sababu ya upungufu wa bajeti na nyie wenyewe mnaelewa kuwa Wizara yetu, kwa bahati mbaya, bajeti yake ni finyu, lakini tunahakikisha kwamba kwa mwaka mmoja wanatembelea Mikoa mine. Kwa hiyo, kwa utaratibu huu, mimi ninaamini

kwamba tutafikia tu Mikoa yote kwa sababu mpaka sasa tumeshafikia karibu Mikoa kumi hivi. Mwaka huu tutakwenda kwenye Mikoa minne, mwaka kesho Mikoa minne na baada ya muda tutafikia Mikoa yote Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili linalohusu *NGO's* hewa, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna *mechanism* ambayo sasa hivi ndiyo inaanza kufanya kazi. Tuna Baraza la *NGO's* Tanzania ambalo linatengenezwa na wadau, lina wajumbe 30 na hao Wajumbe wanatoka kwenye Mikoa yote Tanzania na kazi yao ni kufuatilia nidhamu na maadili ya *NGO's,* sisi kazi yetu ni kuratibu tu, lakini wao ndiyo wanaotakiwa sasa kuisaidia Wizara kufuatilia *NGO's* ambazo zimesajiliwa kwenye maeneo yao kama kweli zina Ofisi na zinafanya kazi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Ma-*DC* pamoja na Wasajili Wasaidizi ambao wako kwenye Wilaya zetu, nao pia wana jukumu la kufuatilia kwamba *NGO* inayotakiwa kusajiliwa kabla hawajaandikia barua kweli ni *NGO* ambayo inatokana na mahitaji ya wananchi. Naomba pia nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu sisi wote ndio tunaangalia maslahi ya wananchi basi kila ambaye anatumia wananchi kupata maslahi ya aina yoyote, tuhakikishe tunafuatilia kwamba kweli kile wanachokipata na malengo wanayoyasema basi yanafikia walengwa.

Na. 65

Utekelezaji wa Mpango wa kuleta Mawasiliano ya Simu za Mkononi

MHE. JENISTA M. MHAGAMA aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu sasa kumekuwa na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi juu ya kuwapatia mawasiliano ya simu wananchi wa Muhukuru, Mgazini, Ifinga na Ndongosi katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Jimbo la Peramiho:-

(a) Je, ni lini sasa utekelezaji huo utafanyika?

(b) Je, ni sababu zipi zinazochelewesha utekelezaji wa mpango huu mpaka sasa?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, Wizara kwa kushirikiana na kampuni ya simu ya *VODACOM*, imefanya tathmini ya awali katika maeneo ya Muhukuru, Mgazini, Ifinga, Ndongosi na maeneo ya jirani, kwa lengo la kufikisha huduma ya mawasiliano. Kwa hivi sasa, kampuni hiyo inaendelea na hatua za

utekelezaji kulingana na bajeti yake ya mwaka 2010/2011 ambayo itathibitishwa na kuanza kutumika mwezi April, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya simu ya *TIGO*, inaendelea na mpango wake wa kupanua wigo wa mawasiliano hususan katika maeneo ya vijijini. Kampuni hiyo, itatoa kipaumbele kwa maeneo ya Muhukuru, Mgazini, Ifinga na Ndongosi katika tathmini ili kuona uwezekano wa kuweka mnara wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni za simu za *ZAIN*, *TIGO* na *ZANTEL* zimeyaweka maeneo ya Muhukuru, Mgazini, Ifinga na Ndongosi katika mipango yake ya kufanya tathmini ili kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshwaji wa utekelezaji wa Mpango wa Mawasiliano katika baadhi ya maeneo nchini, yakiwemo maeneo ya Jimbo la Peramiho, unatokana na ukweli kwamba, Makampuni ya simu hufanya biashara na huwekeza katika maeneo ambayo yataweza kuwaletea faida. Hata hivyo, Serikali inaendelea na itaendelea na juhudi zake za kuyahimiza makampuni haya kufikisha mawasiliano kwenye maeneo mengi hususani ya vijijini, kwa kuwa wananchi wengi wako vijijini, tuna uhakika makampuni haya hatimaye yatapata faida na mawasiliano yatatoa chachu kwa maendeleo ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi ya kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kutoa takwimu muhimu ya matumizi ya simu nchini. Mwaka 2000, watumiaji walikuwa 284,000, mwaka 2005 waliongezeka kufikia 3.12 milioni na ilipofika September 2009, watumiaji wa simu walikuwa wamefikia 16.33 milioni, kwa maana hiyo katika kila Watanzania 100 watu 39 wana mawasiliano ya simu, haya ni maendeleo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Mhagama, kwa jinsi anavyosimamia maendeleo ya wananchi wa Peramiho katika sekta ya mawasiliano na hata katika kuhakikisha kwamba wanapata maji safi na salama na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, ninamhakikishia yeye na wananchi wa Peramiho ushirikiano wa Serikali.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Profesa Mwandosya, kwa majibu yake mazuri kabisa aliyoyatoa hapa. Pia nimpongeze kwa jinsi anavyofanya kazi zake vizuri katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ndani ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkutano huu wa Bunge, tarehe 29 tumepitisha Sheria mpya ya Elektroniki na Posta na Sheria hiyo inatoa nafasi kwa makampuni ya simu kushirikiana katika kutumia minara kwa pamoja ili kurahisisha mawasiliano je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba sasa ni wakati muafaka kwa Sheria kuyashawishi yale makampuni badala ya kutumia muda mwingi wa utafiti na upembuzi yakinifu, kuanza kushirikiana katika minara iliyo karibu ili kufikisha mawasiliano katika

maeneo hayo niliyoyataja ya Mgazini, Ndogosi, Muhukuru, Ifinga na kwingineko katika Jimbo la Peramiho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, makampuni haya yamekuwa yakifuata maeneo ambayo yana biashara, eneo la Muhukuru, ni eneo la mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, biashara imeshamiri na kwa ripoti za *TRA*, sasa hivi mapato yamekua sana kwa sababu ya kufungua mpaka wa Tanzania na Msumbiji, lakini eneo la Mgazini pia ni hivyo hivyo, je, haoni kwamba haya ninayozungumza kila siku yanaashiria kabisa uwepo wa biashara maeneo hayo na sasa ni wakati muafaka wa kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo niliyoyasema?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napokea pongezi alizozitoa, nazipokea kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Pili kuhusu Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta kuweka hali nzuri ya uwekezaji kwa maana ya wawekezaji kushirikiana katika kutumia minara, ni kweli Sheria hii itatusaidia sana na tunafikiri itapanua wigo wa wale ambao hawajapata nafasi ya kuwa katika wigo wa kupata mawasiliano na kupunguza gharama. Kwa kweli ushirikiano sasa ni lazima na siyo wa kuchagua kwa upande wao na kweli makampuni haya yatafaidika na sisi kama wananchi, tutafaidika kwa kupata mawasiliano yaliyo ya haraka zaidi na vilevile kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kibiashara ambayo ameyataja hasa eneo la Mkinda, kata ya Muhukuru ambayo kwa kweli iko mpakani kati ya Tanzania na Msumbiji, hili ni suala la muhimu sana kwa sababu ya biashara kati ya Tanzania na Msumbiji. Eneo la Mgazini ambalo ni ghala la chakula la Taifa kwa sababu mahindi yanapatikana kwa wingi huko, kwa hiyo, hii ni sehemu ya biashara na Kata ya Ifinga ambayo hajaitaja lakini amenitaarifu kwamba iko katika hifadhi ya wanyama na kuna vitalu vya uwindaji kule, kwa hiyo biashara ipo, sababu zote hizi zinatupelekea kuamini kwamba haya makampuni yatapeleka mawasiliano huko mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeneo ambayo siyo ya kibiashara nchini, basi ule Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ambao Bunge lako Tukufu lilipitisha mwaka 2007, utasaidia kuyawezesha Makampuni haya kuyafikia maeneo ambayo kawaida yasingeweza kufikiwa.

MWENYEKITI: Kwa sababu ya muda, naomba niende kwenye swali la mwisho la leo, nalo ni la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila.

Na. 66

Kuboresha Mawasiliano ya Mtandao wa *ZAIN* Kalambo

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA aliuliza:-

Kwa kuwa usambazaji wa mawasiliano katika Jimbo la Kalambo kupitia mtandao wa *ZAIN (CELTEL)* bado haujafikia kiwango kizuri:-

(a) Je, ni lini kampuni hiyo itasambaza huduma hiyo katika maeneo ya mipakani ya Kata za Katete, Sopa, Legezamwendo na Kalembe ili kuboresha ulinzi na usalama?

(b) Je, marekebisho yatafanywa lini ili maeneo ya Kasanga, Mkowe na Matai ambapo kumetokea mtandao kusumbua mara kwa mara sasa mawasiliano yawe mazuri?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *ZAIN* imeandaa utaratibu wa kufanya tathmini ili kuboresha mawasiliano katika maeneo ya Kata za Katete, Sopa, Legezamwendo na Kalembe. Aidha, ripoti ya tathmini hiyo itakayotumika kuboresha mawasiliano katika Kata husika inatarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Machi, 2010.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zinazofanya mawasiliano ya simu kutokuwa mazuri pamoja na nyinginezo ni kama ifuatavyo, eneo linalolengwa kuwa mbali na *station* ya mawasiliano au mbali na mnara, jiografia ya eneo kama vile milima na mabonde na vilevile hali mbaya ya hewa. Hata hivyo, kutokana na mtandao kusumbua mara kwa mara kwenye maeneo ya Kasanga, Mkowe na Matai, Kampuni ya simu ya *ZAIN* inafanya utafiti utakaowezesha kubaini chanzo cha matatizo hayo kwa lengo la kuyarekebisha na hatimaye upatikanaji wa huduma bora zaidi za mawasiliano katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwananzila anatekeleza vilivyo jukumu lake la kuhakikisha kero, matatizo na changamoto za maendeleo ya Kalambo zinaifikia Serikali kupitia Bunge lako Tukufu, nampongeza na kumhakikishia ushirikiano wetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nyami, swali la nyongeza na litakuwa la mwisho.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali madogo sana ya nyongeza mawili. Kwa kuwa tayari kwenye Kata ya Katete na Sopa *VODACOM* wamekwishafika lakini zile kata nyingine zilizotajwa hapo bado hawajafika, je, *VODACOM* na *ZAIN* pamoja na mipango mizuri iliyopo, hawawezi wakaendelea kuweka mtandao katika Kata za Legezamwendo, Kalembe, Kapozwa ambayo ipo Kalambo na vilevile wasisahau maeneo kama vile Yakala, Wapembe pamoja na Ninde yaliyoko eneo la Ziwa Tanganyika upande wa Jimbo la Nkasi? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile *ZAIN* wanafanya utafiti kujua tatizo ni nini hasa katika maeneo ya Kasanga, Mkoi na Matai lakini matatizo hayo hayo yako katika kata ya Kate na Mkwamba yaliyoko katika eneo la Jimbo la Nkasi, je, huko nako hawawezi wakafanya utafiti huo?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo aliyoyataja ya kandokando mwa ziwa Tanganyika hasa yaliyo katika Wilaya ya Nkasi, naomba kumhakikishia kwamba tumelipokea ombi lake na tutalifikisha katika Mkampuni hayo. Mimi nina uhakika ukiangalia tulikotoka mwaka 2000 ambapo tulikuwa na wenye simu 284,000 na sasa milioni 16 nadhani kufikia milioni 40 haitachukua muda mrefu, kwa hiyo, tutafanya kila juhudi ili Watanzania wote waweze kufikiwa na mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuhusu kufanya utafiti katika maeneo ambayo usikivu wake si mzuri sana katika eneo la Nkasi. Tutayataarifu makampuni haya yafanye hivyo kwa sababu ni kwa faida yao wasipofanya hivyo basi wanakosa biashara lakini si kwa Nkasi tu vilevile kwa Rungwe Mashariki na maeneo mengine nchini.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha na muda umepita kidogo, sasa matangazo. Tangazo la kwanza ni kuwakumbusha Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Bunge kwamba saa tano wanahitajika ukumbi wa *Speaker*, kwa ajili ya kikao cha Kamati ya Uongozi.

Taarifa nyingine ya kikao ni kutoka kwa Mheshimiwa Mussa Zungu, Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo leo saa tano asubuhi, sina uhakika kama mnakibali cha *Speaker* kwa sababu tunapojadili Sheria, huwa tunapenda vikao vyote vya Kamati viwe saa saba labda pale mnapokuwa na kibali cha Mheshimiwa *Speaker*.

Mheshimiwa George Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, leo saa saba, katika Ukumbi wa Pius Msekwa, kutakuwa na kikao ili kuangalia Muswada wa *National Security* ***Councel***, kwenye kumbi zile ndogo.

Mheshimiwa Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Nishati na Madini, anaomba Kamati hiyo ya Nishati na Madini, leo saa saba mchana wakutane Ukumbi namba 227.

Mheshimiwa Jecha, anatangaza kuwa Kamati ya Bunge ya Hesabu ya Mashirika ya Umma, wakutane ukumbi namba 231, kwa vile mnakibali cha Mheshimiwa *Speaker*, mnaombwa mkutane saa tano na nusu.

Kamati ya Maliasili, Ardhi na Mazingira, wanaombwa wakutane saa tisa alasiri ukumbi namba 219.

Baada ya matangazo haya ya kazi sasa wageni, Waheshimiwa Wabunge, kuna mgeni wa Mheshimiwa Dr. James Wanyancha ambao ni Mheshimwa Zacharia Kisiroti, Diwani Kata ya Kiambai kule Serengeti, kama yupo asimame, ahsante sana na Mheshimiwa Michael Kunani, ni Mwenyekiti wa Kipindi kilichopita kutoka Rubanda. Ahsante sana Mwenyekiti wa Rubanda, karibu sana, niliwahi kuwa mwanakijiji wake miaka hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Slaa, ana wageni wake ambao wanatoka Shirika la Mtakatifu Augustino Basutu kule Hanang, naomba wasimame wote ikiwa ni pamoja na Sister Justina, Sister Eva Kimario, Fratel Fransisco Mbuja, Fratel Sirupisi Saru, ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna wageni wa Mheshimiwa Professor Raphael Mwalyosi, mgeni wake ni mmoja, mwanafunzi wa *College of Education,* Chuo Kikuu cha Dodoma, mwaka wa pili, ndugu Luka Chaula. *(Makofi)*

Tuna wageni 23 wa Waheshimiwa Wabunge Al-Shymaa Kwegyir, Margreth Mkanga na Zuleikha Haji, ambao ni viongozi wa *Tanzania Albino Society*, tunaomba msimame, ahsanteni sana na karibuni sana. Bunge hili linatambua juhudi kubwa sana ambazo mnazifanya na liko pamoja nanyi katika mapambano yaliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Wageni wa Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, ni wa tatu, Ndugu Mafige Kokuretera Nyamtondo, Afisa Ushirika wa Wilaya ya Bukombe, Ndugu Martha Luhahula, sasa huyu Martha hakuwekewa wadhifa wake, kwa hiyo na mimi naacha hivyo hivyo yuko na Ezekiel Samuel kutoka Jimboni kwake. Ahsante sana, mnakaribishwa sana hasa Martha, nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Katibu kwa hatua inayofuata!

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa Mwaka 2009 *(The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Bill, 2009*

(Kusomwa Mara ya Pili)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. *(Makofi)*

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya mwaka 2009 *(The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Bill, 2009* pamoja na marekebisho yaliyogawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge, sasa usomwe kwa mara ya pili. Muswada huu ulisomwa kwa mara ya kwanza Bungeni tarehe 27 Januari 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada huu, ni kutunga Sheria mpya ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi yaani *The Architects and*

Quantity Surveyors Registration Act ambayo itafuta Sheria ya Ubunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Sura ya 269, inayotumika hivi sasa ili kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Bodi na hivyo kuiwezesha kufanya kazi kwa ubora na ufanisi. Sheria inayotumika hivi sasa, ilitungwa mwaka 1957 kwa lengo la kusimamia, kuendeleza na kuratibu mienendo na ubora wa shughuli na taaluma za Wabunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi nchini tangu wakati huo, Sheria hii imefanyiwa marekebisho mwaka 2001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unakusudia kuboresha majukumu ya Bodi, usimamizi wa kisheria katika usajili wa wataalamu wa ndani na wataalamu wa nje kutoka kwenye taaluma za ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi pamoja na Makampuni yanayotoa huduma za taluuma hizo. Muswada wa Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, umeoanishwa na Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003 ambayo imefafanua vizuri kuhusu kufanyiwa mapitio ya Sheria za Taasisi zilizopo chini ya Sekta ya Ujenzi ili ziweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Muswada huu umelenga kupanua wigo wa usajili ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Bodi kutambua na kuratibu watu waliopata mafunzo ya kati ama *intermediate qualifications* katika fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi. Hivyo Muswada huu ukipitishwa na Bunge, utakuwa nyenzo muhimu itakayowezesha utekelezaji wa maelekezo yaliyomo kwenye sera hii kwa kuyapa nguvu za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kuu za Muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu saba pamoja na majedwali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza, inaweka masharti ya awali kama jina la Sheria pamoja na tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada ili kurahisisha uelewa na utekelezaji wa Sheria yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya Muswada, inapendekeza kuanzishwa kwa Bodi na majukumu yake. Uteuzi wa nafasi ya Msajili na ukomo wa muda wa kukaa kwenye ofisi pamoja na uteuzi wa maofisa wengine wa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya Muswada, inafafanua masuala ya usajili wa wataalamu wa ndani na nje ya nchi kutoka kwenye taaluma za Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi na Makampuni yanayotoa huduma za taaluma hizo.

Katika sehemu hii ya Muswada Msajili wa Bodi amepewa jukumu la kuhifadhi daftari la kumbukumbu au regista ya wataalamu wa Ubunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na makampuni yao pamoja na kutangaza kwenye gazeti la Serikali.

Sehemu hii ya Muswada pia imeainisha taratibu za wataalamu wa nje ya nchi kufanya kazi Tanzania na taratibu za kuwatambua Wataalamu wa Kitanzania waliosajiliwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika sehemu hii ya Muswada, Msajili wa Bodi amepewa uwezo wa Sheria chini ya kifungu cha 21 cha Muswada kutoa zuio ama *stop order* pale ambapo Bodi itabaini kuwa kazi za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi zinaendeshwa na makampuni ambayo hayajasajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ya Muswada, inahusu kufuta au kusitisha usajili pale ambapo Mbunifu Majengo au Mkadiriaji Majenzi, atashindwa kutoa taarifa za anuani yake ya sasa kwa Msajili ndani ya miezi sita kuanzia tarehe ya uchunguzi kuhusu Kampuni yake umefanywa, kushindwa kulipa ada kwa miaka miwili mfululizo, kushindwa kufuata taratibu za usajili, kubainika kuvunja kifungu chochote cha Sheria au kufariki. Sehemu hii pia inaweka taratibu za kufanya uchunguzi, kukata na kusikiliza rufaa pale inapotokea kuwa mtu anakuwa hakuridhishwa na maamuzi yoyote yanayotolewa na Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ya Muswada, inapendekeza taratibu za Kisheria kuzuia Wabunifu Majengo au Wakadiriaji Majenzi kufanya kazi chini ya taaluma zao au kuanzisha Makampuni wakiwa hawana sifa zinazolingana kwa mujibu wa Sheria. Aidha, sehemu hii inapendekeza adhabu kwa watakaokiuka taratibu zilizobainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita ya Muswada, inahusu shughuli na masuala ya kifedha ambapo vyanzo vya fedha vya Bodi, taratibu za ukaguzi wa mahesabu, uwezo wa kuwekeza na uwasilishwaji wa taarifa za hesabu za Bodi Bungeni zimeainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya saba ya Muswada, inahusu masuala madogo madogo yanayohusu utekelezwaji wa Sheria hii ikiwa ni pamoja na makosa na kutoa adhabu kwa yeyote atayebainika kuvunja Sheria. Atakayetenda kosa lilioainishwa katika sehemu hii ya Muswada, atatozwa *fine* isiyopungua shilingi milioni tatu lakini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miaka mitatu au vyote viwili kwa pamoja. Aidha, Sheria inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana kutunga Kanuni na Sheria ndogondogo ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria hii. Sehemu hii ya Muswada, pia inapendekeza kufuta Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Sura ya 269.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu, una majedwali mawili, jedwali la kwanza linahusu muda wa Bodi kukaa madarakani pamoja na taratibu na mwenendo wa mikutano ya Bodi. Jedwali la pili linahusu aina ya majengo ambayo yanapendekezwa kusimamiwa na wataalamu wa Ubunifu na Ukadiriaji Majenzi wakati wa ujenzi. Aidha, Bodi imepewa uwezo wa Kisheria wa kupanga thamani ya Majengo ambayo wataalamu watatakiwa kutumia.

Ni matumaini yangu kwamba Muswada wa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa 2009 ama *(The Architects and Quantity Surveyors*

(Registration) Bill,2009 utajadiliwa na kuboreshwa ili kukidhi mabadiliko ya kisera, kiuchumi na kiteknolojia yanayoendelea kutokea nchini na Duniani katika masuala ya ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi. Kwa mantiki hiyo, suala la usimamizi, uratibu na uendelezaji wa taaluma hizi, litafanyika chini ya Sheria iliyobora na hivyo kuleta ufanisi katika sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nichukue nafasi hii nitoe shukrani zangu za dhati kwa wadau mbalimbali walioshiriki katika kutoa maoni yao katika mkutano wa wadau uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 18 Januari, 2010. Maoni na ushauri wao umesaidia kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutambua mchango wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Uchambuzi wa kina wa Muswada huu uliofanywa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu ndiyo uliowezesha Muswada huu uweze kuwasilishwa leo hii mbele ya Bunge lako Tukufu, tunaishukuru sana Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati, kwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuandaa kwa ufasaha na kwa umakini mkubwa Muswada huu pamoja na orodha ya marekebisho yaliyogawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge. Namshukuru pia Naibu Waziri wa Wizara yangu Mheshimiwa Hezekia Ndahani Chibulunje, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu kwa ushirikiano wao katika kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa ninayo heshima ya kuwasilisha Muswada wa Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa Mwaka 2009 *(The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Bill, 2009* ambao unapendekeza kufuta sheria iliyopo hivi sasa ijulikanayo kama *The Architects and Quantity Surveyors Registration Act, Cap 269.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kisha lipitishe Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana Waziri wa Miundombinu, sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Kamati iliyojadili Muswada huu.

MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.N.Y. MHE. MOHAMED H. MISSANGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Miundombinu, kwa ruhusa yako, naomba kuchukua nafasi hii, kipekee, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uhai na nguvu hadi leo hii na kuendelea kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa ufanisi. Pia naomba kuchukua nafasi hii, kuwatakia heri ya mwaka mpya, wananchi wangu wa Jimbo la Karagwe na kwa kuendelea kunipa ushirikiano mzuri hasa katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi nami nawaahidi kwamba sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nipongeze vyombo vya habari vya Karagwe hasa Radio FADECO ambayo iko Jimboni kwangu Karagwe kwa huduma yao nzuri hasa ya kuendelea kuwahabarisha wananchi Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo, sasa naomba kusoma taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu na maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi wa mwaka 2009 *(The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Bill, 2009).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa Mwaka 2009 *(The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Bill, 2009)* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(5), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii, kuungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole, kwa misiba ya wenzetu walioiaga dunia hivi karibuni. Aidha, naomba nitoe pole kwa wenzetu waliokumbwa na maafa na ajali mbalimbali na wengine kupoteza mali na maisha yao; kama vile maafa ya Same na Kilosa. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze Roho za Marehemu wote mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa Bunge wa Kumi na Saba ulipomalizika, uliipelekea Kamati hii kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Sheria ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa Mwaka 2009 *(The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Bill, 2009),* napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilitekeleza kazi hiyo kama ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii, kwa michango na ushirikiano wao wakati wa kuujadili na kuuboresha Muswada huu. Aidha, naomba niwashukuru Wadau wote kwa michango yao ambayo imesaidia kuuboresha Muswada huu na kuwa kama unavyoonekana. Tunawashukuru wote walioshiriki katika Mjadala *(Public Hearing)* kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wafuatao ndio wanaounda Kamati ya Miundombinu, naomba niwataje kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga, Mwenyekiti na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Pascal Constantine Degera, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Paul Paul Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mheshimiwa Dkt. Getrude Ibengwe Mongella, Mheshimiwa Alhaj Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi. *(Makofi)*

Muswada huu unafuta Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi *(The Architects and Quantity Surveyors Registration Act, 1997)*, Sura ya 269, ambayo ndiyo inatumika kwa sasa. Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mwaka 2001; ambapo bado imeonyesha upungufu mkubwa katika utendaji wa Bodi, hivyo kutokidhi mahitaji ya sekta kufuatana na mabadiliko ya wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Muswada; kutungwa kwa sheria hii kutaiwezesha Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kuwa na nyenzo ya kisheria ya kufanyia kazi zao kwa mujibu wa sheria iliyounda Bodi hiyo. Aidha, itakuwa mwongozo kwa Wasimamizi na kwa Watumiaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii mpya inatarajiwa kuwa suluhisho katika baadhi ya Sheria zinazotumika sasa, ambazo zilikuwa na upungufu katika utendaji wa Bodi wa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007; Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wadau husika wa Muswada wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa Mwaka 2009 na kupata maoni na mapendekezo yao. Maoni ya Wadau hao yaliwasilishwa mbele ya Kamati tarehe 18 na 15 Januari, 2010 katika vikao vilivyofanyika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawapongeza kwa dhati Wadau wote walioshiriki kikamilifu katika kuuboresha Muswada huu, ambao ni kutoka Mashirika, Makampuni, Taasisi na Sekta mbalimbali za Kiserikali na zisizo za Kiserikali kama vile *Architects Association of Tanzania* (AAT), *Tanzania Institute of Quantity Surveyors* (*TIQS*), Bodi ya Wahandisi Tanzania (*ERB*), Bodi ya Wakandarasi Tanzania (CRB), Baraza la Ujenzi la Taifa (*NCC*), *Institute of Engineers Tanzania* (IET), Chuo Kikuu cha

Ardhi (*ARU*), Taasisi ya Ufundi Mbeya (*MIST*), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (*VETA*), *Public Procurement Regulatory Authority* (*PPRA*), *Town Planners Registration Board, Occupational Safety Health Authority, Contractors Association of Tanzania* (*CATA*), *Tanzania Civil Engineering Contractors Association* (*TACECA*), Baraza la Hifadhi ya Mazingira Tanzania (*NEMC*) na Shirika la Msaada wa Kisheria (*NOLA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu, chini ya Wizara ya Miundombinu, ilifanikiwa pia kushirikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kuujadili na kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; Sheria hii ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, ni muhimu katika sekta ya ujenzi, kwa kuzingatia kwamba sekta hii inakua kwa haraka. Sheria inatoa fursa kwa Wataalamu wa sekta hii kuzingatia taratibu na sheria zilizopo ili kujenga majengo yanayozingatia utaalamu na vigezo vilivyowekwa. Kamati inaishauri Serikali iweke utaratibu maalum wa kuwaelimisha wananchi katika Mikoa, Wilaya na Halmashauri zao kuhusu umuhimu wa kuwatumia Wataalamu wa Bodi hii katika hatua zote zinazohusu ujenzi wa nyumba na majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa taaluma ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ni muhimu sana, Kamati inaishauri Serikali kuongeza idadi ya Wafanyakazi katika Bodi hii ili iweze kusimamia vyema kazi za ujenzi na majengo. Kukua kwa sekta ya ujenzi na kuibuka kwa majengo makubwa yasiyofuata ushauri wa kitaalamu, ni hatari kwa maisha na mali za watu. Ipo mifano ya majengo yaliyoporomoka ambayo hayakujengwa kwa utaalamu na viwango vinavyotakiwa. Sheria hii itasaidia kwa kiwango kikubwa kudhibiti ujenzi holela na hatarishi kwa maisha na mali za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii pia inatilia mkazo usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ili kukidhi matakwa ya Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003. Kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 34 cha Muswada huu; Kamati inaishauri Serikali kupitia Bodi hii, kusimamia na kudhibiti shughuli za sekta ya ujenzi na hivyo kupunguza tatizo la Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wasiosajiliwa na wasio na sifa zinazotakiwa. Kamati inaishauri Serikali kuwa; iwapo kuna wanaoitumia vibaya taaluma hii, basi wachukuliwe hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kufutiwa usajili wao kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kumpa uwezo wa kisheria Msajili wa Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kutoa zuio (katika Kifungu cha 21 (1) cha Muswada huu) pale itakapobainika kuwa kuna Makampuni hayajasajiliwa na yanaendesha shughuli za taaluma hii. Ni wajibu wa kila Mbunifu Majengo na Mkadiriaji Majenzi kufuata taratibu zilizowekwa ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha 40 cha Muswada huu, sheria hii mpya inaweka bayana vyanzo vya fedha vya Bodi pamoja na masuala mengine ya fedha. Kamati inaishauri Serikali kupitia Bodi, kuongeza juhudi katika usimamizi wa masuala ya fedha na zaidi kuwa wabunifu wa vyanzo vingine vya mapato. Hii itaiimarisha Bodi na kuipa uwezo wa kujiendesha yenyewe katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali la pili la Muswada huu, Kifungu cha 2 kinazungumzia jengo lolote litakalojengwa, litakaloanzia thamani ya shilingi milioni 50,000,000/= lazima lihusishe Mtaalamu wa Ubunifu Majengo na Mkadiriaji Majenzi. Majengo yenye thamani ya milioni 50,000,000/= ni mengi sana sasa hivi, kwamba Bodi haitakuwa na uwezo wa kuyasimamia ipasavyo kutokana na uhaba wa Wataalamu wa aina hiyo. Kwa mfano majengo ya shule za msingi, zahanati, misikiti, makanisa, majengo ya mashine za kusagia na kadhalika. Pamoja na nia nzuri ya Muswda huu, tukiishaipitisha sheria hii, utekelezaji wake utakuwa mgumu zaidi na kukwamisha ujenzi wa majengo mengi ya Serikali pamoja na yale ya sekta binafsi. Kamati inashauri kuwa, ili sheria iweze kutekelezeka angalau majengo yanayoanzia thamani ya shilingi milioni 250,000,000/= ndio yahusike na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuiangalia kwa makini sheria hii ili iweze kutekelezeka. Maandalizi ya kutosha inabidi yafanyike kwa kuwahamasisha wanafunzi kuipenda na kuisomea taaluma hii. Aidha, Halmashauri za Wilaya, ziajiri na kusomesha Wataalamu wa kutosha watakaokidhi mahitaji ya sekta hii. Kwa kufanya hivyo, ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuwatumia wataalamu hao katika shughuli za ujenzi, sheria hii itaweza kutekelezeka kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali, kwa kupitia Bodi ya Usajili Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, itathmini viwango vya sifa za kitaalamu na kitaaluma, kusajili Wataalamu wenye sifa ili wasaidiwe kupata kazi nchini. Aidha, ili kulipunguzia Taifa hasara, ni vema Serikali kutoa kazi nyingi kwa Wazalendo wenye sifa, ambao kwa namna yoyote ile gharama zao zitakuwa chini kulinganisha na gharama za Wataalamu wa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika utendaji kazi wa kila siku na ugumu wa kupata kazi kwa Wataalamu Wazalendo; Kamati inaishauri Bodi na Makampuni ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, kwa kupitia vyama vyao mbalimbali vinavyowaunganisha, kujiendeleza na kukua. Hii ni kwa ajili ya kukabiliana na ushindani wa kibiashara miongoni mwao na hasa kwa Makampuni yanayotoka nje ya nchi. Ili kuwajengea uwezo Wataalamu Wazalendo, Kamati inaishauri Serikali kuwafikiria Wazalendo kwanza katika kutoa kazi zinazohusiana na taaluma ya ujenzi ili kuwajengea uwezo na uzoefu hasa kwa miradi inayogharamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inatoa fursa kwa Wataalamu wa kigeni kusajiliwa na Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi; Kamati pia inashauri na kusisitiza kuwa kila Kampuni ya kigeni itakayosajiliwa na kupewa kazi nchini ishirikishe Wataalamu Wazalendo katika umiliki na uendeshaji wa Kampuni hizo. Kwa

ushirikiano huo itasaidia kuleta ufanisi, kubadilishana uzoefu na kuongeza kipato kwa Wataalamu Wazalendo. Aidha, Kamati inashauri kuwa, kabla ya Wageni hao kupata usajili, uwepo utaratibu mzuri wa kubaini uwezo wao kwa kushirikisha mamlaka nyingine ili kuona kama Wataalamu hao wanafaa na wanakidhi viwango kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha 54 cha Muswada huu, sheria inatamka bayana kuwa itakapotokea mgongano wa kiutendaji kati ya sheria hii na nyinginezo katika sekta hii, ambazo zinafanana, sheria hii ndio itakayotawala. Kamati inashauri kuwa Serikali ipitie na kuhuisha sheria nyingine ili kuepusha migongano inayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara ya Miundombinu kuongeza juhudi katika kuzisimamia Bodi zake zinazohusika na sekta ya ujenzi. Taasisi hizo ni pamoja na Bodi hii ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (*AQSRB*), Bodi ya Usajili Wahandisi (*ERB*), Bodi ya Usajili Wakandarasi (*CRB*), Baraza la Ujenzi la Taifa (*NCC*) pamoja na Wataalamu wengine wa Mipango Miji. Hii itaziwezesha Taasisi hizo na Wataalamu hao kujenga uhusiano mzuri wa kikazi baina yao na kubadilishana uzoefu wa sekta ya ujenzi na hatimaye kazi zao zitakuwa za viwango na ubora unaokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Miundombinu. Naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Waziri wa Miundombinu; Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Naibu Waziri wa Miundombinu; Mhandisi Bwana Omar Abdallah Chambo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu pamoja na Wataalamu na Watendaji wote wa Wizara walioshirikiana na Kamati katika kuandaa na kutoa ufafanuzi wa kitaalamu wakati wote wa kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pia nitoe shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wataalamu wake, kwa kutoa ufafanuzi wa vipengele mbalimbali vya kisheria mbele ya Kamati pale ilipohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawashukuru Wadau wote waliotajwa hapo awali kwa ushiriki wao katika *"Public Hearing"* na kutoa maoni yao. Maoni hayo, ambayo kwa namna moja au nyingine yamesaidia na kurahisisha kazi ya Kamati katika kukamilisha na kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, nimshukuru pia Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Didimu Kashilillah pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kwa namna ya pekee, naomba niwashukuru Makatibu wa Kamati hii Bibi Justina Mwaja Shauri na Bwana Abdallah Hancha, kwa kuweza kuihudumia vema Kamati na kuandaa Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono kwa dhati kuwasilishwa kwa Muswada huu ili uweze kujadiliwa na Bunge lako Tukufu. Kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na taadhima naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. BAKARI SHAMIS FAKI - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI, WIZARA YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa, nikiwa mzima wa afya ili kutoa maoni juu ya Muswada wa Sheria ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa mwaka 2009, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 53(6)(c), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kutoa salaam zangu za mwaka mpya kwa Watanzania wote na hasa wapiga kura wa Jimbo la Ole, kwa kuingia mwaka wa 1431 Hijiria sawa na mwaka 2010 Miladia; wakiwa na afya njema kabisa. Aidha, natoa pole kwa wale wote waliofikwa na majanga mbalimbali kwa kipindi kilichopita cha mwaka 2009 na mwanzoni mwa mwaka huu wa 2010, Mwenyezi Mungu awape moyo wa matumaini na ujasiri kuweza kukabiliana na mitihani hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa utangulizi huo, sasa naomba kupitia baadhi ya vifungu katika Muswada ambavyo Kambi ya Upinzani inaona vinatakiwa kutolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 8(3) kinachosema kuwa Msajili atashikilia madaraka hayo kwa kipindi cha miaka mitano, ila anaweza kuongezewa muda pale atakapojiridhisha na utendaji wake wa kazi, (*...and may, subject to his satisfactory performance, be eligible for re-appointment...).* Kambi ya Upinzani inataka kuelewa kama Bodi ndiyo inayojiridhisha na utendaji wa kazi wa Msajili au Msajili ndiye anayejiridhisha na utendaji wake wa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 12(2)(b) kinachosema kuwa Kampuni yoyote haitakuwa na sifa ya kusajiliwa kama kampuni ya ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi hadi pale itakapokuwa imesajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni na kusajili jina la biashara. Kambi ya Upinzani inataka kuelewa ni kwa vipi idara zilizo chini ya Wizara za Serikali kama vile Idara ya Magereza, Suma JKT na Idara ya Ujenzi, kifungu hiki kinaziweka katika kundi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 13(7) cha Muswada kinamtaka Mbunifu Majengo au Mkadiriaji Majenzi pale atakapomkodisha au kumwajiri mtaalam mwenye taaluma kama yeye alipe "*fees*" na hivyo hivyo Kifungu cha 18(2) kinaitaka kampuni au mtu yeyote kutokufanya biashara hiyo hapa nchini bila ya kusajiliwa na kulipa "*annual subscription fee*". Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atoe ufafanuzi hiyo *fees* ambayo Kampuni ya ndani inatakiwa kulipa kwa kukodisha huduma za kitaaluma

toka nje, ni kwa ajili ipi? Sisi tunadhani hapa ni utoaji *fees* mara mbili mbili jambo ambalo ni kuwatendea visivyo wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 27(1) katika suala zima la uchunguzi, Bodi inazuia mtu au kampuni inayochunguzwa isiwakilishwe na Wakili au Mwanasheria. Lakini kifungu kinachofuata kinaonyesha kuwa utaratibu utakaotumiwa na Bodi unafuata taratibu zote za Kimahakama. Kambi ya Upinzani, ingekubaliana na dhana ya Kifungu hiki kama utaratibu ambao utatumika sio wa Kimahakama kwa lengo la kusisitiza dhamana ya taaluma kwa mtoa huduma. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki kinamnyima haki yule anayefanyiwa uchunguzi kutokuwakilishwa na Wakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 29(2) cha Muswada kinachohusu Mamlaka ya Rufaa, kuwa yatakuwa ni ya mwisho, naomba kunukuu:-

"*in any appeal, the Appeals Authority may give directions in a manner which it thinks proper, and the directions given shall be final, conclusive and binding upon all parties concerned"*.

Katika majibu ya hoja za wadau, Serikali ilisema kuwa Mahakama Kuu ina mamlaka ya kufanya mapitio ya Mamlaka ya Rufaa endapo upande wowote utakuwa haujaridhika na maamuzi yaliyotolewa. Kambi ya Upinzani haikuona marekebisho yaliyofanywa katika kifungu hicho kwenye jedwali lililotolewa ili kukidhi majibu ya Serikali kwa wadau. Hivyo basi, tunaitaka Serikali iweke wazi kifungu hicho na kutoa haki ya kukata rufaa Mahakama Kuu kama ilivyoahidi wakati ikijibu hoja za wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuchukua fursa hii, kutoa pongezi kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na asasi zake zilizohusika moja kwa moja na maandalizi ya Muswada huu, kwani wamefanya kazi kubwa na kwa busara zao wamekubali kuyafanyia kazi baadhi ya mapendekezo ya wadau katika kufanikisha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na samahani kidogo sauti yangu sio nzuri sana. Katika kuchangia Muswada huu ambao ni muhimu sana katika maisha yetu sisi sote, Muswada wa Sheria ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutajilia tena nafasi hii, nizidi kuwashukuru wananchi wa Wilaya ya Hai, kwa kuwapongeza sana katika ushiriki wao katika shughuli za kimaendeleo na ushirikiano wanaoendelea kunipa, nami nizidi kuwaahidi kwamba nitaendelea kushirikiana nao vyema.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, watendaji wote pale Wizarani na wataalam wake, kwa kutuletea Muswada huu ambao naamini ni muhimu sana, Sheria ambayo itachukua nafasi ya ile Sheria iliyoanza kutumika mwaka 1997 kwa maana ya mambo yalivyobadilika katika dunia ya leo ili tuendane na nyakati. Kwa lugha nyingine tunasema tunakwenda ki-*digital* ili tuachane na mambo ya *analogy*. Nizidi kuwapongeza wale watendaji wengine katika Bodi ambazo ziko chini ya Wizara hii, ipo Bodi ya Ma-*Engineers*, *Contractors Registration Board*, kwa kazi nzuri wanazozifanya katika *construction industry*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii kama inavyozungumzia na sisi wengine tumepata nafasi ya kuipitia, mambo mengi naona yako *covered* vizuri lakini naomba nitoe maoni yangu kwenye vifungu vichacge vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na functions za Bodi ambayo ndiyo haswa tunayoitungia Sheria hii. Kwenye kifungu cha 5(d), nashukuru kwamba umewekwa msisitizo na umuhimu kwa watendaji wa Bodi kupita ghafla au pasipo kutoa taarifa katika *site* za ujenzi. Hii itasaidia sana kuangalia kama taratibu zinazohusika katika ujenzi zimefuatwa na kuzingatiwa na wale wataalam walioorodheshwa kwenye mabango kama kweli wanazo hizo sifa zinazohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu hicho hicho cha 5(j), hapa naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri labda atakuja kutusaidia atakapokuwa anahitimisha pale mwishoni. Kifungu cha 5(j) kinasema:-

"*take disciplinary action against architects, quantity surveyors and others semi-professional registered by the Board*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni wale waliosajiliwa lakini je, ni kipengele kipi kitakachotumika kuwachukulia hatua wale ambao hawajasajiliwa lakini wanatoa huduma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5(n), nakipenda kwa sababu kitatusaidia kudhibiti wahuni upande wetu wa majenzi. Kinasema:-

"*promote and enforce professional conduct, ethics and integrity of architects...*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu muhimu sana na mimi nitaomba ziwepo kanuni zitakazozidi kusisitiza umuhimu wa kuwadhibiti watu ambao wanavamia taaluma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5(p) hapo ndipo kuna umuhimu mkubwa pia, jamii yetu haina elimu. Kuna umuhimu mkubwa sana kutoa elimu kwa umma. Kifungu hiki kinasema:-

"promote awareness and educate the public on the professions of architecture and quantity surveying as well as the duties and responsibilities of architects and quantity surveyors".

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii kwa kiwango kikubwa sana haina uelewa wa taaluma hii, tumezoea mwananchi au raia yeyote anaweza kukwambia bwana nataka nyumba yangu hapa, hatua saba kwa kumi, chumba fulani au kama ulivyoona nyumba ya fulani lakini Bodi hii ikishirikiana na watu wengine ikiweza kuelimisha umma umuhimu wa kuwatumia wataalam, umuhimu wa kuzingatia Sheria, natumaini tutakuwa tumepiga hatua na kuisaidia jamii ikae katika majengo yanayostahili ambayo natumaini hayatakuwa na madhara mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 11, wanazungumzia *sub-register*; hawa labda ni wale waliotoka vyuoni kwa siku za hivi karibuni. Lakini nitaomba Mheshimiwa Waziri atueleze na kusisitiza kwamba wale wataalam waliohitimu nao watangaziwe ili waweze kuji-*register* kwa sababu miaka ya nyuma haukuwepo msisitizo. Hata kama hujawa *registered* kama *Architect* au *Quantity Surveyor* lakini sasa hivi Sheria inatuambia kwamba hata huja-*qualify* kuwa *registered* lakini ni vizuri ukawepo kwenye daftari la kumbukumbu za Bodi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri natumaini hilo nalo ataliweka kwa ajili ya wale waliosoma siku za nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu cha 20, ni ule ule msisitizo kwamba Sheria hii inawataka wananchi hawa au wawekezaji wote kutumia wataalam. Wakati mwingine tunaweza tukalalamika kwamba tunawabana wananchi au wawekezaji lakini ni muhimu sana ili kuepusha matatizo ambayo yanaweza yakatokea pale ambapo wataalam hawajatumika vizuri. Kwa hiyo, kifungu hiki cha 20, nashukuru kwamba kipo na kinazidi kusisitiza suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye kifungu cha 37 ambapo ni *monitoring and control of practices,* kinasisitiza kuwatumia wataalam katika ujenzi, hiyo ni muhimu zaidi kwamba lazima watumike wale wataalam kwamba kweli wanavyo vyeti na wanatambuliwa na Bodi ili kuepusha madhara mazima ambayo yanaweza yakatokea upande wa kiujenzi. Lakini kwenye 37 (3) hapa ni katika uandishi kuna neno kidogo mstari wa tatu ambao unasema ni *five shilling million* nadhani pale ilitakiwa kuwa ni *five million shillings*, ni marekebisho, natumaini yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini fungu hilo hilo la 37(4), nashauri pamoja na kutolewa kwenye gazeti la Serikali lakini na ufafanuzi uliotolewa pia katika vikao vilivyopita kwamba hata magazeti mengine kwa mfano *Daily News* yataweza kutumika kuwaorodhesha wote ambao wameshakuwa *registered* uzingatiwe. Lakini ninapendekeza Bodi ifanye kazi ya ziada zaidi kuchapisha vitabu vidogo ambavyo vitakuwa na orodha ya watu ambao wameshakuwa *registered,* hiyo *list* iweze kwenda hata kwenye Halmashauri zetu kwa sababu siamini kama watu wote wataweza kuangalia magazeti lakini kukiwepo na kitabu kinachoonyesha orodha ya hawa watu ambao wako *registered* itasaidia zaidi na kwa sababu itakuwa ni kila baada ya mwaka ku-*renew* itakuwa ni rahisi kuonyesha hata kama kuna wapya wameingia hapo katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho cha 37(5), natumaini hakijakaa vizuri lakini kwenye *amendments* ambayo tumeipokea naona kimewekwa vizuri na kinaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki cha 37(8), ninazidi kusisitiza umuhimu wa kuwatangazia wale waliosoma miaka ya nyuma ili wakaweze kwenda kuorodheshwa katika daftari la kumbukumbu na utalaam wao. Hii sehemu ya sita, mambo ya *financial provisions,* wale wote wa zamani wakishaorodheshwa, watasaidia sana kuchangia au kutunisha mfuko wa bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 51, naomba nisisitize kwamba ni muhimu na lazima kuwepo na *minimum fees* ile ya kusema kwamba watu wapewe tu uhuru, haitatusaidia. Umuhimu na ulazima wa kuweka *minimum fees* ya hawa watalaam wanapowa-*charge* wale *clients,* itasaidia sana kwa sababu sasa kama utakuwa unamtegemea *contract* ndio aweze kumlipa huyu mtalaam, mtalaam saa nyingine anaweza kuwa na kigugumizi au kushindwa kumsimamia vizuri kwa maana ya kumnyoshea kidole. Naomba izingatiwe sana kwenye *regulations*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa majedwali, napenda nitofautiane kidogo na Mheshimwa Blandes aliyesema labda majengo yawe zaidi ya thamani ya shilingi milioni 250, majengo ya shilingi milioni 50 bado yanahitaji utaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamalizia, namwomba Mheshimiwa Waziri kuna Sheria ya Majengo imekuwa ikizungumziwa miaka mingi sana. Sasa aniambie hii sheria itakuja lini maana baada ya kuunganisha taaluma zote hizi, kwa sababu sasa tuna Sheria ya Ubunifu wa Majengo na Wakadiriaji, Injinia, kuna hii *Contractor Registration Board* lakini kiunganishi cha taalam zote hizi ni pale ambapo tunakuwa na majengo ndio nia na madhumni lakini Sheria ya Majengo hatuna. Sheria ya Majengo itatusaidia kuwa na *specifications, standards* kutegemeana na aina ya jengo, yatakuwepo maelekezo muhimu. Lakini tuna ndugu zetu walemavu lazima tuwe na sheria ambayo inawasaidia hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anielezee hii Sheria ya Majengo lini inakuja, ni sheria muhimu sana na tunaihitaji, itatusaidia kuepuka madhara kwenye majengo mengi sana, matetemeko ya ardhi na vitu vingine. Kwa mfano kule Rungwe mwaka 2000, mwaka jana, hivi sasa Haiti kila mmoja anafahamu yaliyotokea huko. Lakini tunapokuwa na hii Sheria ya Majengo, itatusaidia sana kuepuka majanga makubwa ambayo yanaendelea kutokea na tunafahamu mabadiliko ya tabia nchi sasa hivi ni makubwa na bado yataendelea kuwa makubwa. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri aniambie hii Sheria ya Majengo, ni lini inakuja kwa sababu nafahamu ilishafanyiwa kazi miaka mingi sana ni kiasi cha kuileta na ningeshukuru kama ataniambia itakuja kwenye Bunge la mwezi wa nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizidi kusisitiza tu hata nyumba za vijijini zinahitaji utalaam kwa sababu sisi binadamu hatuishi mijini tu, tunaishi kule vijijini, kwa hiyo, hata kule vijijini tunahitaji utalaam ambapo wananchi wataweza kuupata kupitia kwenye

Halmashauri zetu. Mheshimiwa Waziri ataangalia vizuri kama katika hiyo miongozo ya kule vijijini kupitia kwenye Halmashauri zetu jinsi gani wananchi wataweza kupata misaada ya kiutalaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kusisitiza Mheshimiwa Waziri atueleze je, huo mpango mkakati wa kuwa na Sheria ya Majengo, ni lini hiyo Sheria inakuja? Nizidi kumwomba mwezi wa nne tukiipata, tutashukuru, tungeamini kwamba *construction industry* sasa imekamilika, hapa ilipo inakwenda vizuri lakini pasipokuwepo na Sheria ya Majengo bado *industry* nzima itakuwa haijakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii muhimu sana kwa sababu maisha yetu yote sisi yanategemea majengo. Niombe sana Sheria ya Majengo ije mapema kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Kabla hatujaendelea na uchangiaji, nitoe taarifa tu kwamba wale wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kile kikao kilichokuwa kifanyike saa saba, hakitakuweko tena kwa leo. Kwa hiyo, tuendelee na hoja iliyo mbele yetu ambayo ni Muswada wa Usajili wa Wabunifu, Majengo na Wakadiriaji Majenzi, *Architects and Quantity Surveyors (Registration) Bill.* Kama Mheshimiwa Mbunge yeyote angependa kuchangia Muswada huu, bado ninayo nafasi ya kutosha. Kwa hiyo, tunaendelea na uchangiaji ambapo amemaliza Mheshimiwa *Architect* Fuya Kimbita atafuata Injinia Laus Mhina ajiandae Injinia Stella Manyanya na wengine nitawataja kadri muda unavyoendelea.

MHE. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii, vile vile niwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Korogwe Vijijini, kwa ushirikiano wanaonipa katika shughuli zote za kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze mchango wangu kwa kuipongeza Serikali kwa kuuleta Muswada huu kwa wakati muafaka. Kingine ambacho nataka niipongeze Serikali ni kuiangalia sheria hii na kuikazia zaidi au kutoa kipaumbele zaidi kwa kuwapa wananchi wa Tanzania fursa kubwa katika usajili na pia katika kuwapatia kazi wale ambao wana sifa kama ilivyoelezwa katika sehemu ya tatu ya kifungu namba 12 hadi 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania sasa tunahitaji nyumba bora na si bora nyumba. Nyumba bora tunazozungumzia hapa wala kigezo kisiwe kwa mijini tu kama alivyozungumzia Mheshimiwa Spika, vijijini pia tuna uwezo wa kupatiwa hizo nyumba ambazo tunaita nyumba bora ili mradi tu zikidhi vile vigezo vyote ambavyo vinahitajika. Nyumba bora vijijini inaweza ikawa ya miti, inaweza ikawa ya nyasi kama itafuata utaalamu ambao sasa hivi tunauzungumzia na kuwapa nyenzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii nataka niseme wazi inakwenda sanjali kabisa na usajili wa Wahandisi au sheria za Wahandisi kwani taaluma mbili hizi zinafanya kazi sambamba au zinafanya kazi pamoja. Mara kwa mara kazi inayofanywa na Mhandisi ni lazima ianzie kwa *Architect* na *Architect* hawezi akafanya kazi yake au kazi yake haiwezi ikaonekana kama hatakuwepo Mhandisi. Kwa hiyo, watu wawili hawa Mhandisi na *Architect,* ni watu ambao wanashabihiana vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya sheria hii ni mazuri sana kwa wale ambao tumepata bahati ya kuisoma au kuipitia isipokuwa kwa upande wangu kidogo nimepata utata kwenye sehemu ya tatu ya sheria hii, kifungu cha 21 kinachompa uwezo Msajili wa kusimamisha kazi inayoendelea. Hapa nataka niseme tu kwa kifupi kwamba katika taratibu za kiujenzi, kuna taasisi ambazo pia zimepewa uwezo wa kutoa vibali vya ujenzi. Sasa kwa mfano Halmashauri kwa muono wangu, mimi nadhani ingekuwa ni vema zaidi kabla ya Msajili huyu wa Bodi kutoa hii *stop order* angewasiliana na hizi taasisi ili kuepusha migongano. Maana ufikirie mahali hapa pametolewa kibali cha ujenzi, pamepitia hatua zote na kukubalika halafu ionekane kwamba anasimamishwa bila ya kuwa na mawasiliano yoyote na wale waliotoa kibali. Kidogo hapa naona kama pataleta utata. Hapa ninaomba kama inawezekana kuwe na mawasiliano kati ya Msajili huyu wa bodi na taasisi hizi ambazo zimepewa uwezo wa kutoa vibali kabla ya kutoa hii *stop order*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia labda nisisitizie kwamba Bodi yetu hii izingatie sana vigezo na sifa za usajili katika sheria hii ambayo tunaizungumzia leo hii. Kikubwa zaidi ni kujaribu kuweka hatua kali kwa kifupi za makusudi, za kisheria za kuwachukulia wale ambao wanakiuka taratibu. Hili nalizungumzia makusudi, mimi ni Mhandisi binafsi lakini hata kwenye upande wetu wa Wahandisi kuna wengi tu wanaitwa Wahandisi lakini hawana sifa hizi. Kwa hiyo, hili ninaomba liangaliwe sana. Upande wa Udaktari pia hata Matabibu wanaitwa Madaktari, ni kitu kimezoeleka. Sasa ninaomba labda hili lisizoeleke, kwa upande wa wenzetu Ma-*Architect* mtu anapofikia hatua ya kuitwa *Architect* awe ni *Architect* kweli na awe na sifa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tahadhari ichukuliwe hata kwa hawa wenzetu ambao ni *qualified Architect.* Mimi kwa uono wangu, nimeona mara nyingi majengo mengi yanayojengwa hapa Tanzania utakuta kwenye mabango, kuna jina la *Architect* pale, inawezekana kabisa ni *qualified Architect* na ana sifa zote lakini huwa nakuwa na wasiwasi, unakuta *address* ya *Architect* yule labda ni ya Dodoma au Mbeya lakini jengo linalojengwa liko Arusha. Sasa huwa nakuwa na wasiwasi anakuwa na muda gani wa kwenda kukagua kule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi ninachokizungumzia hapa, kuna mtindo wa kuuza majina. Mkandarasi anakuwa na jengo lake, shida yake ni kupata jina la *Architect* kwa hiyo, ananunua jina la *Architect* linaandikwa pale lakini *Architect* yule hana muda wa kuja kuangalia kazi zile. Kwa hiyo, mimi kwa kifupi naweza kusema kuwa kwa kweli huku ni kudhalilisha taaluma. Ningeomba wenzangu Ma-*Architect* wajaribu kulikwepa hilo. Hilo linatokea sana hata kwenye upande wa sisi Wahandisi matokeo yake nadhani

ndiyo hayo unakuta majengo mengi yanaanguka au hayajengwi katika ubora unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kama nilivyosema awali kwamba maandalizi mazuri ya Muswada huu yamekwishafanyika, nisingependa nirudie yaliyokwishasemwa kwenye kitabu chetu, itakuwa ni kurudia yale yale tu. Kwa kifupi, napenda niishie hapo na kusema kuwa naunga mkono Muswada huu kwa asilimia zote mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie Muswada huu muhimu sana wa Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayofuraha kwa sababu siku za karibuni tumeona jinsi ambavyo majengo yamekuwa yakiporomoka katika miji yetu na kuhatarisha usalama wa maisha ya watu na mali kwa ujumla. Jambo ambalo mimi nasema kwamba hasara ile haimuhusu mwenye mali peke yake bali ni tatizo pia kwa Taifa kwa maana kwamba hela ikipotea inaathiri mpaka kwenye uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, naona Muswada umekaa vizuri na walioufanyia kazi, kwa kweli wamefanya vizuri, naona Mheshimiwa Waziri kwa kuwa ni mzoefu sana katika eneo hili, basi na kazi yake imekuwa haina tabu kwetu, niseme nampongeza sana pamoja na timu yake ambayo wameandaa Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu hasa yatakuwa katika masuala ya ujumla na uzoefu uliopo. Kwanza kabisa, suala la ushirikishwaji, katika eneo hili ambalo ni eneo muhimu sana na ni eneo ambalo mtu kabla hajawasilisha michoro anakuwa kwanza ameliona lile jengo kichwani kwake, kwa hiyo, kwa kweli ni kazi ambayo ni *completed* na ni kazi ambayo inahitaji umakini mkubwa sana.

Sasa ninalozungumzia ni juu ya ushirikishwaji na hasa hasa kwa teknolojia mpya zinazojitokeza sasa hivi. Unakuta nchi yetu bado katika maeneo mengine hatujawa na uzoefu wa hizo teknolojia mpya na tunapomchagua Mbunifu wa Majengo, unakuta kwamba baada ya ku-*compete*, anaweza akujitokeza Mbunifu kutoka eneo lingine si lazima awe kutoka Tanzania ambayo tunaamini kwamba baada ya kukamilisha kazi yake atakabidhi jengo na wewe mwenye jengo ndio utakuwa unahusika katika kufanya *maintenance* na kulitumia katika miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo inakuwa ni ngumu pale inapokuwa kwamba ile teknolojia iliyoletwa ni mpya na humu ndani hatuna wataalam wa kutosha katika eneo lile matokeo yake ukiachiwa jengo baada ya muda unajikuta pa kuanzia huna inabidi uanze tena kutangaza tenda mpya labda ya kufanya *repair* na vitu na kama hivyo. Hili hasa naomba niliweke katika majengo ya Serikali, kwa sababu ni pesa nyingi zinatumika katika majengo kama haya. Kwa hiyo, nashauri Serikali ihakikishe kwamba kile kitengo chake ambacho kinahusika katika kusimamia majengo yake ni vyema kikawezesha wataalam kuwa na taarifa za karibuni yaani *up to date information* kuhusiana na

teknolojia inayojitokeza, hii itasaidia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba majengo haya yanadumu, lakini pia hata kutoa msaada kwa watu wengine ambao wana majengo yao binafsi katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni vyema sana tukawekeza katika teknolojia na jambo hili pia litawezesha kuhakikisha kwamba si lazima kila wakati mbunifu tumpate kutoka nje, hivi karibuni naona kuna uzoefu unaoendelea kwamba yule anayekuwa amepata kazi ya kwanza, ujue huyo huyo ndio atakayepata ya pili, na ya tatu, kwa sababu ile ya kwanza inakuwa imeshamjengea msingi au mtaji, kwa hiyo, mimi naomba pia kwamba katika zile kazi kubwa zinazotolewa na Serikali ambazo naamini huwa zinatoa faida pia za kutosha kwa wale ambao ni wabunifu hawa Makandarasi wa eneo hilo, ni vyema pia tukawa na sura ya kuangalia kwamba kazi ya kwanza aliipata nani, ya pili kaipata nani, ili sio kazi zote zinalundikwe kwa mtu mmoja tu matokeo yake ni kwamba kama itakuwa kulikuwa na upungufu katika eneo fulani basi inamaana ule upungufu unakuwa katika majengo yote anayokuwa ameyapata kwa sababu tunakuwa hatujapata ile *experience* ya tatizo lililopo. Kwa hiyo, nashauri hilo baada ya kupata taarifa mbalimbali kutoka kwa wadau wa eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia juu ya huo ushirikishwaji katika maeneo ya uchoraji au uandaaji wa michoro ya majengo katika maeneo yale ambayo ni nyeti au katika mipango kwa ujumla. Mimi naona kuna wakati labda tunajisahau, tunafikiria kwamba ukiwa mbunifu basi uliangalie jengo peke yake bila kuangalia uhalisia wa maeneo na hili halitoki kwao peke yao kuna watu pia wa mipango miji na kuna makandarasi kama wa umeme na wa ujenzi kwa ujumla wake. Sasa mimi huwa inanigusa kidogo napoona kwamba kuna majengo yanaibuka baadhi ya maeneo ambayo inasemekana siku za nyuma yalikuwa yamezuiliwa kusiwe na majengo marefu kufikia umbali wa kiasi fulani.

Sasa nataka kufahamu kwa mfano ukanda wa Pwani, kwa haraka nilikuwa naelewa kwamba maeneo hayo yaliwekwa kuwa na nyumba za kawaida au zisizokuwa ndefu sana ili kuhakikisha kwamba upepo unaotoka bahari unaweza kwenda umbali mrefu zaidi lakini unakuta maeneo hayo ndio yanayokuwa na majengo makubwa au maeneo ambayo yalistahili yawe ni sehemu za kupitisha maji unakuta hayo ndio yanayokuwa yamewekwa majengo. Sasa huyu Mbunifu yeye kwa kuwa ameonyeshwa kiwanja, atabuni kutokana na hali iliyopo lakini unakuta na hao watoaji wa viwanja kwa nini hawaangalii uhalisia wa lile eneo, kwa nini tunaamua kugawa maeneo yale ambayo tunaamini fika yanaleta athari katika shughuli za kila siku ambazo pia zinaweza zikawa ni tatizo kubwa katika usalama wa makazi? Kwa hiyo, nashauri pamoja na kwamba wajibu wao ni kutengeneza au kubuni majengo yanayostahili lakini ni vyema pia wakaenda zaidi ya ubunifu wao wa majengo kuhakikisha kwamba lile eneo katika michoro ya asili linaonyesha ni eneo ambalo lilikuwa linahusika katika mambo yapi, ili kuweza kushauri na kusaidia kabla hawajaanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa Arch. Kimbita, kwamba kuna jambo ambalo mimi kidogo huwa linanishangaza, unakuta jengo limejengwa mpaka limefikia mwisho halafu linapokuja kupitishwa mtu anasema kwamba hili jengo

halistahili kupitishwa limekiuka utaratibu. Sasa najiuliza mpaka huyu mtu ameanza kuchimba msingi mpaka anajenga mpaka linafika mwisho hao waangalizi walikuwa wapi? Ninao mfano wa jengo la *TANESCO* pale Ubungo lilipata shida sana kwenye kupita na majengo mengine mengine. Kwa hiyo, nafikiria Bodi hii isimamie si tu katika jengo lenyewe lakini pia hata kufahamu kwamba jengo liko katika sehemu zinazokubalika ili kuweza kushauri mapema kabla hasara zaidi hazijapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, niseme pia kwamba bahati nzuri ni kwamba wenzetu Wabunifu wanajitahidi na ninawapongeza sana lakini kwa kweli kuna wakati mwingine wanafanya kazi za ziada. Utakuta huyu Mbunifu yeye akishamaliza kubuni jengo, akakadiria thamani yake basi huyo huyo ndio *Engineer* wa Umeme, huyo ndio *Civil Engineer* yaani unakuta karibu kazi zote wanajirundikia wenyewe kinyemela na hii imekuwa ni tatizo na nilikuwa nafikiria pia hata huu utaratibu wa kusema kwamba labda kazi za ujenzi fulani, zote ziwe chini ya kwa mfano *contractor* wa *civil*, mimi nadhani inasaidia kupunguza ubora wa kazi. Nilikuwa natarajia kwamba kama kuna Mkandarasi wa Umeme basi aweze kutoa gharama zake kabla hazijawa ndani ya Mkandarasi wa Ujenzi. Hii itasaidia kutunza viwango na kuhakikisha kwamba gharama zinazostahili zinakuwa kama ilivyokusudiwa. Kinyume na hapo, unakuta kwamba huyu wa ujenzi anataka achukue karibu faida kubwa halafu wale wengine ambao wanaendelea na maeneo mengine wanajikuta wamewekewa hela kidogo kiasi kwamba wanakuwa hawakidhi zile thamani halisi zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna suala la *standards* na mambo ya kawaida ya kuhakikisha kwamba jengo linakuwa salama. Kuna taratibu ambazo zinahusisha kwa mfano unapoweka waya za umeme au unapoweka nyaya za mawasiliano, hazitakiwi kukaribiana kwa umbali fulani lakini kwa sababu unakuta kwamba ushirikishwaji unakuwa ni mdogo, unaweza ukakuta *port* moja inachanganya hivyo vitu vyote kwa pamoja na hii inaleta athari kubwa sana kwa watumiaji. Kwa hiyo, nashauri sana kwamba katika eneo hili ndugu zetu Wasanifu wa Majengo ni vyema tukawa na heshima ya fani zetu, kila mdau ashiriki vizuri katika eneo lake ili kuhakikisha kwamba majengo yanayojengwa yanakuwa ya kiwango na kuleta tija kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niseme tu kwamba Wasanifu wa Majengo wanao uwezo mkubwa sana wa ku-*serve* pesa za Watanzania hasa hasa kwa kupitia majengo ya Serikali na majengo ya watu binafsi kwa kuwa wao ndio wanakuwa wamesema thamani na ukifuata Sheria yetu ya Manunuzi sasa hivi ni kwamba tunamtafuta yule ambaye ametenda kwa bei ndogo zaidi lakini haitoshi tu kuwa ni bei ndogo zaidi iwe ni bei ndogo ambayo inakidhi utendaji. Sasa wakadiriaji wanapokuwa hawako *competent* katika lile eneo wanaweza wakakadiria aidha chini sana au juu sana kiasi cha kuigharimu nchi. Kwa hiyo, nachowaomba ni wao kuhakikisha kwamba wanakuwa kila wakati wako jirani na teknolojia ya wakati huo ili kuweza kutoa makadirio yaliyosahihi na kuweza kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, niseme kwamba Mheshimiwa Waziri ametuletea Muswada mzuri na kinachotakiwa ni kuziwezesha taasisi ambazo zitasimamia Muswada huu ili ziweze kutekeleza majukumu yake inavyostahili bila kusahau kuwawezesha Wabunifu Majengo au Wakadiriaji Majengo walioko nchini na hasa walioko Serikalini ili waweze kutumika vizuri kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. BASIL PESAMBILI MRAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ingawa mimi siyo Mhandisi, naona wasemaji wote leo ni Wahandisi lakini ninafikiri nina uzoefu wa kutosha kuweza kutoa mchango ambao utasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri kwa kuleta Muswada huu. Ni wa siku nyingi kwenye Wizara hii hata mimi niliwahi kuushughulikia kule mwanzo mwanzo wakati nikiwa pale. Kwa hiyo, umeweza kufika leo na kwa kuzingatia kiu cha wadau wa sekta hii ya *Architect and Quantity Surveyors* kwamba wawe na sheria, nafikiri kwao leo itakuwa siku nzuri na ya furaha kama tukipitisha. Nampongeza Waziri kwa kusukuma jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili au matatu ambayo yatasaidia kuboresha tu Muswada. Ukienda ukurasa ule wa 16, *section* ya 16 (b), inasema kwamba:-

"in the case of a firm, it is incorporated in Tanzania and the majority shares are owned by the citizens of United Republic of Tanzania"

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani kama kampuni ya nje *majority shareholders* siyo Watanzania wasipewe kazi ndani ya nchi. Mimi nafikiri hii siyo lazima; vile vipengele (e) na (c) vinatosheleza ukishasema tu kwamba Watanzania wapewe upendeleo, kwamba kazi zipewe kwa Watanzania basi Watanzania wale watachukua kazi hizo na wataweza kuajiri mtu yeyote wanayemuona anafaa hata kama ni wa nje. Ukitia sharti la Watanzania kuwa *majority shareholders*, uoga wangu ni kwamba Watanzania wengi hawana mitaji na Muswada wenyewe kwenye vifungu vingine unakiri, kwa hiyo, hutakuwa umewasaidia sana hawa Watanzania; badala yake ungesema mtu wa ndani akipewa kazi anaweza kuajiri mtu wa nje kadri anavyoona ni lazima au mtu wa nje akipewa kazi sharti ambalo tungeweka sasa ni kusema ashirikishe Mtanzania, awe na ubia na Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubia huu siyo lazima uwe ndani ya kampuni; ni ubia ndani ya kazi kwamba kama kwa mfano umepewa kazi ya kujenga jengo hili la Bunge, ukimpata Mtanzania na kama anaona hana uwezo kimtaji na pengine kiutaalamu, ni juu yake sasa kwenda kutafuta mtu wa nje na ubia wao unakuwa ni wa jengo hili tu, sio jengo lingine. Kwa hiyo mimi nafikiri tukifanya hivyo Watanzania wataendelea kushika mpini kwenye shughuli hii na hilo ndilo jambo la maana. Hili pia kwa kweli lingewezekana hata kwa kazi nyingine za utengenezaji wa barabara na shughuli za kiuhandisi za ujenzi. Mimi napendekeza tusilazimishe mtu wa nje awe na *majority shares* za Watanzania hata

kama ni *minority*, hata kama ni ubia tu wa kazi fulani *specific* inatosheleza; hiki kifungu cha 16(1)(b) tukikiacha hivi kilivyo kitaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni hapo hapo ukurasa wa kumi na sita, Kifungu cha 16(3), kinasema:-

"*no foreign person or firm shall be registered without evidence of involving local architects…*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, *involving* kwa njia gani? Mimi nafikiri kwamba *involvement* hii tunayoizungumzia, ni hiyo hiyo kama ni ujenzi, kwa kazi maalum, labda ni *Architect* kwa kazi maalum, tunahitaji *definition* ya *involvement.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa kumi na saba, kifungu cha kumi na nane pale inaposema kuweko na *annual license*, mimi nilifikiri kwamba kwenye mambo ya leseni katika nchi hii tunasogea, tunaondoka kwenye *annual licensing*, hata kwenye biashara tunaenda tu kwenye *license* moja lakini kila mwaka labda lazima afanye mambo fulani ambayo yatamuwezesha kuendelea kulinda ile leseni ya awali. Kwa mfano, katika nchi nyingi Wahasibu, ingawa wewe ulishapewa leseni ya kuwa Mhasibu au kuendesha Kampuni ya Uhasibu ni lazima kila mwaka ufanye mitihani fulani, uji-*update* ndio uweze kuendelea ku-*practice* kama Mhasibu hata Madaktari ndivyo ilivyo. Madaktari wakishapewa ile leseni ya kwanza ya Udaktari, kila mwaka haendi kuomba leseni ya pili ya Udaktari, hii naona kama ni njia imewekwa tu kusaidia hii Bodi kupata mapato na nafikiri sio sawa ku-*pegg* sheria kwenye dhana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale pale ukurasa wa kumi na saba, kifungu cha ishirini, kwa nini mnasema mimi ninayejenga lazima nipekue vyeti vya *Architect*? Kinasema ukitaka kujenga jengo kubwa, upekue cheti cha *Architect* na uridhike huyu kweli ana cheti, mimi ni nani kujua cheti cha u-*Architect* cha Urusi, cha Tanzania, cha Ulaya, cha wapi? Mimi nafikiri tukiuacha hivi kama ilivyo itakuja kusumbua sana watu wanaotaka kujenga badala yake tuseme tu kwamba yeyote anayechukua kazi ya u-*Architect*, ahakikishe ana cheti kilichokubaliwa na Bodi sio mimi ninayetaka kujenga kwenda kutafuta mtu mwenye cheti, kwa sababu uki-*extend* hii hata itafika siku kabla hujapasuliwa, utamuuliza Daktari nioneshe cheti chako cha upasuaji, sasa hii haifanyiki katika hali ya kawaida. Mimi nina pesa nataka nyumba, ni juu ya yule *Architect* kuthibitisha na sio lazima anithibitishie mimi, kuthibitisha kwamba leseni yake ni halali na inatumika, yaani imeshahalalishwa na *registration authorities*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule mwisho, ukurasa wa thelathini na tisa pale inapozungumziwa juu ya shilingi hamsini milioni, kwamba majengo ya shilingi hamsini milioni basi ndiyo yaanze kushughulikiwa na ma-*Architect* na ingawa nimeona *amendment* hapa sasa hivi ya shilingi mia mbili na hamsini milioni bado nafikiri ni hela kidogo sana. Tunazungumzia habari za shilingi mia mbili na hamsini milioni, ni hela kidogo sana kwa ujenzi wa siku hizi. Mimi ningekuwa wewe Mheshimiwa Waziri

ningeipandisha mpaka shilingi nusu bilioni au hata shilingi bilioni, shilingi bilioni au nusu bilioni ni nini siku hizi? Kwa hiyo, hii itakuja kuleta usumbufu sana. Wewe ukitaka kujenga kibanda chako, tena na sheria yenyewe inasema hata *maize mill*, mimi nikitaka kujenga banda la kusagishia mahindi au kukobolea mpunga, nikatafute *Architect* wa kazi gani hata *draughtsman* anaweza akakuchorea. Kwa hiyo, nafikiri pamoja na Kamati kusema kwamba iwe shilingi mia mbili na hamsini milioni, nafikiri hiyo bado ni ndogo mno; mimi nilifikiri nusu ya bilioni au bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pointi nyingine labda ya mwisho ni hii ya majengo ya mijini na majengo yasiyo ya mijini. Siku hizi watu wanajenga maghorofa vijijini. Kule kwangu kuna watu wengi wanaishi kwenye majumba ya maghorofa vijijini, sasa huyo naye afanyeje? Mimi nafikiri kwamba labda kwa vijijini, njia rahisi zaidi ya kutekeleza dhana hii ingekuwa kutofautisha majengo ya ghorofa na majengo yasiyo ya ghorofa kwa sababu ukishasema jengo la ghorofa rosheni moja au zaidi, unazungumzia habari za jengo lenye gharama zaidi na mtu anayetaka kujenga hivyo lazima awe na kauwezo zaidi. Kwa hiyo, nafikiri kwamba majengo mengi ya kawaida hayahitaji *Architect* na hata kama ni mijini, hata kama ni vijijini, kwa sababu watu siku hizi wanaanza kujenga majengo makubwa vijijini. Tutafute namna nyingine nzuri zaidi ya kusema jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kupendelea Watanzania na hasa kwenye miradi ya Serikali, mimi naliunga mkono tena nafikiri hili ndilo muhimu katika Muswada huu, kuliko mengine yote. Lakini ukishampendelea lazima vile vile uweke *fee structure*, ambayo pia ni chini kwa sababu watu hawa wanatoza fedha nyingi sana, kwa kawaida ni asilimia kumi na mbili labda, kumi na tano; ni zaidi ya kumi, lakini haiwezekani mimi nikupendelee halafu ukishapata uje tena ukanitoze ada ya juu. Kama tunataka wananchi waendelee kutumia *Architects* na hawa *Quantity Surveyors*, kwa kweli ni lazima pale ambapo tunaweka upendeleo na vile vile tuteremshe zile ada kwa sababu atakachofaidika nacho ni ule mzunguko wa kazi nyingi, kama unapata kazi nyingi lakini kwa *fee structure* iliyo chini ile unayotoza wewe, mimi nafikiri bado unaweza ukatengeneza fedha na unaweza ukafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo sijaliona kwenye Muswada huu ni hili la kufundisha vijana, *apprenticeship*. Sioni mahali ambapo Muswada huu unalazimisha *Registered Architects* ku-*train young Architects* hata kama ni wewe peke yako, fundisha mmoja ukae naye kama msaidizi. Tusipoweka utaratibu wa *apprenticeship* kwenye sheria hii hawa vijana wote wanaotoka vyuo vikuu na *training colleges*, hakuna atakayewafundisha kwa sababu wale wanajua wakiwafundisha wanaongeza *competition*. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwenye sheria hii sijui ni wapi pa kuweka kipengele cha kulazimisha *Practising Architects* wawe *foreign* au *local* kufundisha vijana wanaotoka chuo kikuu. Kumfundisha sio lazima umuajiri lakini mfundishe ili akitoka pale awe na uzoefu kiasi na tuweke na kipindi labda miaka miwili au mitatu ya *apprenticeship*. Bila kuweka hivyo, hata hii tunayozungumza ya kupendelea Watanzania, haitafanikiwa kwa sababu sasa Mtanzania huyo, kama haja-*practice* atapataje kazi? Hataweza hata kuja kuwa Katibu wa Bodi kama hii ambayo tunasema Katibu awe na uzoefu wa miaka saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo nilitaka kutoa kama mchango na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa na mimi nichangie Muswada huu ingawa nilikuwa sijajitayarisha lakini haiwezekani kukosa la kusema na mchango wangu utaweza kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli wa mambo, tushukuru kwamba Muswada huu umekaa katika hali nzuri, kwa ujumla asilimia tisini na tisa na ni mambo madogo sana ambayo yanahitaji *input* zaidi. Kwa mfano nianze na lile alilomalizia Mheshimiwa Basil Mramba; katika Kifungu cha 12(1)(b) ambacho kinasema:-

"a person shall not be eligible for registration as-

(b) a graduate architect, a graduate quantity surveyor, an architectural technician or an architectural draughtsmen unless-

(i) he has attended training and qualified from a recognised university or at a duly accredited technical institution;

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa tunazungumzia *a graduate architect, graduate quantity surveyor* halafu hatoweza kusajiliwa mpaka awe *qualified from a university*. Unajua kwanza tukisema *graduate*, tunategemea kwamba huyo mtu ameshamaliza masomo, ame-*graduate from university or equivalent* ndio maana tunasema *graduate*, sasa hapa ukija tena, ukiandika kwamba *a recognised university*, mimi nilitegemea hapa kwamba kifungu hiki mbali na kuwa ametoka kwenye *recognised university*, sasa labda ana-*acquire a training from a qualified firm or construction firm*. Sasa hapo tutakuwa tumeiweka vizuri zaidi, ndio itakuja na kile kifungu ambacho amesema hakipo, lakini *training* zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tukitoka hapo, tukija kifungu cha 5; *functions of the board*, ziko kama kumi na saba na hii Bodi inaonekana ni ya kitaalamu mno lakini tuna uzoefu kwamba, mwenzangu *Architect* Fuya Kimbita amesema sheria hizi zitatuletea ufanisi wa pamoja na kwamba tuwe na *standard* za kiasi gani. Majengo yetu nchini mpaka sasa hivi, kila mtu anajijengea kwa mfumo ambao amejionea yeye au ameona alivyosafari au namna gani, lakini kama nchi hatuna *standard* kwamba mji fulani majengo yake yana *standard* fulani, sisi tunajijengea tu, sasa haya ni mambo ambayo yanahitajika kuangaliwa. Leo ukienda *Australia*, kwa mfano, mji wa karibuni, *Brisbane* wanaita *Gold City*, utakuta majengo yote yana *standard* fulani na yana picha fulani, yana sura fulani, yana mwelekeo fulani ni kwa msafiri kujua huu ni mji fulani, huu ni mji fulani, sisi kwetu hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hizi *functions* zilizozungumzwa hapa, kumi na saba, *sub-functions of the board* na hiyo ya mwisho kwa kawaida inakuweko siku zote inasema:-

"carry out any other functions which are for the public interests and which the Minister may, in writing, direct".

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi tumuombe huyu Waziri, moja katika kazi ya hii bodi kwa kushirikiana na bodi zinazohusika na mipango miji, wa-*create standard*, pawe na mipango miji hasa katika hizo *developed area* ambazo tunakwenda. Tuwe na mwelekeo wa vitu ambavyo vina *standard* maalum, vina sura maalum isiwe ujenzi wa holela holela tu, wewe ukishachorewa jengo uweke tu, hii bodi isiwe inashughulikia umadhubuti wa lile jengo tu, ishughulikie pia ile *view*, uzuri wa lile eneo na uzuri wa lile jengo na *provision of parking* na vitu kama hivyo. Sasa hii Bodi kwa kushirikiana na vyombo vingine, iwe inafanya kazi hiyo ambayo watapangiwa na Waziri, basi naomba moja iwe hiyo, kwa sababu ni mambo ambayo tunakosa katika miji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni katika Kifungu cha 5(e) kinasema kwamba:-

"promote, monitor and provide continuing professional development opportunities and facilities for the study and training in architecture, quantity surveying and allied subjects".

Sasa hapa na mimi naomba niongeze kwamba isiwe kama ni ku-*provide development* na hizo *opportunities* basi itajwe wazi kwamba hiyo *function* ya *board* siyo kukusanya *fees* tu na mambo mengine, basi iwe pia ni ku-*provide opportunity* kwa ku-*acquire highly qualified*, yaani kupeleka watu wetu, wale *qualified*, kuwe na *routine* ya kupata *latest development* duniani za mambo ya *construction* na iwe hii bodi ndio kazi yake ku-*rotate* hawa wataalamu kwenye makampuni makubwa yaliyopo duniani, yazungumzwe kama *group five companies* na mengineyo ili wataalamu wetu na wao wasibakie na utalaamu waliosoma chuo kikuu na uzoefu wa hapa tu, wawe na *information latest* kwa sababu haya mambo kila siku yako *dynamic* sio ambayo yametulia tu, sasa hii bodi kazi yake moja iwe ni hiyo ili kuwe na *rotation*. Kama ni upendeleo, basi pia kuwe na upendeleo hata wa bodi hii kutafuta mbinu gani za ku-*penetrate* na hawa ma-*architecture* wetu kupata kazi nchi za nje, kubuni mbinu kwamba na wao wawe wanatoka ili kupata hiyo *knowledge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 8(1) ambacho bahati nzuri imeletwa *schedule of amendment* sasa hivi, kilikuwa kinazungumza kwamba bodi ndio itakayomchagua Msajili, sawasawa na uzoefu ulitajwa wa miaka mingi bahati nzuri kwenye *schedule of amendement* imeshakuwa *reduced* mpaka miaka saba, lakini huyu *Registrar*, inazungumza kwamba *Registrar* ataweza kuongeza muda, sasa namna ilivyoelezwa hapa haikukaa vizuri. Bodi ndio inaweza kumuongeza muda, sio *Registrar* yeye mwenyewe ajiongezee muda baada ya kuona amefanya vizuri, ni bodi ndiyo itakayomuongezea muda baada ya kuonekana kwamba huyu *Registrar* amefanya vizuri, nataka pale iwekwe sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 8(3) kinasema kwamba:-

"*the Registrar shall hold office for a term of five years and may, subject to his satisfactory performance, be eligible for re-appointment for one more term*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, iwekwe wazi kwamba bodi baada ya kuridhika na utendaji wake ndiyo atakuwa *subjected* kuongezewa muda mwingine, ningependa iwekwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 12(2)(b) ambacho kinazungumzia kwamba kwa kusajiliwa kama kampuni ya ubunifu majengo na kukadiria majengo hadi pale itakapokuwa imesajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni na kusajili jina la makampuni, hapo sawa. Sasa Kambi ya Upinzani iliweka kiangalizo kwamba je, haya makampuni yaliyoko chini ya Mawizara kwa mfano SUMA-JKT, MAGEREZA, hawa vipi wao? Muswada haujafafanua. Sasa tuseme kabisa hata iwe chini ya Wizara na wao lazima wawe na *qualified* wataalamu, kwa hiyo, na wao wasajiliwe sio kwamba kwa sababu wao wako chini ya Mawizara tena iwe basi, kwa sababu wanaweza wakafanya makosa hao halafu sisi tukawa hatuna la kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nafikiri na mimi nimetoa mchango wangu katika Muswada huu. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

MHE. ENG. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili mimi niweze kuchangia Muswada wa *Architect and Quantity Surveyors.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, ningependa nireje historia fupi ya hii sheria. Sheria hii kabla ya mwaka 1997 ilikuwa sheria moja ilikuwa inaitwa *Engineers Registration Board*. Sasa baada ya kuona kwamba ufanisi wake haukuwa mzuri, Serikali iliamua kwamba itagawanya katika bodi tatu, bodi ya kwanza inaitwa *ERB (Enginners Registration Board),* bodi ya pili inaitwa *Architect and Quantity Surveyors Board*, bodi ya tatu inaitwa *Contractors Board*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwamba mimi nilikuwa Muasisi wa awamu ya kwanza kabisa toka mwaka 1997 mpaka mwaka 2000, Mjumbe wa Usajili wa Uhandisi *ERB,* kwa hiyo nafahamu sana haya mambo. Lakini kwa nini Serikali mara kwa mara imekuwa ikizileta sheria hizi? Nakumbuka mwaka huu au mwaka jana ilileta Marekebisho ya Sheria ya *ERB* na hivi sasa imeleta Marekebisho ya Sheria ya *Architect and Quantity Surveyors Board*. Wakati nilikuwa Mjumbe wa *ERB*, tulikuwa tunapata shida sana juu ya ujenzi wa hovyo hovyo wa maghorofa, hususani pale Kariakoo.

Sasa tulikuwa tunajiuliza, kwa nini majengo yanajengwa na majengo yanaporomoka. Tukawa tunaona iko ombwe pale lakini mwaka 2001 mpaka 2004 nikawa Mjumbe wa *Architect and Quantity Surveyors Board* ambayo hivi sasa tunaijadili. Pia tukawa tunaona iko ombwe pale, Wasanifu wa Majengo wanajenga na *Quantity Surveyors* wanafanya kazi yao, lakini kwa nini majengo yanazidi kuporomoka! Wakati nilikuwa Mjumbe *ERB*, kulikuwa na tatizo la kutokuwa na Sheria ya Majengo katika nchi

yetu tukamuagiza Mares alikuwa *Registrar* aandae rasimu, akaanda rasimu ya Sheria ya Majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwa na Sheria ya Majengo, tutaomba sana, kwa sababu gani, Sheria ya Majengo itaunganisha wadau mbalimbali na pia itaunganisha Wizara mbalimbali. Miongoni mwa Wizara itakuwa Miundombinu, Wizara ya Ardhi, itakuwa *Local Government* na Wizara nyingine nyingi. Hivi kwa mfano kule Temeke lile jengo lililoanguka lile, nani alishtakiwa pale? Maana yake ukienda kwa mtu wa Jiji pale Temeke anasema yeye hahusiki, ukienda kwa *Architect* anasema yeye hahusiki, ukienda kwa *Consultant* anasema yeye hahusiki, lakini Sheria ya Majengo ita-*specify* kwamba katika ujenzi wa jengo, nani anatakiwa kuwajibika *in case* jengo linaporomoka, lakini hivi sasa hakuna Sheria ya Majengo ndiyo maana tunazidi kuhangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa na kwa uchungu mwingi sana, napenda Mheshimiwa Waziri alichukue suala hili kwamba tutaendelea kuhangaika. Kesho tutarekebisha Sheria ya *Engineers Registration Board*, kesho itakuja *Architect and Quantity Surveyors Board*, kesho kutwa utaleta *Contractors Board*, unakwenda hapa pale, hapa pale, tutafika lini? Kwa hivyo ninapenda, mimi sisemi sana tena kwa ufupi kabisa, ndiyo maana sitaki kugusia sana huu Muswada isipokuwa nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nasema kwamba nchi hii lazima ilete Sheria ya Majengo. Itatusaidia sana. *Draft* iko Wizarani, Mares aliandika *draft*. Nakumbuka siku moja tumefanya tafrija pale Jangwani *Oceanic Hotel*, nadhani kule Mbezi Beach, alikabidhiwa Mheshimiwa Magufuli *draft* ile, sasa kwa sababu Mares uko humu ndani, nitamtaka amkabidhi Waziri wa sasa, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa ili kwamba jambo hili liweze kutekelezeka, tutaendelea kuyumba hivi mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua sheria hii itatusaidia, kwa mfano pale Kariakoo, ni jambo la ajabu sana unakuta jengo hili lina ghorofa kumi na mbili, mita tatu linajengwa jengo lenye ghorofa kumi, mita mbili tena kuna jengo lingine lina ghorofa tatu, sasa hivi huu mji utakuaje? Hapo hapo tunasema Kariakoo sijui ndio Jiji la Dar es Salaam. Kama kweli Kariakoo ndio Jiji la Dar es Salaam mbona linajengwa hovyo hovyo? Ni kweli maana yake mtu yeyote akitaka kufanya *shopping* Dar es Salaam lazima aende Karikaoo, sasa kwa kweli kukija kutokea tetemeko la ardi pale Kariakoo itakuwaje si itakuwa mbaya zaidi kuliko Haiti? Dunia nzima inatazama Haiti. Hakika dunia nzima itaitazama Kariakoo, itaitazama Tanzania, lakini najua itakuwa ni aibu. Kwa sababu watu tunajua matatizo ndiyo maana tunaliambia Bunge hili pale Kariakoo ni matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ili tupunguze angalau matatizo haya, napendekeza kabisa Mheshimiwa Waziri wakati ya *widingup,* azungumze juu ya Sheria ya Majengo, mimi nitakuwepo na Mheshimiwa Shukuru rafiki yangu, nitakuwepo, nitamsikiliza kwa kweli asipogusia suala hili, itabidi tubishane wakati wa kupitisha vifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Majengo ingetusaidia sana kama nilivyosema hapo mwanzo kujua kwamba jengo hili lilitakiwa lijengwe ghorofa ngapi, kutoka jengo la ghorofa hii kwenda ghorofa nyingine inatakiwa liwe la mita ngapi yaani

space between one building and another, Sheria ya Majengo ingesema lakini hizi sheria nyingine hazitamki mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii fupi kabisa, nadhani Mheshimiwa Waziri amenielewa na katika kuhitimisha atalizungumzia jambo hili. Nakushukuru. *(Makofi)*

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kupata nafasi na mimi nitoe mchango wangu kidogo katika Muswada huu wa *Architect and Quantity Surveyors* na bahati nzuri sio mbaya mimi ni Mwanasheria sio kama wenzangu waliotangulia ambao ni *Engineers* kwa hiyo mimi nitajikita zaidi katika maeneo ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Kifungu cha 12(4), nashauri kuwepo na *maginal notes* zinazoeleza kwamba kifungu hicho kinahusiana na masuala ya *penalty*, pale imekaa tu *general* inaelezea tu *qualification for registration*, lakini ni vizuri katika sheria wakati unaenda kuisoma ukiwa unatafuta jambo fulani unajua kwamba jambo hilo linapatikana eneo gani. Sasa kifungu kile cha nne kinaelezea kuhusu adhabu ya masuala ya *qualifications* za usajili, kwa hiyo kwa pembeni yale maneno machache tunayaita *maginal notes*, kuwepo na *maginal notes* zinazoeleza kwamba hicho kifungu kinahusiana na masuala ya *penalty* kwa sababu Sheria hizi zinasomwa na watu wengi, wengine ni wakulima, wengine ni wafanyakazi, wengine ni watu kutoka kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pale kwenye kifungu cha 12 (4) kinaeleza kwamba mtu yeyote atakayekuwa ametenda kosa chini ya kifungu hicho atatakiwa kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kifungo kisichopungua miezi sita.

Neno la kwanza limesema mtu yeyote, lakini kwa mujibu wa kifungu hicho inawezekana isiwe mtu ikawa ni shirika *(firm),* sasa katika tafsiri haijasema kwamba neno *any person includes firm or company;* kwa hiyo ni muhimu kusema *any person or company or firm who gives false information, otherwise* kifungu hicho kitahusiana na mtu tu na inapotokea shirika au kampuni au *firm* imekosea, basi kifungu hicho hakitakuwa kinamgusa. Kwa hiyo, ninaomba kushauri iwe ni *any person or firm or company.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama inawezekana basi isiwe mtu akikosea anatozwa shilingi milioni tatu, kampuni kubwa ya ukandarasi nayo ikikosea faini ni shilingi milioni tatu, wajaribu kuangalia ile shilingi milioni tatu kwa kampuni ni sahihi. Yapo makampuni makubwa sana ya ujenzi, nyingine ni *international companies*, wakitoa *fine not less than three million* ni sahihi lakini *for an individual* nilikuwa tu najaribu kulitafakari kama linaweza likarekebishwa ili tunapopitisha mambo hapa yawe vizuri katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ambacho nilikuwa naomba nitoe maoni yangu ni Kifungu cha 13, sehemu ya nne ambacho neno la mwisho linasema *or*

investment shall be conclusive, kuna neno pale linaelezea *conclusive* kwamba, Bodi inaweza ikatoa maamuzi fulani na yale maamuzi yakawa ni *conclusive; shall be conclusive*. Sasa kwa manufaa ya kifungu hiki, nilidhani katika masuala ya maamuzi, kunapotokea mgogoro baina ya pande mbili ni muhimu upande husika unaopewa maelekezo au adhabu au upande unaotakiwa kuwajibika kwa jambo fulani au lingine ukapewa haki ya kusikilizwa. Kisheria unasema *right to be heard* na ndiyo misingi ya *natural justice. Of course*, humu ndani kuna kifungu kimeeleza kwamba, kifungu chochote ambacho kitakuwa kimekosewa, kunakuwepo na haki ya ku-*appeal* lakini katika kifungu hiki kimesema *shall be conclusive*. Sasa hili neno *shall be conclusive* ndilo nilikuwa nalitafakari kwamba, endapo mtu hajaridhika na maamuzi ya Bodi itakuwaje maana ni muhimu akipewa hata nafasi ya kitu kinachoitwa *revision*, yaani hiyo Bodi ikapokea tena maelezo kutoka kwa yule mtu ika-*revise* juu ya jambo hilo ambalo huyu mtu amelalamikiwa. Kwa hiyo, nilidhani lile neno *conclusive* wataalamu wetu wajaribu kuangalia katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ni kile cha 13(7) ambacho kinasema kwamba: *"A person, client or institution which hires the services or employs foreign architects or foreign quantity surveyors shall ensure he pays the fees imposed by this Act."* Hii sheria itatoa haki kwa Bodi ku-*charge fees* za aina fulani, lakini kifungu kinachotoa haki hiyo kwa Bodi hakipo. Kwa mujibu wa kifungu hiki, haya ni maelezo tu, kwa hiyo ni lazima kiwepo kifungu kinachotoa mamlaka kwa Bodi hii ya Usajili ili iweze ku-*charge* hizo gharama, lakini kwa kifungu hiki bado hakitoshelezi Bodi ku-*charge*. Kifungu hiki kimeeleza tu kwamba, kutakuwepo na ada lakini lazima kiwepo kifungu sasa kinachotoa hayo mamlaka, inakuwa kwa mujibu wa kifungu fulani basi Bodi hiyo ya Usajili inaweza kutoza ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 13(9) kinazungumzia kuhusu *penalty*, endapo mtu au kampuni itakuwa imekwenda kinyume na Sheria hii ya masuala ya usajili wa wabunifu majengo na wakandarasi, basi Bodi itamtoza faini ya *ten thousand US dollars.* Sasa hii ni Sheria ya Tanzania, inatumika Tanzania; kwa nini tutamke dola humu kwenye Sheria za Tanzania? Kwa nini tusiseme hiyo dola elfu kumi ni sawa sawa na shilingi ngapi za Kitanzania maana hapa tunawaenzi watu wa mataifa mengine, Watu wa Marekani? Kwa hiyo, naomba kushauri neno *ten thousand US dollars* libadilike, waifananishe na hela ya Kitanzania kwamba, ni kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 21(2) kinaendelea kusisitiza kwamba, masuala ya *revision* na *appeal* katika hoja hizi zinazohusiana na masuala ya *penalty* ni muhimu yakazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 26 kinaelezea kuhusu masuala ya *registration of name to the register*; masuala ya majina, jinsi ya ku-*register* kwamba ni wakati gani basi inaweza ika-*register* na wakati gani inaweza ikafuta *registration*. Wakati mwingine kampuni inaweza ikaamua kubadilisha jina inaitwa kampuni X wakati inafanya kazi au katikati ya kazi kampuni hiyo inaamua kujiita kampuni Y, kwa hiyo, nilidhani ipo haja ya kuelezea pia kwamba, endapo kunatokea mabadiliko ya aina hiyo;

je, kampuni hiyo Y itapaswa tena kwenda ku-*register* upya au itatambulika kwa usajili ule wa mwanzo wa Kampuni X.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza masuala hayo ya kimsingi ya Sheria, niende kwenye masuala ya jumla. Kwanza, nizidi kusema kwamba, naunga mkono Muswada huu muhimu sana ambao umeletwa mbele ya Bunge hili Tukufu. Sasa yako masuala mbalimbali ambayo Muswada huu ni muhimu sana ukayazingatia hasa maeneo mapya ambayo Tanzania tunaendelea kujenga; kwa mfano, eneo la Kivukoni ni muhimu sana wataalamu hawa wa masuala ya ubunifu majengo na wakadiriaji majenzi wakatoa maelekezo kwamba, eneo jipya kama la Kigamboni utaratibu utakuwaje kuliko tukiacha tu watu wakajenga kawaida. Kwa hiyo ni muhimu sana eneo jipya likazingatia maeneo muhimu ya *Supermarket*, tukatengeneza barabara ambazo zitakuwa na *fliers* na vitu kama madaraja. Kwa hiyo, nina imani kwamba, Sheria hii itasaidia sana kuweka maeneo haya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, utaalamu wa masuala ya ubunifu majengo ni muhimu sana, lakini gharama za ubunifu majengo na wakadiriaji majenzi katika nchi zetu zimekuwa kubwa sana; kwa hiyo, mara nyingi sana hupelekea watu kushindwa kutafuta utaalam huu kutokana na gharama zao ambazo hazilingani. Utaalam huu wakati mwingine tunauhitaji hata katika shule zetu za kata, katika zahanati, majengo ya *public consumption* na hata katika majengo binafsi.

Sote tumekuwa ni mashahidi, maeneo mengi mtu akitaka kujenga anaambiwa ramani tu kuipitisha kwenye kompyuta ikatolewe kitu kidogo, anaambiwa labda kiasi kadhaa; mtu anasema sasa hicho kiwango si nimemaliza kujenga msingi. Kwa hiyo, nilidhani maadam kutakuwepo na Bodi, Bodi hii izingatie sana suala la gharama za wataalam hawa ili Watanzania wote waweze kutumia wataalam katika ujenzi wa nyumba zao katika maeneo mbalimbali na kujenga kitaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo gharama zitaendelea kuwa kubwa, hakika watu watashindwa ku-*access*, wataendelea kufanya shughuli kienyeji na matokeo yake, baada ya muda mfupi majengo hayo wakati mwingine yanadondoka, umakini haupo kwa hiyo, nilidhani ipo haja kabisa ya kutafakari suala zima la gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo, naendelea kuunga mkono hoja na ni imani yangu kwamba, ushauri nilioutoa utazingatiwa. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pindi Chana, tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri. Masuala ya majengo na majenzi hayawezi kukamilika bila kuzingatia masuala ya mazingira, kwa hiyo na sisi wa mazingira tuna neno kidogo. Naomba Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, atupe mchango wake kama mchangiaji wa mwisho asubuhi ya leo. Mheshimiwa Profesa Mwalyosi.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii. Nami nimeona mazingira ni sekta muhimu ikiwa ni *cross cutting;* ni vema katika kila Muswada tujitahidi kuyasemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujikita kidogo tu kwenye Kifungu cha (4) na (5), tunapozungumzia habari ya Bodi na watu watakao-*constitute* Bodi hiyo; uzoefu unaonesha katika nchi yetu hususan kuhusu aina ya majengo yanayobuniwa siku hizi. Ukienda Dar es Salaam hasa Kariakoo, mazingira ni *monotonous* kwa sababu ni vibiriti hasa ukitazama kutoka juu, hata watu wa *The Comedy* wamewahi kulizungumzia hili kwamba, Dar es Salaam haipendezi kwa sababu ni viberiti tu. Ubunifu ule wa zamani ukienda miji ya wenzetu Ulaya, unakuta *designers* wa zamani walikuwa na vitu vya vizuri, walibuni majengo ya ajabu sana; leo hii vile vitu vya ajabu walivyokuwa wanavi-*design* nyakati zile huvioni miaka hii, naita ni *simple designs,* ni *squares,* unaviunganisha viberiti *you get a building*; sasa ule ubunifu wa wenzetu wa zamani umepotelea wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Bodi hapa ina watu wengi sana, lakini utakuta watu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) hawamo. Watu hawa ndiyo wanaokwenda kuangalia hiyo *design*, wajiridhishe kimandhari *(aesthetic quality)* kama inaridhisha *vis a vis* eneo unalojenga kama jengo linaendana na mandhari hayo. Watu wa mazingira wanatakiwa waseme kwamba, kwa mazingira hayo jengo hili halifai au *design* hii haifai kwa sababu zitakazotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na aina ya *designs* zinazoletwa siku hizi ambazo ni viberiti; ni *very simple* ukilinganisha na zamani. Vilevile utakuta jengo linajengwa na mazingira yaliyolizunguka ni vitu tofauti kabisa. Wenzetu wanazungumza hapa kwa mfano, KUjenga kule Kigamboni, kama kweli tuna nia ya kuubadilisha uwe mji wa kisasa, naamini kwa maelezo tuliyopewa tunaambiwa wamezingatia mambo ya mazingira kwamba, ujenzi uendane na mandhari ya eneo hilo, isionekane jengo linajitokeza mahali ambapo inakuwa *very awkward* kwamba, hili jengo limekujaje hapa; yaani aina ya jengo lililojengwa halikutakiwa liwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yanahitaji Wataalam wa Mazingira, Watu wa NEMC wangeweza kuwemo kwenye Bodi hii, wakatakiwa kuangalia *designs* zote zinazotolewa kujengwa katika mazingira mbalimbali, wayaangalie na kutoa mapendekezo yao kwamba, hii ni sawa, hii irekebishwe, ibadilishwe iwe namna nyingine au vivyo hivyo inakubaliwa. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo kwa nini Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) hawapo, wanaoweza kutusaidia katika hili ninalolisema kutokana na kwamba, *designs* zetu za siku hizi ni za kushangaza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo litaangaliwa kwenye kifungu cha tano ambacho ni *functions*, hapa tuseme vilevile kwamba, kazi moja ya Bodi hii ni kuangalia haya mambo ya mazingira, kuainisha ubunifu katika michoro ile, walinganishe vilevile na mazingira yanayozunguka pale waweze kutoa mapendekezo, Bodi iweze kushauri kwamba *design* hii na mazingira itakakojengwa haviendani au vinaendana. Nilidhani kazi moja isemwe kwenye kazi za Bodi vilevile ni kuangalia masuala hayo ya mazingira kwamba, *designs* hizi zinaendana na masuala ya mazingira au hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye suala la *bill of quantities* ambayo ni kukadiria gharama kama kuleta kwa mfano; vifaa vya ujenzi, iwe kokoto, iwe wataalam hawa wanaziweka kwa kuzingatia umbali watakwenda kuleta hizi rasilimali, lakini huwa hawaangalii mazingira ya eneo lile. Ni pamoja na vitu kama kokoto utategemea kwamba, Wizara watatakiwa wa-*survey* aidha nchi nzima na kutambua maeneo ya kupata mchanga na kokoto kwa ajili ya ujenzi na kiutaratibu yanatakiwa yafanyiwe EIA au *Strategic Environment Assessment* ili kuona kama ukitumia *site* hii kuchimba kokoto au mchanga pamoja na gharama lakini athari zake nyingine kwenye mazingira ni zipi. Kwa hiyo, unaweza uka-*rule out* kwamba, *site* hii haifai kuchimbwa kabisa au *site* hii inafaa lakini gharama zake ni kubwa. Kwa sasa mambo haya hayafanyiki na katika Muswada huu kwenye kifungu hicho cha (4) na (5) hayajitokezi. Huu ni udhaifu mkubwa sana kwenye mambo ya majenzi, pamoja na kuboresha viwango vya *bill of quantities*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani ingawa ni vitu vidogo lakini vinatusaidia sana mbele ya safari kuzuia kuharibu mazingira yetu tunakoishi aidha mandhari, *aesthetics* au kuweka mashimo ovyo ovyo maeneo mbalimbali ambako hakutakiwi kama ni maeneo ya hifadhi au ni maeneo oevu *(wet-lands*), kwa mfano maeneo kama hayo una-*rule out* kujenga. Kwa hiyo, ndiyo maana utakuta Dar es Salaam maeneo oevu *(wet-lands)* yalikuwa mengi sana, yote yamejengwa, ukienda hata kule Mbezi Beach kuna *wet-lands* watu wanajaza udongo wanaita (ku-*reclaim).* Maeneo haya yalitakiwa yabaki kama yalivyo lakini nadhani wataalam wa mazingira hawahusishwi kwenye kuangalia *designs* hizi, *otherwise* ilitakiwa ipigwe marufuku kwamba, hayo siyo maeneo ya kujenga na hata kama wangeweza kujenga basi ni aina fulani ya majengo tu ndiyo yaruhusiwe kujengwa maeneo hayo. Sasa nitapenda Waziri atoe maelezo kidogo kuhusiana na suala hili katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalikuwa ni hayo tu ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa michango ambayo imetoka tangu tulipoanza kuujadili Muswada huu, tutakaporudi hapo saa kumi na moja tutaanza na Mheshimiwa Waziri ili tupate majibu ya hoja zetu. Kabla ya hapo, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati mbalimbali ambao tulitangaza vikao mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ambayo saa tisa nitaomba tukutane pale Chumba Na. 219, mkutane kwa sababu kwa wale ambao kuanzia mwisho wa wiki hii Kamati zao zitaanza kutoa taarifa humu, tunatarajia kabisa kwamba, mapema iwezekanavyo taarifa hizo zitakuwa zipo tayari kumfikia Mheshimiwa Spika, kabla hazijawasilishwa hapa ndani.

Baada ya kusema hayo, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 6.50 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa niliyonayo ni kwamba, wachangiaji wote ambao walikuwa wameomba kuchangia walikwisha kuchangia na kwa vile Naibu Waziri pia hatumwoni, kwa hiyo moja kwa moja nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ili aanze kutufungia huu mjadala. Mheshimiwa Waziri, tafadhali.

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha majumuisho ya hoja yangu, kwa ridhaa yako naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza sana Wananchi wa Mkoa wa Pwani, wakiwemo wa Jimbo langu la Bagamoyo na Wilaya ya Bagamoyo kwa kuwa wenyeji wazuri na kufanikisha Sherehe za Uzinduzi wa Maadhimisho ya CCM kutimiza miaka 33 ambazo zilifanyika Bagamoyo jana tarehe 31 Januari, 2010. Wananchi wa Bagamoyo mmekuwa wenyeji wema na Mkoa wa Pwani na Tanzania nzima imefarijika sana; mimi kama Mbunge wa Bagamoyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchukua fursa hii kuwapa pole Wananchi wa Jimbo langu na hususan wavuvi, wachuuzi, wapaa samaki na wafanyabiashara wa samaki kwa ujumla, kwa kuunguliwa na soko la samaki lililopo Mjini Bagamoyo tarehe 25 Januari, 2010. Tukio hili ni baya na la kusikitisha, kwani limeathiri sana juhudi za maendeleo za Wana-Bagamoyo. Mimi Mbunge wenu, nawapa pole sana kwa tatizo hili, nitaendelea kushirikiana nanyi na mara tu nitakapopata wasaa, nitakuja kuwa nanyi ili tujipange upya. Kwa sasa namwomba Mwenyezi Mungu awape subira, nguvu na ujasiri wa kukabiliana na janga hili na mitihani mingine ambayo imetupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi nyingine ili niweze kuhitimisha hoja iliyotolewa Bungeni leo asubuhi. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu na wale waliochangia kwa maandishi. Waliochangia kwa kuzungumza ni Waheshimiwa Wabunge wanane na waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa Wabunge saba. Wote ninawashukuru sana, wametusaidia sana katika kukamilisha utungaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kawaida, naomba niwatambue waliochangia kwa kuzungumza na wale waliochangia kwa maandishi hapa Bungeni. Nianze na waliochangia kwa kuzungumza ambao ni Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu na Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

Wabunge wengine ni Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mheshimiwa Eng. Laus Omar Mhina, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana na Mheshimiwa Profesa Raphael Benedict Mwalyosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni Wabunge wafuatao: Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji,

Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahaman Msomi, Mheshimiwa Profesa Raphael Benedict Mwalyosi, ambaye alichangia kwa kuzungumza na kwa maandishi, Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, hoja zilizotolewa ni za msingi na zitasaidia katika kuboresha usimamizi wa sheria inayotungwa. Aidha, kabla sijajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na kama nilivyosema awali katika hotuba yangu, napenda kurudia kusisitiza madhumuni ya kuleta mapendekezo ya kutunga Sheria hii na manufaa yatakayopatikana baada ya Muswada huu kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii italeta manufaa makubwa sana katika kusimamia kazi na mwenendo wa wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi nchini. Aidha, sheria hii itaipa uwezo Bodi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi hususan katika maeneo yafuatayo:-

- Kukagua na kuratibu shughuli za wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi katika utekelezaji wa miradi inayoendelea kwa njia ya kudhibiti upungufu katika usimamizi wa miradi ya ujenzi.

- Kupanua wigo wa usajili ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Bodi kutambua na kuratibu watu waliopata mafunzo ya kati ama *intermediate qualifications* katika fani za ubunifu wa majengo na ukadiriaji wa majenzi.

- Kusimamisha miradi ya ujenzi ambayo imekiuka sheria kwa lengo la kulinda usalama wa wananchi na mali zao.

- Kuiwezesha jamii kupata mazingira ya ujenzi yaliyo bora na yaliyo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa ufafanuzi huo, sasa napenda kujibu na kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa na Kamati ya Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambayo iliwasilishwa na Mheshimiwa Gosbert Blandes, kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu kuhusu majengo yaliyo na thamani ya shilingi milioni 50 ni lazima yahusishe mtaalamu au mbunifu majengo na mkadiriaji majenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imefanyiwa kazi katika Jedwali la Pili la Marekebisho kwa kufuta kiwango hicho na kuipa Bodi Mamlaka ya kuweka kiwango cha majengo yatakayohitajika kupata huduma za mbunifu majengo na mkadiriaji majenzi. Serikali itafanya mapitio katika sheria nyingine ili kuepusha mgongano unaoweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ya Kamati inasema ifuatavyo; unapotokea mgongano kati ya sheria na sheria nyingine, sheria hii ndio itakayotumika. Sheria ihusishwe, ihuishwe na sheria nyingine ili kuepusha mgongano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni haya yamepokelewa na Wizara na yatafanyiwa kazi ili Serikali ianze mchakato wa kuboresha sheria nyingine zote ambazo zinaweza zikawa na mgongano na sheria hii kwa maana ya kuepusha mgongano wowote ambao unaweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imeishauri Serikali iweke utaratibu maalum wa kuwaelimisha wananchi katika Mikoa, Wilaya na Halmashauri zao kuhusu umuhimu wa kutumia Wataalamu wa Bodi hii katika hatua zote zinazohusu ujenzi wa nyumba na majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu umepokelewa na Serikali itaufanyia kazi kuhakikisha kwamba, elimu itatolewa kwa Mamlaka zote husika na kwa Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati imeishauri Serikali iongeze idadi ya wafanyakazi katika Bodi hii ili iweze kusimamia vyema kazi za ujenzi na majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu umepokelewa na tayari mchakato wa kutayarisha muundo mpya wa Bodi umeanza. Bodi pia imefungua Ofisi za Kanda katika Miji ya Mwanza, Arusha na inatarajia kufungua Ofisi katika Miji ya Dodoma na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati imeishauri Serikali kupitia Bodi hii, kusimamia na kudhibiti shughuli za Sekta ya Ujenzi na hivyo kupunguza tatizo la wabunifu wa majengo na wakadiriaji wa majenzi wasiosajiliwa na wasio na sifa zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imeishauri Serikali kupitia Bodi kuongeza juhudi katika usimamizi wa masuala ya fedha na zaidi kwa kuwa wabunifu wa vyanzo vya mapato. Pia Kamati imeshauri kuwa ili sheria iweze kutekelezeka, anagalau majengo yanayoanzia thamani ya shilingi milioni 250 ndio yahusike na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wote huu wa Kamati umezingatiwa. Kama nilivyoeleza hapo awali, kuhusiana na thamani ya majengo ambayo yatamhusisha mtaalamu mbunifu wa majengo na mkadiriaji majenzi, sheria hii imefanyiwa marekebisho katika *schedule* namba mbili, na kwamba sasa kima kile kimekasimiwa kwa Bodi ili iweze kutenga kima hicho cha majengo kwa kadiri ya muda unaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Msemaji kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki; Kambi ya Upinzani ilipendekeza katika kifungu cha 8(3) kinachozungumzia muda wa Msajili kushika madaraka kwa kipindi cha miaka 5. Je, ni Bodi au ni Msajili ndio mwenye mamlaka ya kuongeza kipindi hicho cha Msajili kuendelea na madaraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yake ni kwamba, kifungu cha 8(i) kimeeleza kwamba, uteuzi wa Msajili hufanywa na Bodi, lakini hata hivyo kifungu kidogo cha (3) kinaelezea kwamba: *"Subject to his satisfactory performance,"* inamaanisha kwamba, kama Bodi itaridhishwa na utendaji wa huyo Msajili, siyo kwamba Msajili ajiridhishe na utendaji wake yeye mwenyewe. Kwa hivyo, Bodi itapendekeza kuteuliwa tena pale tu ambapo msajili huyo utendaji wake utakuwa umeiridhisha Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia imezungumzia kifungu cha 12 (b); ni kwa vipi idara zilizo chini ya Serikali zitasajiliwa kama makampuni ya ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba, wataalamu waliopo chini ya Taasisi za Serikali, kwa mfano, SUMA JKT, Magereza na Taasisi nyingine, watatakiwa kusajiliwa kwa mujibu wa sheria hii kama ilivyo kwa wataalamu wengine wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia imezungumzia kifungu namba 13(7) na kifungu cha 18(2) kwamba, tofauti ya ada zinazotozwa chini ya vifungu hivi ni ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kuwa, kwa mujibu wa kifungu cha 18(2), ni jukumu la kila mtaalamu au kampuni ya kitaalamu kulipa ada. Aidha, katika kifungu cha 13(7), muendelezaji au taasisi inayomwajiri mtaalamu wa nje ya nchi, analo jukumu la kuhakikisha kuwa mtaalamu huyo amelipa ada husika. Kwa mantiki hiyo, mtaalamu ambaye atakuwa amelipiwa na mwajiri, hatawajibika kulipa ada tena chini ya kifungu cha 18(2). Hivyo, dhana kwamba mtu atalipishwa ada mara mbili, haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia imegusia kifungu cha 27(1) kuhusu Uwakilishi wa Wakili au Mwanasheria katika mwenendo wa uchunguzi wa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kuwa, kisheria chombo hiki, yaani Bodi siyo Mahakama; hivyo, uwakilishi hauhitajiki. Aidha, Bodi inawasiliana na wale iliowasajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kambi ya Upinzani imezungumzia kifungu cha 29(2), stahili ya kukata rufaa dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka ya Rufaa ya Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba, pamoja na maelezo yaliyopo katika kifungu cha 29(2) cha sheria hii; pamoja na maelezo yaliyotolewa katika kifungu hicho ni haki ya Kikatiba kwa mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na maamuzi ya mamlaka dhidi yake, kuwasilisha suala hilo katika Mahakama Kuu. Kwa hiyo, pamoja na melekezo haya ya sheria kwa maamuzi yatakayofanywa chini ya Bodi kama mhusika hakuridhika kufuatana na Katiba ya Nchi yetu, bado ana haki ya kuwasilisha madai yake mbele ya Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya mapitio katika hoja za Kamati ya Miundombinu na Kambi ya Upinzani, naomba sasa nifanye mapitio katika hoja mbalimbali ambazo zimewasilishwa na Wabunge kwa njia ya kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita aliuliza Muswada wa Sheria ya Majengo utaletwa lini Bungeni na Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba, maandalizi ya rasimu ya Sheria ya Majengo yamekamilika. Kwa sasa Wizara ipo katika mchakato wa kupata kibali cha Serikali, kwa ajili ya kuwasilisha Muswada wa Sheria hii katika Kikao kijacho cha Mwezi Aprili, 2010. Kazi imeshafanyika imekamilika, kibali kikishatoka tutauwasilisha Muswada wa Sheria hii katika Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Kimbita, amegusia kifungu cha 5(1) na (j); ni adhabu gani itatolewa kwa wale wanaotoa huduma bila kusajiliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kuwa vifungu vya 34, 35(6) na kifungu cha 47(1)(a), vinatoa adhabu kwa wale wote watakaoendesha shughuli bila kusajiliwa. Vifungu hivyo vimeorodhesha na vimeainisha adhabu mbalimbali ambazo zitakuwa zinatolewa kwa wale watakaothubutu kutoa huduma bila ya kusajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kimbita amehoji kifungu cha 11 juu ya wataalamu waliohitimu miaka ya nyuma na akapendekeza kwamba, hawa nao wasajiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba, kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha sheria hii ambayo Muswada wake umewasilishwa hapa ni kuwa ni wajibu wa kila mtaalamu kusajiliwa ili kazi zake ziweze kutambulika kisheria. Wataalamu ambao wame-*graduate* zamani na hawa ambao wata-*graduate*, baada ya sheria hii ni kwamba wote watahitajika kusajiliwa ili kazi zao ziweze kutambulika kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kimbita pia alizungumzia kuhusu kifungu cha 37(3), maneno *five shillings million* yasomeke *million shillings.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yamepokelewa na yamezingatiwa na kwa hiyo hilo badiliko litafanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 37(4), uchapishaji wa majina uwekwe pia katika magazeti ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri umepokelewa na tutafanya hivyo, pamoja na uchapishaji wa majarida au vijitabu ambavyo vitakuwa na orodha ya waliosajiliwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kuhusu majengo ya shilingi milioni 50 yanahitaji taaluma. Mheshimiwa Fuya Kimbita, amezungumzia kwamba, aina yoyote ya majengo

madogo iwezekanavyo, lakini yanahitaji utaalamu na wataalamu watahitajika sana kuhakikisha kwamba, wanayashughulikia majengo haya ili tupate ufanisi katika ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu tumeupokea na unazingatiwa. Kama nilivyozungumza awali, kwenye *Schedule No. 2* nimeainisha pale ni majengo ya aina gani, baada ya mchakato mkali wa wadau pamoja na mchakato mkali wa Kamati ya Miundombinu ambayo ilielekeza kuhusu suala hili na ndio tukapata *Shedule* hiyo *No. 2* kama ambavyo inasomeka hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Laus Mhina, k alitoa pongezi kwa maandalizi mazuri ya sheria; tunapokea pongezi hizi kwa mikono miwili kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Wataalamu wa Wizara ya Miundombinu. Halafu amezungumzia kifungu cha 21, Msajili atakapotaka kutoa *Stop Order,* ashirikishe wadau katika sekta nyingine za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu umepokelewa, hata hivyo, Bodi italazimika kushirikisha wengine katika utendaji wa kazi zake. Bila ya shaka jambo hili litafanyiwa kazi kwa taratibu zile ambazo zipo za ufanyaji kazi chini ya Bodi.

Mheshimiwa Injinia Stella Martin Manyaya, kwanza, amepongeza maadalizi mazuri ya Muswada huu na kama nilivyosema awali, nimezipokea kwa niaba ya Serikali. Pia amezungumzia kuporomoka kwa majengo ni hasara kwa nchi, hivyo taaluma zitumike. Ushauri tunaupokea kwa mikono miwili, tutaufanyia kazi kupitia sheria hii pia.

Mheshimiwa Manyanya amependekeza pawepo njia ya kutoa uzoefu kwa wataalamu wetu, kuendana na teknolojia za kisasa. Paweze kuwa na njia za kuendesha elimu endelevu ama *continuing professional development* mara kwa mara kulingana na mahitaji ya wakati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mategemeo yetu ni kwamba, katika utendaji wa Bodi tutahakikisha kwamba, programu hizi za *continuing professional development* au kutoa mafunzo kwa wataalamu ya mara kwa mara kwa ajili ya kujiendeleza basi baada ya kupitisha sheria hii, yataimarishwa na kuhakikisha kwamba wataalamu wetu wanakuwa bora zaidi.

Vilevile amezungumzia pia kwamba, wabunifu sio lazima watoke nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kwamba, wataalamu wetu wana uwezo mzuri na ni kweli kwamba, siyo lazima watoke nje ya nchi, lakini pale ambapo inabidi kwa kazi maalum basi taratibu maalum zimewekwa chini ya sheria hii ambazo zitawawezesha wataalamu wa nje kuweza kufanya kazi hapa Nchini Tanzania.

Mheshimiwa Manyanya pia amependekeza kwamba, pawepo na njia ya kugawa kazi ili kutolimbikiza kazi kwa wachache na pawepo utaratibu wa mipango miji katika kutoa huduma katika maeneo nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wote huu umezingatiwa na Serikali na kupitia Bodi hii, itahakikisha kwamba haya yanatekelezwa kama ambavyo yamependekezwa.

Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, amezungumzia kuhusu kifungu cha 16(1)(b) na kupendekeza kwamba kifungu hicho hasa cha (b) kifutwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kuwa, kifungu hiki kilifaa kibaki kama kilivyo kwa sababu kinasimamia makampuni yanayomilikiwa na wataalamu wa nje ya nchi; kwa maana ya idadi ya hisa zinazomilikiwa na wataalamu hawa. Kwa vile tunatoa ruhusa ya makampuni ambayo yanamilikiwa na wataalamu wa nje pia kufanya kazi katika nchi yetu, bila shaka itabidi tuwe na vifungu ambavyo vinadhibiti namna ambavyo wanafanya kazi; tukiondoa hiki maana yake ni kwamba, pale kutakuwa na pengo ambalo halitaweza kuzibwa na vifungu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kifungu cha 16(3), maana ya neno *involvement of local architects or quantity surveyors,* neno hili litafsiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kuwa, kwa mujibu wa sheria hii, wataalamu wazalendo watakuwa wanahusishwa kwa mujibu wa muda wa mradi husika. Kwa sababu kifungu cha 13(3) na (4), kinawataka wataalamu wa nje kusajiliwa kwa ajili ya miradi maalum.

Mheshimiwa Mramba pia amegusia kifungu cha 18(2) na kusema kwamba, kifungu hiki kiondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kuwa, nia ya *Annual Licence* ni kubainisha wale walio hai kiutendaji kila mwaka. Hili linafanyika siyo tu hapa kwetu Tanzania, lakini pia hata katika nchi nyingine, halina uhusiano na mapato ya Bodi maana kuna ada za kila mwaka zinazotolewa na wote waliosajiliwa. Kwa hiyo, ili kuhakikisha kwamba, wataalamu wanaofanya kazi hizi ni wataalamu hai, inabidi wawe *licenced* na kila mwaka wapate *licence* za kuwawezesha kufanya kazi.

Vile vile Mheshimiwa Mramba amegusia kifungu cha 20 kwamba; kwa nini mwendelezaji afanye upekuzi wa vyeti vya wataalamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kuwa, mantiki ya kifungu cha 20 ni kumlinda mwendelezaji kwa kuhakikisha kuwa, anakwenda kwa mtaalamu anayesajiliwa ili kupata huduma bora; yaani atawa-*engage* au atawapa kazi wale tu ambao wamesajiliwa kufuatana na sheria hii, maana ni wataalamu ambao wana taaluma hiyo ambayo wanaisema. Kwa hiyo, ni muhimu kwa mwendelezaji ahakikishe kwamba, anapekua vyeti vya wale wataalamu ambao anawatumia.

Mheshimiwa Mramba aligusia pia Jedwali la Pili; thamani ya majengo yanayotakiwa kusimamiwa na wataalamu iwe nusu bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nimelitolea maelezo hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia amezungumzia kuhusu Muswada, haujazungumzia namna ya kutoa mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba, suala hili au mafunzo kwa vitendo yanafanyika hata hivi sasa na litaendelezwa katika sheria mpya kwa kuweka sheria ndogo ndogo ambazo zitasimamia mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, amezungumzia kifungu cha 12(b) kwamba, Kifungu hiki kirekebishwe kwa kuondoa neno *graduate* na badala yake iwe *has qualified training from a recognized University.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kuwa, Kifungu hiki ni sahihi kwani ni moja ya Kifungu ambacho kinabainisha wataalamu ambao wana sifa za kusajiliwa kama zilivyoainishwa na Bodi. Inaambatana na sifa zile ambazo zitamuwezesha mtu kusajiliwa. *Of course, semantics, graduate* ni nani na kama *graduate* ni yule ambaye *has acquired* kama alivyosema Mheshimiwa Mnyaa, *has acquired training from recognized University.* Hizi zimepitishwa na wataalamu ambao wanazihakiki kusema kwamba, hiki kifungu kimekaa sawa kwa maana halisia ya maneno ambayo yametumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa amezungumzia pawepo na utaratibu wa kuwa na viwango vya ujenzi kulingana na sehemu za miji ama vijiji ili kupata sura maalum kwa kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba, hili litawezeshwa chini ya sheria hii mpya kwa taratibu ambazo zimewekwa katika sheria hii.

Mheshimiwa Benito Malangalila, amezungumzia kuwa Sheria ya Majengo ni muhimu sana katika kuunganisha wadau wa Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, kama nilivyojibu awali kwamba, maandalizi ya rasimu ya Sheria ya Majengo yamekamilika na kwamba, Sheria hii baada ya kupata kibali cha Serikali, basi tutaiwasilisha katika Bunge hili Tukufu mwezi Aprili mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa amegusia kifungu cha 12(4) kiwekewe *marginal note.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, nitakuwa nimechanganya hapa kidogo, kwa sababu hii siyo hoja ambayo ameiwasilisha Mheshimiwa Malangalila ni Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, ndiye ambaye ameiwasilisha hii kwamba, kifungu hiki cha 12(4) kiwekewe *marginal note.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba, katika taratibu za kiuandishi wa sheria, kifungu hicho wataalamu wameelekeza kwamba, hakiwekewi *marginal note.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 13(4) kinamnyima muwekezaji haki ya kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba, kwa mujibu wa kifungu cha 29 cha sheria, mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Bodi kama nilivyosema hapo awali, bado ana haki ya kukata rufaa, ana haki ya kwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kifungu kinachoipa Bodi mamlaka ya kutoza ada na kuwa kifungu cha 13(7) ni maelezo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba, vifungu vya 5(b), 18(a) na 53(a), vinaipa Bodi uwezo wa kisheria wa kutoza ada. Vipo vifungu maalum ambavyo vinaipa Bodi uwezo wa kisheria wa kutoza ada husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 13(9) kwa nini faini zitozwe kwa thamani ya Dola za Kimarekani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kuwa, faini hii inalipwa kwa thamani ya fedha za kigeni kwani walengwa ni wageni. Hata hivyo, wamepewa uwezo wa kulipa katika thamani ya fedha za Kitanzania kwa thamani ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, kifungu hiki ukikiangalia ni kifungu ambacho kina-*refer* kwa *foreign companies*. Kwamba, kinawagusa moja kwa moja makampuni ya nje na kwamba yatakapofanya makosa ndani ya nchi yetu, yatatozwa faini kama makampuni mengine. Kwa vile ni makampuni ya nje, faini yake imenukuliwa hapa kwa pesa za Kimarekani, lakini pia wanaruhusiwa kulipa pesa hizo kwa hela za Kitanzania. Wakilipa kwa hela za dola, tunazikaribisha pia hatuzikatai. Tunafikiri kwamba, kwa sababu kinahusu makampuni ya nje na faini yake iwekwe katika fedha za nje ama thamani yake kwa hela za Tanzania.

Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, amezungumzia kifungu cha 4 kwamba, wataalam wa mazingira wahusishwe katika shughuli ya usajili ya wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi, maoni haya yamepokelewa na yatafanyiwa kazi.

Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliwasilisha maoni yao kwa njia ya maandishi na naomba niyatolee ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, kwanza ameipongeza Wizara kwa kuleta Muswada wa Sheria ya Usajili wa Majengo na Ukadiriaji Majenzi; pongezi hizo nazipokea kwa mikono miwili kwa niaba ya Serikali. Pili, Muswada haukuzingatia masuala kuhusu watu wenye ulemavu kuhusu matumizi ya majengo mbalimbali. Maelezo ni kwamba, Muswada huu unahusu masuala ya msajili wa wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi. Serikali ipo katika mchakato wa kuwasilisha Muswada katika Kikao cha Bunge la Aprili mwaka 2010. Muswada huu utatoa kipaumbele kwa masuala ya matumizi kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, pamoja na pongezi amezungumzia kuhusu Ibara ya 4(1)(c) ya Muswada kuhusu uteuzi wa Wajumbe wa Bodi na anashauri kuwa, Wajumbe wapunguzwe; apunguzwe mmoja ili Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ipate nafasi. Pia Ibara ya 21(1) anashauri ni vema Manispaa au Halmashauri nazo zikahusishwa katika hili.

Kwanza, niseme kwamba, kuhusu Wajumbe wa Bodi, ushauri huu umefanyiwa kazi na kuna marekebisho ambayo tayari yapo katika *schedule of amendment*, ambayo yanajumuisha uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ambao watachaguliwa ili tuweze kukidhi mahitaji ya kuwa na Bodi ambayo inaweza ikamsimamia vizuri Msajili na kuweza kupata maboresho katika utendaji wa msajili.

Pia kwa vile Bodi itakuwa inafanya kazi na mamlaka nyingine, ushauri huu wa kufanya kazi pamoja na Manisapaa na Halmashauri utazingatiwa.

Vilevile amezungumzia kuhusu dhana ya upungufu wa malighafi za ujenzi katika ujenzi inaibuka vibaya, hivyo wataalam wasaidie kusimamia viwango vilivyohitajika. Ushauri huu umepokelewa kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi katika mchango wake wa maandishi amezungumzia kuhusu Ibara ya 4(1) ya Muswada kuhusu muundo wa Bodi na akashauri uwakilishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ili masuala ya mazingira yazingatiwe. Ibara ya 5(1) anashauri kazi zake iwe ni pamoja na kushughulikia masuala ya mazingira hasa *aesthetics.* Ushauri huu umepokelewa; namna ya mfumo wa uteuzi wa Bodi kama ambavyo umeainishwa katika Muswada huu, unamuwezesha Waziri mhusika kuweza kulizingatia hili na kuweza kulitekeleza na nina imani kwamba kwa maboresho ambayo tutayafanya katika Muswada huu, yatawezesha mazingira kujitokeza vizuri zaidi.

Mheshimiwa Juma Killimbah, ameipongeza Wizara kwa kuandaa Muswada huu; pongezi ambazo tunazipokea kwa mikono miwili kwa niaba ya Serikali. Pia amezungumzia wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi ni watu muhimu katika shughuli za majenzi. Sheria hii ihakikishe inasimamia juu ya utendaji wa kitaalam kwani kinyume ya hapo, madhara makubwa yanaweza kujitokeza ikiwa ni pamoja na maafa na kupoteza maisha ya watu yanayoambatana na hasara inayotokana na majenzi hafifu. Ushauri ambao tumeupokea na utazingatiwa wakati wa utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mbunge, amezungumzia pia kuhusu sheria hii impe meno ya kutosha Msajili wa Bodi kukagua wakati wote majenzi yanayoendelea. Maelezo ni kwamba, kifungu kimewekwa kwa ajili ya kazi hiyo, kwa hiyo, hili limezingatiwa katika sheria hii.

Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, ameshauri usimamizi uimarishwe katika Halmashauri za Wilaya ili majengo ya umma kama zahanati, madarasa, makanisa na kadhalika, yasimamiwe katika kiwango na ubora unaotakiwa ili kupunguza gharama na kubwa zaidi ni kulinda maslahi na maisha ya watumiaji majengo hayo. Maelezo ni kwamba, ushauri umezingatiwa na ndiyo hasa nia kubwa ya kuomba Bunge litunge

Sheria ya Usajili wa Ubunifu wa Majengo na Ukadiriaji Majenzi ya Mwaka 2009. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mtakapopitisha sheria hii, hili litakuwa limefanikiwa.

Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, kwanza, amepongeza kwamba, Muswada umeandaliwa na hoja imeungwa mkono na kwake pia nasema kwamba, napokea pongezi kwa mikono miwili kwa niaba ya Serikali. Amegusia adhabu ya udanganyifu kwa faini hii ya shilingi milioni tano kwa nini iwe ile ile kwa makosa yote na ina maana makosa yote yanalingana na sheria inasemaje juu ya mtaalam anayehusika kusimamia jengo au majengo yanayopata maafa? Katika sheria hii ni kwamba, makosa mbalimbali yameainishwa na faini au adhabu mbalimbali kwa kiwango cha chini na kiwango cha juu; faini ya fedha na faini ya kifungo ama faini ya fedha pamoja na faini ya kifungo. Uamuzi wa kiasi gani cha kutozwa, ameachiwa hakimu baada ya kutathmini mazingira ya makosa yaliyofanywa ili aidha aweze kutoa kiwango cha juu, cha chini, cha katikati ama faini zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani baada ya kupitia hoja hizi mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa, najua pengine kuna moja au mbili ambazo kuna uwezekano nimeziruka kwa sababu maandalizi yalikuwa ya muda mfupi na kama nimefanya hivyo, nawaomba radhi kwa wale ambao wametoa hoja zao. Nategemea kwamba, nitaweza kutolea majibu wakati tutakapokuwa kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa Mwaka 2009 *(The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Bill, 2009)*

Ibara ya 1

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 2

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 3

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 4

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 8

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 9

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 10

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 11

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 12

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 13

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13(9), Mheshimiwa Waziri ameitolea maelezo na Mheshimiwa Pindi Chana alielezea kuhusu ile *ten thousand dollars;* katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri anasema haiwezi

kubadilika iwe hivyo hivyo *ten thousand dollars* kwa sababu mlengwa ni kampuni ya kigeni.

Sikubaliani na maelezo hayo, kwa sababu juzi tulipopitisha hii *Electronic And Postal Communication Act,* ibara zote zilizohusiana na kutaja pesa za kigeni ilibidi tubadilishe zitaje kwa Shilingi ya Tanzania na hii ni kwa sababu kwanza ni kuiweka thamani yenyewe ya pesa yetu ya Tanzania, hatuwezi kutunga Muswada tukaweka thamani ya pesa ya kigeni, sidhani kama hii inaelekea. Kwa hiyo, tuweke kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania na kama ni *ten thousand dollars* juzi tuliweka *fifteen million Tanzanian shillings.* Halafu kwa vile hiyo kampuni ya kigeni inafanya kazi hapa Tanzania, hatuwezi kuweka thamani ya pesa kule. Ahsante. *(Makofi)*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Mheshimiwa Mbunge ni sawa na tutabadilisha hiyo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa vile tupo kwenye *process* ya kutunga sheria, naomba ututamkie hapa itakuwa ni ipi kwa sababu moja kwa moja hilo tamko lenu ndio linaingia huku kwenye mabadiliko?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba iwe *equivalent to Tanzanian shillings* kama ilivyo hapa. Nafikiri watu wanaweza kufanya hesabu, mimi sikusomea hesabu.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu juzi tulisema milioni 15 basi tuwe *consistent* na hii itamkwe milioni kumi na tano.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa sawa milioni 15. *(Makofi)*

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 14
Ibara ya 15

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 16

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, nitashindwa kunukuu kifungu moja kwa moja kwa sababu tumepita, lakini nimeona kwamba, kuna uharaka ambao umefanyika kuhusiana …

MWENYEKITI: Mheshimiwa Manyanya, kama kifungu kimepita tunaomba utuache tuendelee, ulitakiwa utusimamishe kwenye kifungu husika ndio utoe hiyo hoja, kwa sababu tupo kwenye Kamati ya Bunge Zima na sasa hivi tunapitisha vifungu. Unatakiwa unyanyuke wakati kifungu kinachohusika kinapotajwa halafu ndio utoe hoja yako na wengine wote wanafanya hivyo hivyo. (*Makofi*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, ningeomba unisikilize kidogo halafu ndio unikatalie mwisho kama itawezekana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Manyanya, tafadhali kaa chini.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 34

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 35
Ibara ya 36

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 37

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 51

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 52

MHE. BASIL P. MRAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nauliza tu kwamba; Waziri haioni kuwa ingefaa zaidi kama kwenye *regulations* angeweka kile kifungu cha kuelekeza namna makampuni yatakayokuwa yameandikishwa au watu binafsi watakaokuwa wameandikishwa kufundisha kutoa fursa za kufundisha vijana kuwapa *practical experience apprenticeship;* si vema ikaingizwa hiyo kwamba Waziri atakuwa na madaraka hayo badala ya kuiachia Bodi; na hiyo ingekuwa kwenye kifungu

cha 52 au kwenye *schedule* au *regulations* nyingine lakini hapa labda ingefaa *unless* yeye atasema kuna mahali pengine itafaa zaidi lakini iwekwe kabisa kwenye Muswada maana haionekani mahali popote?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kwamba, Mheshimiwa Waziri atatumia mamlaka yale ambayo yako kwenye 52(2)(f) kwa ujumla, kwa sababu siyo rahisi kuweka kila kitu katika sheria. Ahsante.

MHE. BASILI P. MRAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio nielewe kwamba Waziri atakuja kuweka kipengele hicho kwenye 2(f)? Mimi nataka hii habari ya *apprenticeship* itamkwe kabisa mahali.

MWENYEKITI: Nadhani kama tutakuwa tumemuelewa vizuri Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ni kwamba, Mheshimiwa Waziri atatumia Kifungu cha 2(f) ambacho kinasema: *"Any other matter which is reasonable and in accordance with the laws regulating architecture or quantity surveying in the country."* Kwa hiyo, watatumia kipengele hicho kwa ajili ya kuweka hiyo ambayo unaitaka.

Mheshimiwa Mramba, unaonekana hujaridhika au nimpe Mheshimiwa Waziri?

MHE. BASILI P. MRAMBA: Mimi nilitaka hiyo dhana iwekwe kabisa kama kifungu pekee kisimame chenyewe kwamba, Waziri atasimamia na iwekwe kwa namna tu ilimradi hili suala la *apprenticeship* liwekwe hapa, lakini lisimame lenyewe kwa sababu kifungu kile Waziri asipofanya hakuna mahali tutakapokuja kumuuliza hicho cha (f).

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa umuhimu ambao Mheshimiwa Basili Mramba ameuweka katika kujengea uwezo wataalam wetu ndani. Napokea hilo wazo. Niseme kwamba, kwa vile itakuwa vigumu sana kui-*fit* hapa kwenye kifungu hiki, basi kwenye kanuni ambazo nitaziandaa kwa ajili ya utekelezaji nitaweka kifungu hicho cha elimu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mramba, unaonekana umeridhika.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 53

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 54

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 55

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 56

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Jedwali la 1
Jedwali la 2

(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

(Bunge lilirudia)

Muswada wa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa Mwaka 2009 *(The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Bill, 2009)*

(Kusomwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imepitia Muswada wa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa Mwaka 2009 *(The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Bill, 2009),* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Hivyo, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada huu sasa ukubaliwe rasmi na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mpaka hapo, tutakuwa tumekamilisha ule utaratibu wa kupitisha hii Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo. Kwa kuwa kwenye *Order Paper* hatuna shughuli nyingine yoyote inayoendelea, kabla sijaahirisha Bunge nitoe tangazo.

Nimetakiwa niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kuna marekebisho yamefanyika kwenye ratiba ya shughuli za Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge, kwa hiyo, natumaini mtagawiwa ratiba mpya wakati wowote, ziko kwenye *process* zimekwenda kutolewa *photocopy* ili muweze kuona mabadiliko yaliyojitokeza.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hayo machache, nawashukuru sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kuweza kupitisha Muswada wake. Kwa kuwa hatuna shughuli inayoendelea, napenda sasa nichukue nafasi hii kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 11.58 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 2 Februari, 2010 Saa Tatu Asubuhi)